

**DHIMA YA LUGHA TEULE KATIKA KUWASILISHA  
TASWIRA YA MTOTO KATIKA JAMII YA ABAGUSII**

**TASNIFU**

**YA**

**ROBERT OMUGA OMBAYE**

**C50/CE/14559/2009**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**2018**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawaasilishwa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote au kuwasilishwa kwa mbinu yoyote ile ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa niaba yake.

**ROBERT OMUGA OMBAYE – C50/CE/14559/2009**

**(MTAHINIWA)**

Sahihi\_\_\_\_\_ Tarehe\_\_\_\_\_

Tunathibitisha kwamba kazi ambayo imetolewa katika tasnifu hii ni ya mtahiniwa aliyoifanya kwa kufuatilia maelekezo yetu kama wasimamizi wake walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**DKT. PAMELA M. Y. NGUGI**

**IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

Sahihi\_\_\_\_\_ Tarehe\_\_\_\_\_

**DKT. JOSEPH N. MAITARIA**

**IDARA YA LUGHA NA FASIHI CHUO KIKUU CHA KARATINA**

Sahihi\_\_\_\_\_ Tarehe\_\_\_\_\_

## **TABARUKU**

Tasnifu hii naitabaruku kwa mke wangu mpendwa Christine Nyaboke kwa kunifaa kwa hali na mali. Pili, wanetu Janet Nyanchama, Naomi Osebe, Enock Ondieki na Caleb Nyagwansa kwa uvumilivu wao wakati sikuweza kutekeleza majukumu yangu nilpokuwa masomoni. Pia, naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu Anderson Ombaye na Milkah Gesare kwa vile waliikita hamu ya masomo ndani yangu tangu utotoni pamoja na akraba zangu Caren Moraa, marehemu Joyce Nyatichi, marehemu Gladys Nyang'ara, Teresa Kwamboka, Rose Kerubo, Rispa Kemuma, Wilfred Maturu, Dickson Mocha na Irene Kemunto kwa ushauri wao wa dhati ulionitia moyo hadi kukamilisha kazi hii. Sitawasahau marehemu baba mkwe Peterson Ndege na mama mkwe Wilkister Nyabika na shemeji zangu Mike Nyakwana, marehemu Alice Moraa, Gilbert Tai, Pamela Monyangi, Naftal Gesembe, Benard Nyangena, Glanis Nyanduko, Keith Boko, Geoffrey Gisiora na Philis Nyanchama kwa mawaidha yao ya kila mara nilipokuwa masomoni.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukururu Maulana aliyenipa uhai, afya, hekima, uwezo na nguvu za kuifanya kazi hii. Pili, nawashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Pamela Ngugi na Dkt. Joseph Maitaria kwa jitihada zao za kunishauri, kuniongoza na kunipa moyo wa kuifanya kazi hii. Tatu, shukrani kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunifunza na kunipa motisha ya kufanya utafiti huu. Nne, shukrani kwa wakutubi wa maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa msaada wao wakati nilihitaji vitabu, kumbukumbu, ripoti, tasnifu, makala na majalida kuhusu mada ya utafiti.

Tano, sitasahau kuwashukuru wazamili wenzangu hususan Leah Mwangi, Justus Muusya, Walter Webukha, Angela Kilonzo, Millicent Onyango, Daniel Khaemba, Nehemiah Kiplang'at, Andrew Mwirabua, Hilda Masiolo, Japhet Mwenda, Joel Lomatolo, Margret Shiholo, Joyce Muema, Peter Ndwiga, Joseph Makau, Franklin Mucee, Josephine Muthoni, Rachel Otieno, Ezekiel Imbiakha na Martha Aberi kwa ushirikiano wao wakati wa masomo yetu, tulitiana shime hadi kufikia kiwango hiki.

Sita, shukrani za dhati zinawaendea mke wangu Christine Nyaboke pamoja na watoto wetu Janet Nyanchama, Naomi Osebe, Enock Ondieki na Caleb Nyagwansa kwa kuniombea, kunishauri, kunitia moyo na kuwa wavumilivu. Mlinipa utulivu na amani inayostahili nilipokuwa masomoni, msaada wenu haukadiriki. Mwisho, nawashukuru wazazi wangu, Anderson Ombaye na Milkah Gesare, kwa kunizaa, kunilea, kunipeleka shuleni, kunipa maoni ya busara na kunihimiza wakati wote kufanya bidii. Nawaombea Mungu awabariki, awalinde na kuwaongezea siku maishani mwenu.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kutambua lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto na kubainisha dhima na athari zake katika jamii ya Abagusii. Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano iliyoasisiwa na Hymes (1964) ilitumika katika utafiti huu. Nadharia hiyo ilifaa kwa sababu ilianguzia jinsi mawasiliano yalivyochanganuliwa kwa kuzingatia vipengele vya: mada, umbo la ujumbe, muhtadha, wahusika, sababu za mawasiliano, kanuni za ufafanuzi wa ujumbe, njia za mawasiliano na utendaji. Data ya kimsingi ilipatikana kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Ugatuzi Mdogo wa Kisii ya Kati, Kaunti ya Kisii. Aidha, data nyingine ilikusanywa maktabani kwa kusoma vitabu, kumbukumbu, ripoti, tasnifu, makala na majalida kuhusu mada ya utafiti. Nyanjani mtafiti alitumia sampuli iliyoteuliwa kwa kutumia mbinu ya kimakusudi kuwahoji watu sabini na wawili. Mbinu ya makusudi ilitumiwa kupata watafiti waliomudu vyema lugha ya Ekegusii kuhojiwa ili kupata matokeo faafu. Mtafiti aliwahoji watu wawili (2) kutoka kila kikundi; watoto, vijana, watu wazima, naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto kutoka wodi sita (6) za eneo bunge la Nyaribari Chache. Vifaa vilivyotumiwa kuwahoji ni hojaji wazi na maswali ya mahojiano ya ana kwa ana na wahojiwa. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo na nadharia ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa kutumia maelezo na yalibainisha kuwa, lugha hasi na chanya ilitumika katika kuwasilisha taswira mbalimbali za watoto katika jamii ya Abagusii. Matokeo ya utafiti huu vilevile yalibainisha kuwa dhima za lugha hiyo ni: kuelimisha, kukuza maadili, kuonya, kurekebisha tabia, kuwasiliana, kutia motisha, kusifu, kufariji, kulinganisha, kushauri na kukemea. Aidha, matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa lugha hiyo ilizua athari kadhaa kwa mtoto ambazo ni: kuhama kutoka nyumbani kwao, kutelekezwa, kubaguliwa, kukata tamaa, kuchanganyikiwa akili, kuwa na tabia nzuri au mbaya, kupendwa, kukubalika na kufurahi. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa katika jamii ya Abagusii kwa vile uliwawezesha kuelewa kuhusu lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto. Ufahamu wa lugha hiyo ni muhimu kwa vile ulichangia katika kuamua maisha ya mtoto siku za usoni. Aidha, ufahamu huo ulichangia pakubwa katika utoaji wa mielekeo, maoni na matendo ya watu wazima kwa watoto katika jamii ya Abagusii.

## **ABSTRACT**

This research was intended to examine the importance of the language that is used to portray the image of the child in the Abagusii community. The objectives of this research were to investigate the language that was used to portray the images of children and identify its importance and effects in the Abagusii community. This research was guided by the theory of Ethnography of Communication that was advanced by Hymes (1964). This theory was appropriate because it focuses on analyzing speech in any conversation using the following tenets: subject, style, context, characters, reasons of conversation, components, channels and acts. Data of this research was obtained from Nyaribari Chache Constituency, Kisii Sub County, Kisii County. The researcher also obtained more information on the research topic from the library where he read books, minutes, reports, texts and magazines on the research topic. In the field, the researcher used purposive sampling method to select seventy two (72) respondents. Purposive sampling method was appropriate because respondents who were well versed with Ekegusii language were selected to provide correct data for this research. The researcher interviewed two respondents from each group; children, youths, adults, assistant chiefs, chiefs and experts of rights of children from six (6) wards in Nyaribari Constituency. Tools used to obtain data were questionnaires and face to face interview with respondents. Data collected was recorded and analyzed using research questions, objectives and theory of this study. The results were presented using explanation method. The findings of this study revealed that negative and positive language was used to portray images of children in the Abagusii community. This study further revealed that the importance of using such language to children was to: educate, highlight values, warn, correct bad behavior, communicate, encourage, praise, comfort, compare, encourage and advise. The findings further showed that the effects of language that portrayed images of children in the Abagusii community were the child: running away from home, abandonment, segregation, discouragement, brain disturbances, obtaining good or bad behavior and feelings of being; loved, accepted and happy. The study concluded that language that portrayed images of children enabled Abagusii to understand childrens behavior. Such understanding is important because it contributed greatly in the adult's attitude, decisions and actions towards children in the Abagusii community.

## UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

**Lugha:** Huu ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa katika mawasiliano ya watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana. Katika utafiti huu, jamii ni ya Abagusii iliyotumia lugha ya *Ekegusii* katika kuwasiliana.

**Lugha teule:** Ni lugha iliyoteuliwa na mzungumzaji katika kuwasilisha jambo fulani.

**Dhima ya lugha:** Wajibu mkubwa pamoja na uwezo wa lugha wa kufanya jambo fulani.

**Athari za lugha:** Matokeo yaliyotokea kwa muda baada ya mtu kutumia lugha fulani.

**Mtoto:** Ni mwanadamu ambaye hajakomaa, ni kijana aliye chini ya ulinzi na udhamini wa mtu au watu wazima. Katika utafiti huu, mtoto ni binadamu mwenye umri mdogo wa miaka tisa hadi kumi na saba aliyetegemea mzazi au mtu mwingine mzima asiye mzazi amsaidie katika mahitaji yake ya kila siku.

**Taswira:** Picha iundwayo na maneno au udhahiri wa maelezo unaohusisha na kujumuisha dhana tofauti ndani ya dhana moja ili kuleta athari maalumu katika mawazo ya msomaji au msilkilizaji. Katika utafiti huu, taswira ni picha ya mtoto iliyotokea katika fikra au akili ya mzungumzaji.

## **ORODHA YA VIFUPISHO**

A.I.D.S:	Acquired Immune Deficiency Syndrome
C.R.C:	Convention on the Rights of the Child
H.R.W:	Human Rights Watch
I.L.O:	International Labour Organization
K.C.P.E:	Kenya Certificate of Primary Education
MOH	Ministry of Health
N.C.A.N.D.S:	National Child Abuse and Neglect Data System
U.K:	United Kingdom
U.K.I.M.W.I:	Upungufu wa Kinga Mwilini
U.N:	United Nations
U.N.H.C.R:	United Nations High Commissioner for Refugees
U.N.I.C.E.F:	United Nations International Children Educational Fund
V.V.U:	Virusi Vya Ukimwi
W.H.O:	World Health Organization



# YALIYOMO

## UKURASA

Mada-----	i
ikirari-----	ii
Tabaruku-----	iii
Shukrani-----	iv
Ikisiri-----	v
Ufafanuzi wa dhana muhimu-----	vii
Orodha ya vifupisho-----	viii
Yaliyomo-----	ix

## **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI----- 1**

1.0 Usuli wa mada-----	1
1.1 Suala la utafiti-----	5
1.2 Maswali ya utafiti-----	5
1.3 Malengo ya utafiti-----	6
1.4 Sababu za kuchagua mada-----	6
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti-----	7
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada-----	8
1.7 Misingi ya nadharia-----	14
1.8 Mbinu za utafiti-----	19
1.8.1 Eneo la utafiti-----	19
1.8.2 Uteuzi wa sampuli-----	20

1.8.3 Ukusanyaji wa data-----	21
1.8.4 Uchanganuzi wa data-----	22
1.8.5 Uwasilishaji wa data-----	23
1.9 Hitimisho-----	23

**SURA YA PILI: LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO KATIKA  
JAMII YA ABAGUSII-----24**

2.0 Utangulizi-----	24
2.1 Lugha hasi iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii-----	26
2.1.1 Mtoto aliyekuwa mgonjwa-----	26
2.1.2 Mtoto aliyekuwa mlemavu-----	28
2.1.3 Mtoto aliyekuwa yatima-----	31
2.1.4 Mtoto aliyeshi katika mazingira ya umaskini-----	34
2.1.5 Mtoto aliyetutumia pombe na dawa za kulevya-----	36
2.1.6 Mtoto aliyekuwa mwizi-----	39
2.1.7 Mtoto aliyefanya uasherati-----	41
2.1.8 Mtoto aliyewatusi watoto wengine-----	43
2.1.9 Mtoto aliyepigana na watoto wengine-----	45
2.1.10 Mtoto aliyekuwa zeruzeru-----	47
2.1.11 Mtoto aliyekuwa mzembe-----	49
2.1.12 Mtoto aliyeoa au kuolewa-----	50
2.1.13 Mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu-----	53
2.1.14 Mtoto aliyetelekezwa-----	56

2.2 Lugha chanya iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii-----	59
2.2.1 Mtoto aliyekuwa na kipaji maalumu-----	60
2.2.2 Mtoto aliyekuwa na furaha-----	62
2.2.3 Mtoto aliyekuwa na nidhamu-----	65
2.2.4 Mtoto aliyekuwa na afya-----	67
2.2.5 Mtoto aliyekuwa na bidii-----	69
2.2.6 Mtoto aliyekuwa na ujasiri-----	70
2.2.7 Mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri-----	72
2.2.8 Mtoto aliyependa kucheza-----	74
2.3 Hitimisho-----	75

**SURA YA TATU: DHIMA ZA LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO  
KATIKA JAMII YA ABAGUSII-----77**

3.0 Utangulizi-----	77
3.1 Kuelimisha-----	78
3.1.1 Kumwelimisha mtoto kuhusu tabia-----	79
3.1.1.1 Kumwelimisha mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya-----	79
3.1.1.2 Kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kuwapenda watoto wengine-----	80
3.1.2 Kumwelimisha mtoto jinsi ya kufanya kazi-----	81
3.1.2.1 Kumwelimisha mtoto kufanya kazi bila kunung'unika-----	81
3.1.2.2 Kumwelimisha mtoto kufanya kazi kwa bidii-----	82

3.1.2.3 Kumwelimisha mtoto kuwa na ari ya kufanya kazi-----	83
3.1.3 Kumwelimisha mtoto umuhimu wa kutia bidii katika masomo-----	84
3.1.3.1 Kumwelimisha mtoto jinsi ya kufaulu mitihani na kuendeleza masomo-----	84
3.1.3.2 Kumwelimisha mtoto umuhimu wa kuwasaidia watoto wengine kuendeleza masomo-----	85
3.1.3.3 Kumwelimisha mtoto mambo muhimu ya kuzingatia ili kufaulu mitihani-----	86
3.2 Kukuza maadili-----	87
3.2.1 Uaminifu-----	87
3.2.2 Nidhamu-----	89
3.2.3 Upendo-----	89
3.3 Kuonya-----	90
3.3.1 Kumwonya mtoto asiibe-----	91
3.3.2 Kumwonya mtoto asitumie pombe na dawa za kulevya-----	92
3.3.3 Kumwonya mtoto asiwe jambazi-----	93
3.3.4 Kumwonya mtoto asiwatusi watoto wengine-----	94
3.4 Kurekebisha tabia-----	95
3.4.1 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyefanya uasherati-----	96
3.4.2 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyekuwa mzembe-----	96
3.4.3 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyekosa nidhamu-----	97
3.5 Kuwasiliana-----	98
3.5.1 Kuwasiliana kuhusu majukumu ya mtoto-----	99

3.5.2 Kuwasiliana kuhusu maadili-----	100
3.5.3 Kuwasiliana kuhusu vipawa vya mtoto-----	101
3.6 Kutia motisha-----	102
3.6.1 Kumtia mtoto motisha ya kufanya kazi kwa bidii-----	102
3.6.2 Kumtia mtoto motisha ya kuwa na tabia nzuri-----	103
3.6.2.1 Kumtia mtoto motisha ya kuwaheshimu watoto wengine-----	104
3.6.2.2 Kumtia mtoto motisha ya kuwapenda watu wengine-----	104
3.6.3 Kumtia mtoto motisha ya kupata nafuu-----	105
3.7 Kusifu-----	106
3.7.1 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu-----	107
3.7.1.1 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuimba-----	107
3.7.1.2 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuchora-----	108
3.7.2 Kumsifu mtoto aliyetenda mema-----	109
3.7.2.1 Kumsifu mtoto aliyefaulu katika mitihani-----	109
3.7.2.2 Kumsifu mtoto aliyewasaidia watu-----	110
3.8 Kufaraji-----	111
3.8.1 Kumfaraji mtoto aliyeteswa-----	111
3.8.2 Kumfaraji mtoto aliyekuwa mgonjwa-----	112
3.8.3 Kumfaraji mtoto aliyekuwa yatima-----	113
3.8.4 Kumfaraji mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu-----	114
3.8.5. Kumfaraji mtoto aliyefiwa-----	115
3.9 Kulinganisha-----	116
3.9.1 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia tabia zao-----	116

3.9.2 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia bidii zao-----	117
3.9.3 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia afya zao-----	118
3.9.4 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia mazingira waliyoishi-----	119
3.10 Kushauri-----	120
3.10.1 Kumshauri mtoto kuwa na nidhamu-----	120
3.10.2 Kumshauri mtoto kutia bidii katika masomo-----	121
3.11 Kukemea-----	122
3.11.1 Kumkemea mtoto mzembe-----	122
3.11.2 Kumkemea mtoto mwizi-----	123
3.11.3 Kumkemea mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya-----	124
3.11.4 Kumkemea mtoto aliyewatusi watoto wengine-----	125
3.11.5 Kumkemea mtoto aliyepigana na watoto wengine-----	126
3.11.6 Kumkemea mtoto aliyeoa au kuolewa-----	127
3.12 Hitimisho-----	127

**SURA YA NNE: ATHARI ZA LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO  
KATIKA JAMII YA ABAGUSII-----129**

4.0 Utangulizi-----	129
4.1 Kuhama-----	131
4.1.1 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi katika mji-----	131
4.1.2 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi kwa jirani-----	132
4.1.3 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi katika makao ya watoto-----	133
4.1.4 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi kwa rafiki-----	134

4.2 Kutelekezwa-----	135
4.2.1 Mtoto zeruzeru aliyetelekezwa na wazazi wake-----	135
4.2.2 Mtoto mlemavu aliyetelekezwa na wazazi wake-----	136
4.2.3 Mtoto mgonjwa aliyetelekezwa na wazazi wake-----	137
4.3 Kubaguliwa-----	138
4.3.1 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia bidii-----	139
4.3.2 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia mazingira aliyoishi-----	139
4.3.3 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia matokeo ya mitihani-----	140
4.4 Kukata tamaa-----	140
4.4.1 Mtoto aliyekata tamaa ya kuishi-----	140
4.4.2 Mtoto aliyekata tamaa ya kuendeleza masomo-----	141
4.4.3 Mtoto aliyekata tamaa ya kupona-----	142
4.5 Kuchanganyikiwa akili-----	143
4.6 Tabia mbaya-----	145
4.6.1 Mtoto aliyekuwa na tabia nzuri aliyeamua kuwa na tabia mbaya-----	145
4.6.2 Mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini aliyeamua kuwa mwizi----	146
4.7 Kupendwa-----	147
4.8 Kukubalika-----	148
4.8.1 Mtoto aliyekubalika katika familia-----	148
4.8.2 Mtoto aliyekubalika katika jamii-----	149
4.9 Kufurahi-----	150
4.9.1 Mtoto aliyefurahi kwa kufaulu katika mitihani-----	150
4.9.2 Mtoto aliyefurahi kwa kuwa na nidhamu-----	151

4.10 Tabia nzuri-----	152
4.10.1 Mtoto aliyerudi nyumbani kwao baada ya kuolewa-----	152
4.10.2 Mtoto aliyeacha tabia ya kuiba-----	153
4.10.3 Mtoto aliyeacha tabia ya kupigana na watoto wengine-----	155
4.10.4 Mtoto aliyeacha tabia ya kutumia pombe na dawa za kulevya-----	156
4.11 Hitimisho-----	157

**SURA YA TANO: HITIMISHO-----158**

5.0 Utangulizi-----	158
5.1 Muhtasari-----	158
5.2 Matokeo-----	161
5.3 Changamoto-----	164
5.4 Mchango-----	165
5.5 Mapendekezo-----	166

**MAREJELEO-----168**

**VIAMBATISHO-----175**

**KIAMBATISHO CHA 1-----175**

Maswali ya mahojiano nyanjani kwa watu wazima kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii-----	175
--	-----



**KIAMBATISHO CHA 2-----176**

Maswali ya mahojiano nyanjani kwa naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii-----176

**KIAMBATISHO CHA 3-----177**

Maswali ya mahojiano nyanjani kwa watoto na vijana kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii-----177

**KIAMBATISHO CHA 4-----178**

Hojaji kwa watoto, vijana, watu wazima, naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii-----178

**KIAMBATISHO CHA 5-----181**

Ramani ya Kenya inayoonyesha Kaunti ya Kisii-----181

**KIAMBATISHO CHA 6-----182**

Ramani ya Kaunti ya Kisii-----182

**KIAMBATISHO CHA 7-----183**

Ramani ya maeneo bunge katika Kaunti ya Kisii-----183

**KIAMBATISHO CHA 8-----184**

Ramani ya eneo bunge la Nyaribari Chache-----184

**KIAMBATISHO CHA 9-----185**

Ramani ya wodi katika eneo bunge la Nyaribari Chache-----185

**KIAMBATISHO CHA 10-----186**

Ramani ya mitaa midogo katika eneo bunge la Nyaribari Chache-----186

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.0 Usuli wa mada

Watoto huwa na taswira mbalimbali ambazo wanajamii hupenda kuzifahamu. Zipo njia nyingi zimetumika katika kuwafahamisha wanajamii hao kuhusu taswira hizo. Njia hizo za kuwasilisha taswira hizo ziliwawezesha wanajamii kumtofautisha mtoto mmoja kutoka kwa mwingine. Watoto waliozungumziwa walipewa taswira kwa kutegemea tabia, maumbile au mazingira yao katika jamii. Kwa mfano iwapo mzazi alinua kuwasilisha taswira ya mtoto wake katika jamii, alitumia njia ya mawasiliano kufanya hivyo. Kwa mujibu wa Beeman (1977) mawasiliano ni tendo la kuarifu au kubadilishana mawazo, hisia, maoni na habari kwa usemi, uandishi au ishara nyinginezo. Mawasiliano ni mfanyiko unaolenga kuwasilisha ujumbe miongoni mwa viumbe kwa nia ya kubadilisha tabia na mienendo ya wahusika wote kwenye mfanyiko huo. Anachomaanisha Beeman ni kuwa si binadamu pekee ambao huwasiliana, japo mawasiliano kati ya binadamu ni bayana yakilinganishwa na yale ya viumbe wengine. Pia, anaeleza kuwa mawasiliano hulenga kuathiri wanaoshiriki kwenye mchakato huo.

Dhana hii ya mawasiliano imefafanuliwa pia na Lyons (1977) anayeieleza kama uwasilishaji wa ujumbe kwa kutumia mfumo fulani wa uashiraji. Mawasiliano hivyo basi huwasilishwa kwa ishara zinazounda mfumo fulani. Matumizi ya ishara katika mawasiliano yamerejelewa na Berelson na Steiner (1969). Wawili hawa wamefafanua mawasiliano kama kule kuwasilisha ujumbe, maoni, hisia, ufundi na mengineyo kwa kutumia ishara. Wanataja maneno, picha, michoro na majedwali kama baadhi ya ishara zitumikazo kwenye

mawasiliano. Naye Finnegan (2002) ameeleza kuwa mawasiliano hujumuisha namna zote za mahusiano na maisha ya binadamu kupitia kwa kusikia, kunusa, kugusa, kuona, kuonja, mwendo na hata vifaa halisi. Kama anavyosisitiza Finnegan, binadamu huwasiliana wakati wote, hata wakati ambao hawakusudii kuwasiliana. Hisia zote sita pamoja na hata vifaa mbalimbali hutumika ili kuwasiliana kwa ufanisi.

Mawasiliano kufanyika katika jamii sharti wanajamii watumie mfumo wa lugha. Kama anavyoeleza Lyons (1977), lugha ndiyo mfumo unaotumiwa sana na binadamu kuwasiliana, japo kuna mifumo mingine. Kwa mujibu wa Morreale (2004) lugha ni mfumo wa ishara za kiusemi unaomwezesha binadamu kubuni taarifa na matamashi kwa maneno na kufasiri maana yake. Ishara hizi za kiusemi zinaweza kuandikwa au kutamkwa. Mifumo mingine inayotumika katika mawasiliano ni ishara zisizo za kiusemi ambazo hujumlisha sauti za kutamkwa, matendo, ishara za mikono, miondoko na misogezo ya mwili, na hata vifaa halisi ambavyo wanajamii hukubaliana kuwa vina maana. Tendo la usemi aghalabu huandamanishwa na ishara mbalimbali kama vile za uso, msogezo wa mwili pamoja na sifa za sauti kama vile kupasa sauti kwa kasi au kubadilisha toni katika utamkaji. Ili kuwasilisha ujumbe kikamilifu, ishara zisizo za kiusemi ni lazima ziwepo (Liles, 1975). Kadhalika, Leathers (1997) anaeleza kuwa mawasiliano hufanikiwa zaidi yakihusisha ishara zisizo za kiusemi.

Jamii ya Abagusii hutumia lugha ya Ekegusii ambayo ni mojawapo ya lugha za Kibantu katika kuwasiliana. Dhima za lugha hiyo ni kuwa inawatambulisha kama mojawapo ya jamii zinazoishi nchini Kenya. Lugha hiyo vilevile inapotumika katika mawasiliano ya kila siku

baina ya wanajamii inawawezesha kuimarisha na kuendeleza imani, ibada na uhusiano wao na *Engoro* (mungu wao). Aidha, lugha hiyo inawawezesha Abagusii kutoa hisia na mawazo yao kwa watu wengine. Mawasiliano kwa kutumia lugha hiyo pia inawawezesha Abagusii kubariki, kulaani, kutukuza na hata kuonyesha chuki au mapenzi. Abagusii kadhalika hutumia lugha ya Ekegusii katika kueleza uhalisia wa mambo na kudhibiti ukweli kuhusu imani yao. Aidha, Abagusii hutumia lugha hiyo katika kueleza miiko ya jadi pamoja na mantiki au falsafa kuhusu maisha katika jamii.

Benedict (1976) na Korac (1983) wamebainisha kuwa lugha ni chombo muhimu katika jamii ambacho hutumika na wanajamii katika kuwasilisha hisia za mtu. Wataalamu hawa wanazidi kutueleza kuwa, lugha ni muhimu kwa vile hutumika kueleza kuhusu tabia ya mtu na jinsi atakavyoikuza katika maisha yake. Maoni ya wataalamu hawa yanaingiliana vyema na mtazamo wa jamii ya Abagusii kuwa wao hutumia lugha ya Ekegusii katika kumwelimisha mtoto kuhusu mambo kadhaa katika jamii kama vile mila, desturi, tabia na kazi. Aidha, lugha hiyo hutumika katika kumweleza mtoto kuhusu umuhimu wa kukuza maadili kama vile nidhamu, uaminifu na upendo walipokuwa wakitekeleza shughuli zao za kila siku kama vile kusoma, kucheza na kufanya kazi yoyote katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ya Ekegusii vilevile ilitumika katika kuwatahadharisha watoto kujiepusha kutenda vitendo viovu vilivyosababisha hasira, chuki na mafarakano katika jamii ya Abagusii. Lugha ya Ekegusii pia ilitumika katika kuwapa moyo watoto waliopitia changamoto mbalimbali kama vile maafa ya wazazi wao au unyanyasaji na uonevu na watu wazima katika jamii ya Abagusii. Watoto waliofanya vizuri katika jambo fulani kadhalika walisifiwa kwa kutumia lugha ya

Ekegusii kama njia mojawapo ya kutambua vipawa vyao na kuwahimiza kuzidisha kufanya vyema zaidi siku za usoni katika jamii ya Abagusii.

Lugha ya Ekegusii ndiyo iliyotumika katika mawasiliano ya kila siku katika jamii ya Abagusii kueleza kuhusu taswira mbalimbali za watoto zilizopatikana katika jamii ya Abagusii. Aidha, Abagusii hutumia lugha ya Ekegusii katika kutoa mwelekeo uliostahili kuzingatiwa na watoto ili kuboresha maisha yao katika jamii. Lugha ya Ekegusii vilevile ilipotumika katika mawasiliano ya kila siku, iliwawezesha Abagusii kutoa maelezo ya kina kwa wanajamii kuhusu taswira mbalimbali za watoto zilizopatikana katika jamii ya Abagusii. Lengo la kufanya hivyo ni kujenga mwingiliano wa lugha na taswira za watoto ili kuwawezesha Abagusii kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu watoto waliozungumziwa. Aidha, mawasiliano haya kwa kutumia lugha ya Ekegusii katika kueleza kuhusu taswira za watoto yaliwawezesha Abagusii kuweka mikakati iliyostahili kuzingatiwa na wanajamii wote katika kuboresha maisha ya watoto. Mikakati hiyo ilichangia katika kuondoa kila aina ya unyanyasaji na uonevu wa watoto ili nao wapate fursa nzuri ya kuimarika na kuwa wanajamii wema wenye kujali misingi ya utu.

Mtoto huwa na taswira ambayo ilimtambulisha kutoka kwa watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Taswira hiyo ni picha iliyotokea katika fikra ya mzungumzaji yeyote aliyemlea, kumtunza na kumshughulikia mtoto katika maisha yake ya kila siku. Waliomzungumzia mtoto hasa walihakikisha kuwa alipokea mahitaji yake ya kila siku. Waliotumia lugha ya Ekegusii hasa katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni wale walioishi naye kama vile wazazi, walezi na marafiki zake. Watoto katika jamii ya Abagusii walikuwa

na taswira mbalimbali zilizozungumziwa na wanajamii kwa kutumia lugha ya Ekegusii kwa lengo la kufafanua kwa kina kuhusu tabia zao. Kadhalika, imebainika wazi kuwa japo jamii ya Abagusii imetumia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto kwa miaka mingi katika mawasiliano yao ya kila siku, haijafanyiwa utafiti wa kina kubaini ni ya aina gani, dhima na athari zake ni zipi. Hivyo basi, utafiti huu umenuia kujaza pengo hilo na kuendeleza taaluma ya isimu-jamii hasa uwanja wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii.

### **1.1 Suala la utafiti**

Ingawa wataalamu mbalimbali wameshughulikia namna lugha inavyotumika katika jamii, imebainika wazi kuwa kulingana na udurusu wa awali wa mtafiti, lugha iliyotumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto alipokua katika jamii haijafanyiwa utafiti wa kina, hususan katika jamii ya Abagusii. Hali hii ilidhihirisha kuwepo kwa pengo katika lugha. Hivyo basi, utafiti huu ulidhamiriwa kujaza pengo hilo kwa kubainisha aina ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Aidha, dhima na athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii zimebainishwa katika utafiti huu.

### **1.2 Maswali ya utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- (i) Ni aina gani ya lugha hutumiwa katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii?
- (ii) Lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii inapotumika ina dhima gani?

(iii) Athari za matumizi ya lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni zipi?

### **1.3 Malengo ya utafiti**

Utafiti huu umetimiza malengo yafuatayo:

- (i) Kutambua lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
- (ii) Kubainisha dhima za lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
- (iii) Kuchunguza athari za lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

### **1.4 Sababu za kuchagua mada**

Utafiti huu utasaidia katika kuelewa kuhusu maisha ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Ufahamu huo ni muhimu kwa vile utasaidia katika kujenga na kuamua maisha yake siku za usoni. Aidha, utafiti huu utasaidia jamii ya Abagusii kuelewa jinsi lugha inayowasilisha taswira ya mtoto inavyochangia katika utoaji wa mielekeo, maoni na mambo anayotendewa na watu wengine wanaoishi naye. Utafiti huu pia, utasaidia katika kufahamu kuhusu maisha ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu vilevile utasaidia katika kutambua lugha inayowasilisha taswira mbalimbali za watoto zinazopatikana katika jamii ya Abagusii. Ufahamu huo wa mapema ni muhimu kwa vile utachangia katika wanajamii kumkubali mtoto aliyekuwa na taswira hiyo maishani mwake. Aidha, utafiti huu utasaidia katika kutafuta masuluhisho ya baadhi ya matatizo ya mtoto yanayosababishwa na matumizi ya lugha inayowasilisha taswira yake katika jamii ya Abagusii. Masuluhisho hayo yanapotambuliwa mapema yatawawezesha Abagusii kuweka mikakati inayostahili kutumika katika kuboresha maisha ya mtoto katika jamii.



Aidha, utafiti huu utawachochea Abagusii kuibuka na mikakati ya kuboresha maisha ya mtoto ili nao waweze kuwa watu wanaowajibika katika maisha yao siku zijazo. Utafiti kuhusu lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii vilevile utawawezesha Abagusii kugundua mapengo ambayo bado yapo katika masuala ya mtoto na yakishughulikiwa yanaweza kuimarisha maisha yake katika jamii. Utafiti huu kadhalika, utachangia katika kuongezea hazina ya maandishi yanayohusu taaluma ya isimu-jamii. Aidha, utafiti huu utatoa changamoto kwa wasomi wa isimu-jamii wa kizazi hiki kuwa na uchu wa kufanya tafiti zaidi katika taaluma hiyo. Mawanda mengi ambayo hayajatafitiwa yataweza kudhihirishwa na kuwekwa bayana kwa wasomi chipukizi ili waweze kufanya tafiti zaidi. Hali hii itawezesha taaluma ya isimu-jamii kupiga hatua na kuimarika zaidi. Fauka ya hayo, utafiti huu utakuza na kunufaisha viwango vya wasomi wa lugha ya Ekegusii na lugha nyinginezo katika kupata tajiriba pana kuhusu matumizi ya lugha kwa mtoto katika jamii. Ufahamu huo ni muhimu kwa vile utawawezesha wasomi hao kuibuka na sheria ambazo zinastahili kufuatwa na wanajamii ili kufanikisha mawasiliano kwa mtoto katika jamii ya Abagusii na jamii nyinginezo.

### **1.5 Upeo na mipaka ya utafiti**

Utafiti huu ulichunguza lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto. Kuna vipengele tofautitofauti vya lugha ambavyo ni aina, dhima, ufaafu, athari na matamshi. Utafiti huu ulijikita katika aina ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto, dhima na athari zake. Mtafiti hakujihusisha na matamshi na ufaafu wa lugha hiyo. Aidha, utafiti huu ulijikita katika jamii ya Abagusii kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache linalopatikana katika ugatuzi mdogo wa Kisii ya Kati, Kaunti ya Kisii. Eneo bunge hilo lilichaguliwa kuwakilisha maeneo bunge mengine

yaliyopatikana katika jamii ya Abagusii kama vile; Bobasi, Bomachoge, Bonchari, Bogirango ya Maate, Bogirango ya Rogoro, Bogetutu na Nyaribari Masaba. Eneo bunge la Nyaribari Chache vilevile liliateuliwa kuwakilisha jamii pana ya Abagusii iliyoishi katika Kaunti za Kisii na Nyamira. Utafiti huu vilevile ulijikita katika mada ya mazungumzo, umbo la ujumbe, muktadha wa mazungumzo, sababu za mawasiliano na mazingira mawasiliano yalifanyika.

### **1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Wataalamu kadhaa wametafiti kuhusu suala la lugha na taswira ya mtoto katika jamii. Marcia (2011) alitafiti kuhusu taswira ya mtoto kule Uingereza. Alidai kuwa watu wakubwa yaani, wazazi na walimu wana taswira fulani kumhusu mtoto na yote yanayomzunguka ambayo yalijumuisha jinsi alivyobuni, alivyoamua, alivyoachagua, alivyoibua mbinu za kuteka mawazo yao na kuwa na mafundisho yao kupitia kwa njia ya kugusa, kutafiti, kuuliza maswali, kujihusisha, kutazama, kushiriki, kusikiliza, kujadiliana na kuweka pamoja vitu vyote katika mazingira alimoishi. Marcia alizingatia suala la taswira alizopewa mtoto pekee katika jamii tofauti na utafiti huu ambao ulishughulikia taswira za mtoto pamoja na lugha iliyotumika katika kuwasilisha taswira hizo katika jamii ya Abagusii.

Kunkel na Smith (1999) nao walichunguza kuhusu lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika vyombo vya habari kule Marekani. Wataalamu hawa walibainisha kuwa taswira ya mtoto tangu kuzaliwa kwake ilitegemea mazingira, lugha, sheria na sera zilizohusu mtoto katika taifa husika. Watafiti hawa walishughulikia taswira ya mtoto katika vyombo vya habari kama vile runinga, redio na magazeti yaliyochapishwa kila siku. Aidha, Jelana na

Korac (2003) walibanisha kuhusu lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika vyombo vya habari ambavyo vilitawaliwa na watu wazima. Walibainisha lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika redio, runinga, magazeti na majarida katika eneo la Serbia. Aidha, walidhihirisha kuwa lugha hiyo iliwasilisha taswira za watoto waliodunishwa vilevile za uwongo katika vyombo vya habari ambavyo vilitawaliwa na habari kuhusu watu wazima. Japo wataalamu hawa walishughulikia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika vyombo vya habari kule Marekani na Serbia, utafiti huu ni tofauti kwa vile ulishughulikia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Nao Jerop na Oyori (2002) walitafiti kuhusu majina na methali zilizotumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto mlemavu katika jamii za Abagusii na Nandi. Walibainisha kuwa mtoto mlemavu alistahili kushughulikiwa kama watoto wengine wasio na kasoro walivyoshughulikiwa. Aidha, walistahili kuheshimiwa na watu wote katika jamii. Walibainisha vilevile kuwa wakati mwingine watu walitumia lugha isiyostahili katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii. Walifafanua kuwa mtoto wakati mwingine alipewa taswira ya mnyama kama vile tumbili. Aidha, walidhihirisha kuwa majina kadhaa ya watoto walemavu yalikuwa na uhusiano na ulemavu wao, ingawa kuna majina mengine yaliyotumika kwa njia ya utani au kumsifu mtoto mlemavu. Ingawa watafiti hawa walishughulikia majina na methali zilizowasilisha taswira ya mtoto, utafiti huu ni tofauti kwa vile ulishughulikia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Mathalani, Aries (1962) alifafanua umuhimu wa taswira za watoto nchini Uingereza na umuhimu wa malezi mema kwa watoto katika jamii. Alieleza kuhusu taswira za watoto za

kusikitisha ambazo zilionyesha jinsi watoto walivyowasilishwa kama vinyago vya watu wazima; lakini baada ya muda mrefu pia, aliwaonyesha watoto kama sehemu ya familia, kisha baadaye akatengeneza sanamu ya mtoto peke yake. Kwa mintarafu ya mtafiti, mtoto alionyeshwa kama sanamu ya kutazamwa bila hiari yake. Mtoto hakuwa na usemi wowote katika jamii. Utafiti huu ulichangia katika kutambua taswira mbalimbali za mtoto zinazopatikana katika jamii ya Abagusii.

Bellamy (2002) ni mmoja wa watafiti waliochunguza taswira ya mtoto na tamaduni za karne ya ishirini katika nchi ya Kenya. Alichunguza namna taswira ya mtoto ilivyoubwa na kuakisiwa katika kazi za nathari za kisasa. Alidai kuwa watoto wengi katika jamii wamedhalilishwa na kuachwa nyuma na jamii iliyoendelea kwa kasi mno. Aidha, alishangaa kuwa vyombo vya habari havitoi uamuzi uliostahili kuhusu watoto kama vitu vya kuogofya au watu waliohitaji usalama, ni malaika au shetani. Mshangao wake ulichangia katika kuchochea mtafiti kushughulikia utafiti huu kuhusu lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii. Mtafiti huyo alishughulikia taswira ya mtoto katika vyombo vya habari, tofauti ni kuwa utafiti huu umejikita katika matumizi ya lugha kwa mtoto katika jamii ya Abagusii.

Ezra (2007) naye alitafiti kuhusu jinsi ya kuwatunza na kuwalea watoto katika jamii ya Abagusii. Alidai kuwa utamaduni wa jamii ya Abagusii ulichangia pakubwa katika kubainisha tabia za wazazi na watoto. Aidha, alibainisha kuwa watoto huzaliwa na wanakua katika mazingira yenye vielelezo na kanuni za kuwaongoza katika maisha yao yote. Alikuwa na mtazamo kuwa jamii ya Abagusii ni mahali ambapo mtoto aliweza kupata elimu. Aidha, alibainisha hatua muhimu ambazo mtoto hupitia katika maisha yake. Alichanganua kuhusu

mambo muhimu ambayo mtoto hufundishwa katika maisha yake. Utafiti huo ulitoa mchango mkubwa katika kufanikisha utafiti huu, japo ni tofauti kwa vile utafiti huu ulijikita katika lugha. Lugha iliyobainishwa ni ile iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Mtaalamu mwengine ambaye alishughulikia lugha iliyotumika na watoto ni Jay (1996). Alibainisha kuhusu lugha ya laana na matusi iliyotumika na watoto katika mawasiliano baina yao. Pia, alibainisha athari za lugha hiyo. Alidai kuwa jamii mbalimbali zina maoni tofautitofauti kuhusu lugha hiyo. Utafiti wa Jay ulikaribiana na huu ingawa tofauti ni kuwa utafiti wa Jay ulijikita katika lugha ya laana na matusi iliyotumiwa na watoto. Utafiti huu ulichanganua lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Waliotumia lugha hiyo hasa ni wazazi au wale waliowalea na kuwatunza watoto katika jamii. Hata hivyo utafiti huo ulisaidia katika kuelewa iwapo kuna uhusiano wowote kati ya lugha iliyotumiwa na watoto na ile iliyotumiwa na wazazi au walezi watoto katika jamii ya Abagusii.

Lyons (1977) ametafiti kuhusu lugha na jinsi inavyotumika katika jamii. Alidai kuwa lugha ni mfumo uliotumika sana na binadamu kuwasiliana, japo kuna mifumo mingine. Madai ya mtaalamu huyo yalifafanuliwa na Morreale (2004) kuwa lugha ni mfumo wa ishara za kusemi uliowawezesha binadamu kubuni taarifa na matamshi kwa maneno na kisha kufasiri maana yake. Ishara hizi za kusemi ziliweza kuandikwa au kutamkwa. Mifumo mingine iliyotumika katika mawasiliano ni ishara zisizo za kusemi ambazo zilijumlisha sauti zisizo za kutamkwa, matendo, ishara za mikono, miondoko na misogezo ya mwili na hata vifaa halisi ambavyo wanajamii walikubaliana navyo kuwa vina maana. Tafiti za wataalamu hawa zilishabihiana na utafiti huu kwani tafiti zote ziliangazia jinsi lugha ilivyotumika katika

jamii. Tofauti ni kuwa utafiti huu uliangazia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Lyons na Morreale walishughulikia jinsi lugha ilivyotumika katika jamii.

Benedict (1976) na Korac (1983) walibainisha umuhimu wa matumizi ya lugha katika kukuza tabia na mazingira alikoishi mtoto. Walieleza kuwa jinsi lugha ilivyoyumika na watu wakati mawasiliano yalifanyika ilijenga maisha ya mtoto katika jamii. Aidha, lugha hiyo ilitumika kubainisha tabia ya mtoto katika jamii. Nao Gudgeon (1991) na Phelan (2001) walipiga hatua kwa kuchunguza mambo yaliyozingatiwa wakati wa kuwashughulikia watoto na vijana katika jamii. Walieleza kuwa kazi hiyo ilikuwa ngumu yenye changamoto nyingi. Aidha, walisema kuwa kazi hiyo ilihitaji mtu kutumia lugha iliyoeleweka kwa urahisi. Sababu ni kuwa lugha hiyo ilitumika kama chombo cha kujenga uhusiano baina ya watoto au vijana na watu wazima. Vilevile walibainisha kuwa watoto na vijana bado walitegemea malezi kutoka kwa wazazi au watu wazima katika jamii. Aidha, Brown (2006) alibainisha lugha iliyostahili kutumika katika mawasiliano kwa watoto na vijana. Alidai kuwa lugha hiyo ilitegemea uhusiano uliokuwepo kati ya watoto, vijana na waliowatunza. Tafiti za Benedict, Korac, Gudgeon, Phelan na Brown zilishughulikia lugha iliyostahili kutumika kwa watoto na vijana. Tofauti ni kuwa utafiti huu umejikita katika lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Kunazo tafiti zilizokaribiana na utafiti huu kama wa Aries (1962) kule nchini Uingereza, alibainisha taswira za watoto kuwa ni viumbe dhaifu waliohitaji kulindwa na kurekebishwa kwa uadilifu na kupokea elimu ambayo ingewawezesha kuwa raia wema. Madai yake yaliungwa mkono na Pollock (1983) aliyedai kwamba waandishi wametoa mifano mingi ya

kuonyesha taswira za kikatili kwa watoto walipoadhibiwa. Vitendo vya aina hiyo vilistahili kulaumiwa na waandishi hao kama ukiukaji wa sheria. Bado hata hivi leo kuna watoto wengi katika jamii ambao wana taswira ya kudhalilishwa, kunyanyaswa na kuonyeshwa ukatili katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Pia, kuna mamilioni ya watoto ambao bado waliishi wakiwa na taswira ya umaskini katika bara Uropa na Marekani ambapo kuna utajiri mwingi (Ozment, 2001). Konner (1991) aliandika nathari akieleza taswira ya mtoto ambapo alihoji kwamba, tunaporejelea maisha yetu ya utotoni, ni maisha yaliyozungukwa na taswira mbalimbali zikiwemo za kuogofya na kikatili zilizosababishwa na watoto wenzao au watu wazima dhidi ya watoto. De Mause (1976) aliye mwandishi wa Kifaransa naye alifanya utafiti kuhusu taswira ya mtoto katika jamii. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa watoto wengi wamewahi tendewa ukatili tangu walipokuwa wadogo. Kihistoria, taswira hii ni ya kuhuzunisha, kwa vile watoto wengi hawana ulinzi mwema, hawasikilizwi wala kuheshimiwa. Hata katika jamii ya Abagusii kuna taswira za watoto ambazo ni za kuhuzunisha kwa vile waliteswa.

Utafiti huu ulikuwa tofauti na tafiti zilizofanywa awali kwa sababu zifuatazo: Kwanza, uliangazia kubainisha aina ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Pili, ulichunguza dhima na athari za lugha katika jamii ya Abagusii. Kulingana na udurusu wa mtafiti, tafiti za awali hazijashughulikia suala la aina, dhima na athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii. Utafiti huu hivyo basi, ulijaza pengo hilo na hivyo kuendeleza taaluma ya Kiswahili hasa kipengee cha matumizi ya lugha katika jamii.

## 1.7 Misingi ya nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano iliyoasisiwa na Hymes (1964). Alianzisha nadharia hii katika miaka ya sitini pale ambapo wanaanthropolojia, wanasosholojia na wanaisimu walitafiti matumizi ya lugha katika jamii mbalimbali huku wakizingatia jinsi wanajamii walivyotumia kipengele cha lugha kama kiini chao katika uchunguzi. Aidha, alifanya utafiti kuhusu uhusiano uliopo kati ya lugha na utamaduni kisha akauita mtazamo huo 'Ethnografia ya Mawasiliano'. Mwaka wa 1962, aliwasilisha makala ya 'Ethnografia ya Uzungumzi'. Miaka ya baadaye, kukazuka waandishi wengine kama vile Gumperz na Hymes (1972), Saville – Troike (1982), Wardhaugh (1986), Bauman (1989), Fasold (1990) na Spolsky (1998) walioiendeleza nadharia hii ya Ethnografia ya Mawasiliano. Ethnografia ya Mawasiliano ni mtazamo wa isimu jamii ambao hujikita katika vipengele vitatu vikuu; muktadha, utamaduni na mazingira katika jamii ili kuainisha lugha na matumizi yake. Mtazamo huu huchunguza namna tukio fulani katika jamii linavyoibusha matumizi maalum ya lugha ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Sapir (1949) alisadiki hayo alipoeleza kwamba matumizi ya lugha hayawezi kutenganishwa na utamaduni wa jamii yaani mila, desturi na itikadi ambazo ndizo zinazoamua na kuongoza maisha ya watu.

Hymes (1972, 1974) anabaini kuwa mawasiliano huwepo na kukamilika miongoni mwa wanajamii kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- (a) **Muktadha:** Aina ya tukio hupelekea kuwa na muktadha fulani. Kwa mfano, matumizi mahususi ya lugha hupata maana kwa kuzingatia muktadha wa maongezi katika jamii.



- (b) **Lugha:** Lugha inayotumika hutegemea mada inayozungumzwa na wanaohusika, kwamba jamii husika huelewa yale yanayoelezwa, wakati mwingine lugha inaweza kubadilika kwa vile kinachoelezwa huingia katika mada nyingine mpya kando na ile iliyokuwa inazungumziwa.
- (c) **Hadhira:** Kuzingatia hadhira lengwa, na hasa kwa misingi ya umri, uana, utabaka, elimu na uhusiano wa wahusika.
- (d) **Ujumbe:** Aina ya ujumbe unaodhamiriwa kuwasilishwa. Ujumbe huo unaweza kuwa wa moja kwa moja au wenye maana fiche. Kwa mfano, matumizi ya mafumbo au jazanda.
- (e) **Mwingiliano:** Taratibu zinazoambatana na mwingiliano. Hii ina maana kuwa katika mawasiliano lazima wanajamii kutilia maanani suala la utamaduni. Kwa mfano, nani anayeanza mazungumzo, wakati wa kunyamaza au kuuliza maswali.
- (f) **Mandhari:** Huwa na maana ya wakati, mahali pa tukio na mazingira.
- (g) **Ufafanuzi:** Taratibu zinazoambatana na ufafanuzi wa lugha. Misingi ya kitamaduni sharti ishirikishwe katika ufafanuzi wa matumizi ya miundo fulani ya lugha.
- (h) **Uwasilishaji:** Namna ya uwasilishaji. Uchaguzi wa uwasilishaji unaweza kuwa wa masimulizi ya mdomo, maandishi, kwa njia ya simu au njia nyinginezo zinazoweza kuwasilisha ujumbe. Masimulizi ya mdomo yanaweza kutumika kama vile kuimba, kuvuma, kupiga mluzi, kuimba kwa kusifia mtu au kitu pamoja na maongezi ya kawaida. Kwa mfano, ufafanuzi wa msemaji wa chifu, masimulizi ya wanyama, mawaidha ya wanandoa wapya na kwa wanajamii ambao tabia zao si nzuri husemwa.
- (i) **Umbo:** Umbo la ujumbe huwasilishwa kwa njia mbalimbali kwa kutegemea ishara zinazotumika, maana ya ishara hizo, matamshi na pia lahaja husika.

Nadharia hii ilitumika kutathmini namna mbalimbali za mawasiliano baina ya watu wa kundi moja la jamii katika miktadha mbalimbali. Page (1985) anasema kuwa lugha huchukua sehemu muhimu ya kuwa na wajibu mchangamano ikilinganishwa na kuhusishwa na kundi maalumu la watu, kabila au taifa. Anazidi kudai kuwa matumizi ya lugha miongoni mwa kundi fulani la kijamii huwezesha jamii kuweka mipaka baina yao na makundi mengine ya kijamii. Mipaka hiyo ni ya kijiografia na lugha. Anadai kuwa jamii huweza kumiliki lugha na matumizi yake na kuitofautisha kabisa na lugha za jamii zingine.

Kulingana na Hymes (1964), sheria za mazungumzo ni njia ambazo kwazo mzungumzaji huhusisha namna mbalimbali za mazungumzo, ujumbe, miundo na maumbo ya lugha, mahali na shughuli mbalimbali. Anazingatia nadharia hii hujishughulisha na mitazamo na ufahamu wa watu wa kundi husika la kijamii badala ya kujihusisha na maana ya maneno na tabia za wanajamii. Kuna mihimili mbalimbali ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano kama ilivyopendekezwa na Hymes (1962, 1972, 1974, 1996). Mihimili hiyo ilikuwa nguzo muhimu ya kuzingatiwa katika utafiti huu. Mihimili hiyo ni:

- 1. Mada:** Ni jambo linalozungumziwa au linalojadiliwa. Maudhui ya ujumbe unaowasilishwa yanawezesha uchanganuzi wa mada inayozungumziwa. Mhimili huu utatumiwa katika kuchunguza mada ya utafiti kuhusu lugha inavyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
- 2. Umbo la ujumbe:** Humaanisha aina ya ujumbe unaowasilishwa. Mhimili huu ulitumiwa katika kubainisha umbo la ujumbe katika lugha iliyotumika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

3. **Muktadha:** Hii ni hali na mazingira ya matumizi ya lugha wakati wa mawasiliano. Muktadha unahusu mambo yanayosababisha kuchukua maana ya kawaida au fiche. Mhimili huu utatumiwa katika kuchunguza lugha inayotumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii huku tukizingatia muktadha wa mahali na utamaduni wa jamii ya Abagusii.
4. **Wahusika:** Wahusika ni muhimu katika uteuzi wa lugha ya mawasiliano katika jamii. Mambo muhimu yanayozingatiwa ni umri wao, tabaka lao, jinsia yao pamoja na uhusiano baina yao. Mambo haya ni muhimu na hayana budi kuzingatiwa kwani ndio msingi wa kuamua lugha inayoteuliwa katika mawasiliano. Mhimili huu utatumiwa kuchunguza wahusika wote wanaoshiriki katika mazungumzo kwa kutumia lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Wahusika hao ni wazazi, vijana, watoto na wataalamu wa haki za watoto.
5. **Sababu za mawasiliano:** Sababu za mawasiliano ni muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe. Sababu zinaweza kuwa za kibinafsi au za kijamii. Sababu hizi zinatumiwa kuamua aina ya lugha itakayotumiwa katika mawasiliano. Sheria za kuyaongoza mawasiliano hayo hubadilika kulingana na wahusika na muktadha. Mhimili huu utatumiwa katika kuchunguza sababu mbalimbali zinazowafanya Abagusii kuitumia lugha katika kuwasilisha taswira ya mtoto.
6. **Kanuni za ufafanuzi wa ujumbe:** Kanuni za ufafanuzi wa ujumbe zinahusu utaratibu wa imani katika utamaduni wa jamii ambao ni sharti ushirikishwe katika ufafanuzi wa matumizi ya lugha fulani katika mawasiliano. Mhimili huu utatumiwa katika kuchunguza kanuni za ufafanuzi wa ujumbe katika lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

7. **Njia za mawasiliano:** Hizi ni njia zilizoteuliwa katika mawasiliano. Mawasiliano yanaweza kuwa kupitia kwa mazungumzo, kuandika, kuimba, kupiga mbinja na kadhalika. Njia hizi ni muhimu kwa uwasilishaji, ufafanuzi na uelewaji wa ujumbe. Mhimili huu utatumika katika kubainisha njia mbalimbali za mawasiliano zinazotumika katika lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
8. **Utendaji:** Hurejelea sio maneno yanayosemwa bali uzungumzi wenyewe yaani utendaji huo wa kuzungumza. Pana uhusiano mkubwa baina ya tendo na maneno yanayozungumzwa kwa kuwa haiwezekani kuwa na tendo la uzungumzaji bila maneno, wala kuwa na maneno bila tendo la kuzungumza. Mhimili huu utatumika katika kuchunguza utendaji wa lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
9. **Aina ya ujumbe:** Kinachorejelewa hapa ni kwamba ujumbe wenyewe waweza kuwa wa kijuujuu au ni ule wenye maana fiche.

Mihimili ambayo imeorodheshwa na kufafanuliwa hapo juu ilikuwa msingi wa ujenzi wa maana katika lugha kutambuliwa. Nadharia ya Ethinografia ya Mawasiliano ilifaa utafiti huu kwa vile ilimwezesha mtafiti kuchambua na kuhakiki kwa uyakinifu mengi ambayo yalitekelezwa na lugha katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ili kuyafanikisha mawasiliano. Aidha, nadharia hii ilimwezesha mtafiti kufasiri na kufafanua iwapo jamii-lugha na mazingira yake vilizingatiwa. Mtazamo huu ulihakikisha kuwa utamaduni na uhusiano wa wanajamii vililindwa mawasiliano yalipokuwa yakiendelea.

## **1.8 Mbinu za utafiti**

Utafiti huu ulihusisha mbinu mbalimbali za utafiti. Mbinu zitakazojadiliwa katika sehemu hii ni; eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Mbinu hizi zilimwezesha mtafiti kupata data ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

### **1.8.1 Eneo la utafiti**

Njanjani mtafiti alifanya utafiti wake katika jamii ya Abagusii ambayo imegawika katika kaunti mbili. Kaunti hizo ni Kisii na ile ya Nyamira. Mtafiti alizuru eneo bunge la Nyaribari Chache linalopatikana katika ugatuzi mdogo wa Kisii ya Kati, Kaunti ya Kisii. Mtafiti alizuru wodi sita na mitaa midogo kumi na tisa na kuwahoji watoto, vijana, wanawake, wanaume, manaibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto. Wodi na mitaa midogo mtafiti alizuru ni:

<b>Wodi</b>	<b>Mitaa midogo</b>
i) Bobaracho	Nyamemiso, Bobaracho, Nyanguru na Kegati.
ii) Kisii ya Kati	Masongo, Nyaura na Nyanchwa.
iii) Keumbu	Nyamware na Bomwangi.
iv) Kiogoro	Boronyi, Nyaguta na Matunwa.
v) Birongo	Keumbu na Birongo.
vi) Ibeno	Kerera, Kirwa, Kabosi, Chirichiro na Nyamagwa.

Eneo bunge hilo liliateuliwa kwa sababu watu wengi kutoka jamii ya Abagusii waliishi huko. Watu hao walitumia lugha ya Ekegusii katika mawasiliano baina yao wakati walifanya

shughuli zao za kila siku. Mtafiti aliweza kupokea mawasiliano mengi yaliyokuwa na matumizi ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto kutoka kwa eneo hilo. Mawasiliano hayo yalimsaidia mtafiti kukusanya data kutoka kwa eneo hilo iliyofanikisha utafiti huu. Mtafiti aliweza kuzuru wodi zote na mitaa midogo yote na kuwahoji wanajamii mbalimabali kuhusu suala la utafiti. Aidha, mtafiti aliweza kurekodi mazungumzo yao katika mikutano mahususi na isiyo mahususi. Mtafiti vilevile aliweza kutambua na kuzingatia miktadha halisi ya kila tukio wakati wa ukusanyaji wa data.

### 1.8.2 Uteuzi wa sampuli

Sampuli ya waliotafitiwa ilichaguliwa kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii. Kulingana na hesabu ya wananchi wa Kenya mwaka wa 2009, Kaunti ya Kisii ilikuwa na watu milioni 1.152. Eneo bunge la Nyaribari Chache lilikuwa na idadi ya watu 129,745. Wodi, idadi ya watu katika kila wodi na mitaa midogo katika eneo bunge hilo ni:

	<b>Wodi</b>	<b>Idadi ya watu</b>	<b>Mitaa midogo</b>
i)	Bobaracho	29,338	Nyamemiso, Bobaracho, Nyanguru na Kegati.
ii)	Kisii ya Kati	32,203	Masongo, Nyaura na Nyanchwa.
iii)	Keumbu	15,024	Nyamware na Bomwangi.
iv)	Kiogoro	13,102	Boronyi, Nyaguta na Matunwa.
v)	Birongo	19,368	Keumbu na Birongo.
vi)	Ibeno	20,710	Kerera, Kirwa, Kabosi, Chirichiro na Nyamagwa.
	<b>Jumla</b>	<b>129,745</b>	<b>Kumi na tisa (19)</b>

Mtafiti alizingatia vigezo vya umri na jinsia kupata wawakilishi wa jamii nzima ya Abagusii. Mtafiti alitumia mbinu ya kimakusudi kuwateua wahojiwa kumi na wawili (12) kutoka kila wodi. Mtafiti aliwahoji watu wawili (2) kutoka kila kundi; watoto, vijana, watu wazima, naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto. Jumla ya watu sabini na wawili (72) walihojiwa. Mbinu ya kimakusudi ilitumiwa kwa vile iliwapa watafitiwa walioimudu vyema lugha ya Ekegusii kuhojiwa ili kupata matokeo faafu. Aidha, Mtafiti alitumia mbinu hiyo ya kimakusudi kutokana na ukweli kuwa utafiti huu ulihusu matumizi ya lugha ambao haukuhitaji sampuli kubwa kupata data nyingi, isipokuwa kama lengo ni kupata mifano mingi ya data ileile. Pia, uteuzi huu ulifuata kanuni ya utambuaji wa mapema ya watafitiwa waliolengwa. Jambo muhimu mtafiti alizingatia ni kwamba mhojiwa alikuwa na uwezo wa kutoa ufafanuzi wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Aidha, mtafiti alitumia sampuli hiyo kwa sababu ndiyo iliyolingana na muda wa kuikusanya data, kuiainisha, kuifasiri, kuichanganua na kuiandika tasnifu hii. Pia, idadi hiyo ya sampuli iliwakilisha vizuri jamii nzima ya Abagusii pamoja na kumwezesha mtafiti kupata lugha ya kutosha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii kulingana na uchanganuzi wa aina ya lugha hiyo, dhima na athari zake ili kupata matokeo mwafaka.

### **1.8.3 Ukusanyaji wa data**

Mtafiti alitembelea maktaba ya Vyuo Vikuu vya Kenyatta, Kisii, Egerton na Moi ambapo alisoma vitabu, kumbukumbu, tasnifu, makala, majalida, na machapisho yaliyohusiana na mada ya utafiti. Haya yalimsaidia mtafiti kuelewa zaidi kuhusu nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Mtandao wa mawasiliano nao pia ulikuwa wa msaada hasa kwa makala ya hivi karibuni yanayolenga mada. Ujuzi huu ulichangia utaratibu wa utafiti nyanjani. Aidha,

nyanjani mtafiti alikusanya data kutoka jamii ya Abagusii kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii. Mtafiti alitumia hojaji wazi katika kuwahoji watu katika mikutano ya hadhara, mabaraza ya wazee, waumini kanisani, arusi na matanga. Njia hiyo ilikuwa mwafaka kwani katika ule mwingiliano huru, mtafiti aliweza kupata data zaidi kwa kutumia kinasa sauti, kalamu na daftari kwa vile haya yalinaswa na kunukuliwa. Majibu yaliandikwa kwenye kijitabu cha utafiti na kudondoa yale yaliyofaa utafiti huu. Maoni yao yalisaidia katika kuchanganua data ambayo ilitarajiwa. Aidha, data zilizokusanywa zilirekodiwa kwa kutumia kinasa sauti. Kanda hizi zilikidhi upungufu ambao ulijitokeza kwa kushiriki katika mahojiano kwani haikuwa rahisi mtafiti kunukuu daftarini kila kitu. Ili kukusanya data ya kutosha, mtafiti alinukuu daftarini yote yaliyo muhimu ambayo yalimwezesha kukamilisha utafiti lengwa kwa kupata data toshelevu na ya kina. Data ya pili changishi ilikusanywa kutoka kwa kudurusu; tasnifu, vitabu, majarida, machapisho na wavuti.

#### **1.8.4 Uchanganuzi wa data**

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Data ya pili changishi ilikusanywa kutokana na hojaji wazi, tasnifu, vitabu, majarida, machapisho na wavuti vilichanganuliwa. Mazungumzo yaliyohusu mada ya utafiti yalinakiliwa katika lugha ya Ekegusii. Kisha, mtafiti aliyatafsiri mazungumzo hayo kwa lugha ya Kiswahili. Baada ya hayo, mtafiti alichanganua lugha hiyo kwa kutoa maana yake kulingana na miktadha ya matumizi yake katika jamii ya Abagusii. Uchanganuzi ulitolewa katika lugha ya Kiswahili. Habari zilizokusanywa zilikuwa za maana kwa sababu zilikuwa za muhimu katika ukuzaji wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mtafiti alizingatia maswali na malengo ya utafiti na matokeo yaliwasilishwa kwa njia



ambayo ilibainisha jinsi lugha iliwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Shughuli kama vile ujenzi na matumizi ya kategoria zilihusishwa kwa kuziorodhesha kulingana na sifa na majedwali kisha kuibuka na takwimu maalum. Mtafiti alihakikisha kuwa, data kubwa iliyokusanywa nyanjani ilibanwa katika makundi madogo, ambayo yalifanyiwa uchanganuzi zaidi. Uchanganuzi huu wa data ulifafanua jinsi data iliainishwa katika kategoria muhimu.

### **1.8.5 Uwasilishaji wa data**

Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo hayo yalizingatia matumizi ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Aidha, yalikusisha ubainishaji wa lugha hiyo, kuichanganua namna ilivyofasiriwa na kueleza dhima na athari zake katika jamii ya Abagusii. Data iliwasilishwa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Maelezo yote ya utafiti huu yaliwasilishwa kama tasnifu.

### **1.9 Hitimisho**

Yaliyoshughulikiwa katika sura hii ni masuala ya kimsingi katika utafiti ambayo ni: usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu, na mbinu za utafiti zilizohusisha; eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Haya yote yamefafanuliwa katika sura hii kwa lengo la kutoa mwelekeo na mwongozo kuhusu mada ya utafiti. Sura ifuatayo imeshughulikia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

**SURA YA PILI**  
**LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO KATIKA JAMII YA**  
**ABAGUSII**

**2.0 Utangulizi**

Lavine (1977), Mayer (1949), Nerlove (1969) na Ochieng (1974) wamebainisha kuwa Abagusii wanaishi katika miteremko ya kusini magharibi mwa milima ya Mau iliyo nyanda za Ziwa Victoria magharibi mwa nchi ya Kenya. Wataalamu hawa wameeleza vilevile kuwa Abagusii walifika eneo hilo katikati ya karne ya kumi na nane. Wamefafanua pia jamii ya Abagusii inaishi katika eneo lenye milima na rutuba katika wilaya ya Kisii na wanatumia lugha ya Ekegusii katika mawasiliano baina yao wanapotekeleza shughuli zao za kila siku. Miongoni mwa shughuli hizo ni jukumu la kuhakikisha kuwa watoto waliozaliwa katika jamii ya Abagusii wamefundishwa kuhusu masuala mbalimbali kama vile mila na desturi za Abagusii. Aidha, Abagusii wanatumia lugha hiyo katika kuwasilisha taswira mbalimbali za watoto zilizopatikana katika jamii ya Abagusii.

Kwa mujibu wa Phelan (2001), lugha inayotumika kwa mtoto katika kuwasilisha taswira yake katika jamii inastahili kuwa ile inayoeleweka kwa urahisi na wote wanaohusika katika mazungumzo. Utafiti huu umebainisha kuwa, jamii ya Abagusii ilitumia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii kwa lengo la kutoa maelezo ya kina kuhusu tabia ya mtoto huyo anapokua katika jamii. Sura hii kwanza imeshughulikia maelezo ya kimsingi kuhusu lugha hasi, kisha yale ya lugha chanya yamejadiliwa baadaye. Aidha, Mtafiti amechanganua mifano kadhaa ya lugha hasi na chanya na kuhakikisha kuwa amebainisha jinsi ilivyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano imetumika katika kuchanganua lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mihimili yake ilitumika katika kutambua na kufafanua lugha hiyo katika jamii ya Abagusii. Mihimili ya nadharia hiyo ambayo ilichangia pakubwa katika sura hii ni pamoja na mhimili wa mada zilizozungumziwa. Mada mbalimbali zilitumika katika kuwasilisha taswira mbalimbali za watoto katika jamii Abagusii. Aidha, Mada hizo ziliwaelekeza wanajamii kuamua lugha iliyostahili kuwasilisha taswira ya mtoto na yote aliyoyapitia katika maisha yake.

Wahusika katika mawasiliano ni mhimili mwingine wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliotumika katika uchanganuzi wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mhimili huo ulikuwa muhimu kwa vile katika mawasiliano yoyote, sharti wahusika watambuliwe. Utafiti huu ulibainisha kuwa wahusika waliohojiwa katika utafiti huu walikuwa ni; watoto, vijana na watu wazima kutoka jamii ya Abagusii. Wataalamu wa haki za watoto, manaibu wa chifu na machifu vilevile ni wahusika waliohojiwa.

Sababu za mawasiliano ni mhimili mwingine wa Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulioongoza uchanganuzi wa utafiti huu. Mhimili huu ni muhimu kwa vile uliwaongoza wazazi, walezi wa watoto pamoja na wanajamii kubuni na kutumia lugha iliyostahili katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Kwa mfano, ikiwa taswira ya mtoto iliyozungumziwa ni ya yule aliyeishi katika mazingira ya umaskini katika jamii, mnenaji alilazimika kuteua lugha iliyostahili na iliyokubalika kutumika katika jamii bila kuleta chukizo kwa vile watoto wote hawaishi katika mazingira sawa katika jamii ya Abagusii.

## **2.1 Lugha hasi iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii**

Lugha hasi ni ile ambayo baada ya kutumika katika mazungumzo iliibua hisia za kukasirishwa au kuhuzunishwa baina ya mzungumzaji na mtoto. Lugha hiyo ilipotumika kwa mtoto katika jamii ya Abagusii, ililenga kuweka wazi taswira yake alipokuwa akifanya jambo ambalo ni kinyume na maadili katika jamii ya Abagusii. Aidha, taswira ya mtoto huyo ilisababisha chukizo katika jamii. Sehemu hii imeshughulikia lugha hasi iliyowasilisha taswira za mtoto zifuatazo; mgonjwa, mlemavu, yatima, aliyeishi katika mazingira ya umaskini, aliyetumia pombe na dawa za kulevya, mwizi, aliyefanya uasherati, aliyewatusi watu, aliyepigana, zeruzeru, mzembe, aliyeoa au kuolewa, aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu na aliyetelekezwa katika jamii ya Abagusii.

### **2.1.1 Mtoto aliyekuwa mgonjwa**

Magonjwa kadhaa yalimsumbua mtoto alipoendelea kupokea malezi kutoka kwa wazazi wake katika jamii ya Abagusii. Mtoto aliweza kushambuliwa na magonjwa kama vile utapiamlo, ukimwi, kifua kikuu, dondakoo, malaria, nimonia na kifafa. Utafiti uliofanywa katika nchi ya Kenya na Wizara ya Afya ulibainisha kuwa watoto waliogua zaidi ni wale waliokuwa chini ya miaka mitano (MOH, 2005).

Mathalani, Edmond na wengine (2007) walifafanua kuwa mtoto alistahili kulala chini ya neti ili kumzuia kushambuliwa na mdudu mbu aliyesababisha ugonjwa wa malaria. Aidha, mtoto alistahili kupewa lishe bora na kupelekwa katika zahanati au hospitali kupokea chanjo zinazowakinga wasishambuliwe na magonjwa. Chanjo hizo zilitolewa kwa mtoto pindi alipozaliwa na aliendelea kupokea chanjo hizo hadi wakati alikomaa. Chanjo hizo zilisaidia

kuwakinga watoto kutokana na maradhi mbalimbali ambayo yaliwaangamiza watoto na kuwanyima fursa ya kuwa na afya maishani mwao. Wataalamu hawa vilevile walipendekeza mazoea kadhaa katika familia na jamii yaliyosaidia katika kuimarisha afya ya mtoto. Mfano wa mazoea hayo ni kumlea mtoto katika mazingira safi, kumpeleka mtoto kwa tabibu alipokuwa mgonjwa na kumpa mtoto chakula kilichopikwa vizuri.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeugua ugonjwa wa malaria ni:

*Omwana oyo nigo are omorwaire. Oborwaire obwo nigo bokogera otwara emechando emenge mono ase obogima bwaye. Nigo chingaki chinyinge okomonyora araire ase egetanda kiaye ase engencho ataigweti buya ase omobere oye. Kero kende nigo okomonyora omwana oyo akona korera boireboire ase engencho agoteba nigo agwatigwa omotwe. Naende omwana oyo tari kogosoria na abana bande ase engencho aigwete bobo ase omobere oye. Abaibori baye nigo bagoteba buna omwana oyo nigo agosaa na koroka naende tabwati erang'o yokoria endagera ende yonsi. Nigo akobachanda abaibori baye chingaki chia botuko egekogera tari korara chitoro nonya ng'ake. (Mtoto huyu ni mgonjwa. Ugonjwa huo unamfanya awe na shida nyingi katika maisha yake. Wakati mwingine alilala katika kitanda chake kwa muda mrefu kwa sababu alikuwa mgonjwa. Pia, alilia kila wakati kwa vile alikuwa na maumivu kama vile ya kuumwa kichwa. Aidha, mtoto huyu hachezi pamoja na watoto wengine kwa sababu ana maumivu mwilini mwake. Wazazi wake walisema kuwa mtoto wao anahara na kutapika na hana hamu yoyote ya chakula. Anawasumbua wakati wa usiku kwa vile hapati usingizi wowote).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada katika mfano wa lugha hii ni mtoto aliyekuwa mgonjwa. Taswira yake ilijitokeza wazi kupitia kwa maelezo kuwa mtoto huyo alishindwa kutekeleza shughuli zake za kila siku. Hivyo basi alihitaji msaada kutoka kwa watu wengine. Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa taswira ya mtoto huyo iliwasilishwa kupitia kwa lugha iliyoeleza dalili kadhaa za ugonjwa wa mtoto huyo kama vile *goatiwa omotwe* (kuumwa kichwa), *koroka* (kutapika), *koba neriberera rinyinge ase omobere* (kuwa na joto jingi mwilini), *gosaa* (kuhara), *gotaba nerang'o yokoria endagera ende yonsi* (kukosa hamu ya kula chakula chochote), na *koba omoreu* (kukonda).

Aidha, taswira ya mtoto huyo iliwasilishwa kupitia lugha iliyobainisha mahali mtoto alikuwa wakati aliendelea kuugua. Mtoto huyo aliweza kuwa *oraire ase egetanda kiaye egeka egetambe* (amelazwa katika kitanda chake kwa muda mrefu), *atimogete atari gokora egasi ende yonsi* (ametulia bila kutenda kazi yoyote), *ainkaransete nse atari gokwana kende gionsi* (ameketi chini bila kunena jambo lolote), na *akoba nyomba chingaki chionsi atari kogenda kogosoria amo nabana bande* (anakaa muda mrefu nyumbani bila kwenda kucheza pamoja na watoto wengine).

### **2.1.2 Mtoto aliyekuwa mlemavu**

Kwa mujibu wa WHO (1993), ulemavu ni hali iliyotokana na dosari mwilini au akilini. Hali hiyo husababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida alitegemewa kuyaweza na hivyo kumletea kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake. Kizuizi katika utendaji kinatokana na mfumo wa mtazamo wa jamii dhidi ya mtoto huyo. Ingstad (1990)

alibainisha kuwa watu walemavu wanapitia changamoto nyingi katika maisha yao. Baadhi ya changamoto walizopitia ni kubaguliwa kutoka kwa watu wengine kwa vile walikuwa walemavu. Aidha, watoto walemavu walikataliwa katika jamii nyingi kwa vile waliamini kuwa watoto hao walikuwa chanzo cha laana zilizowaandama katika jamii zao.

Katika jamii ya Abagusii, hali ya watoto kuwa na ulemavu iliambatana na unyanyapaa uliotokana na mila zilizopitwa na wakati. Kutokana na hali hiyo, mtoto mlemavu alionekana kuwa ni tegemezi asiye na uwezo. Alistahili vilevile kusaidiwa na watu wasio na ulemavu katika kumudu maisha yake. Mtazamo huu ulisababisha mtoto mlemavu kutengwa na watoto wengine waliomzunguka. Aidha, mtazamo huu ni hasi na ulikuwa kinyume na haki za kimsingi za watoto.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa mlemavu ni:

*Omwana oyo nigo ere aremarete. Nigo aiboretwe kare ekerema na korwa engaki eyio nabo achandegete ase obogima bwaye. Ase engencho yoborema bwaye tari konyara gotara buya. Nigo akobogorigwa na abaibori baye gose abana bamwabo korwa aiga gochia aaria. Oborema bwaye nigo bogerete ere agoikaransigwa nse na takonyara kobera ase ekerogo igoro egekogera ateme gokora boigo nabo arakere nse abuneke ebimo binde ase omobere oye bire buya. Abaibori baye tibari kwenyara ango bamogoreire ekerogo keria gekogendiwa. Omwana oyo nigo abaete emechando emenge nyore ekerog aganetie gwekonya nigo ere akobogorigwa gochia kebara. Tari ayio oka naende ere nigo akoragerigwa endagera obekerwa monwa ekerog akoigwa*

*enchara ase engencho aremarete ase amaboko aye. Tari konyara kobogoria gento kende gionsi ase amaboko aye. Nabo akoragerigwa na abaibori baye gose abana bamwabo. Asengencho aremareta ase amaboko aye nigo akobatebia abaibori baye keria aganetie bamorentera.* (Mtoto huyu ni mlemavu. Alizaliwa akiwa mlemavu na tangu wakati huo anasumbuka sana maishani mwake. Kutokana na ulemavu wake hana uwezo wa kutembea vyema. Anabebwa na wazazi wake au ndugu zake kutoka sehemu moja hadi nyingine. Ulemavu wake unamfanya kuketishwa chini, hawezi kukalia kiti kwa sababu akijaribu kufanya hivyo anaweza kuanguka chini na kuumiza viungo vingine vya mwili wake vilivyo sawa. Wazazi wake ni maskini na hawana uwezo wa kumnunulia kiti cha magurudumu. Mtoto huyu anawasumbua wazazi wake kwa vile yeye hubebwa hata kwenda msalani kwenda kujisaidia. Si hayo pekee, yeye hulishwa vyakula kwa kuwekewa kinywani wakati anahisi njaa kwa vile yeye ni kikono. Hawezi kubeba kitu chochote mikononi mwake. Hulishwa na wazazi au ndugu zake. Kwa vile yeye ni kikono husema anachohitaji wanamletea na kisha wazazi wake wanamwekea mdomoni anakunywa au anakula).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyekuwa mlemavu. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika lugha iliyobainisha kuwa mtoto huyo alipitia changamoto mbalimbali kama vile hakuwa na uwezo wa kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine, hakuweza kufanya kazi yoyote kwa kutumia mikono yake na aliketishwa chini kwa muda mrefu. Aidha, taswira ya mtoto huyo imewasilishwa kuwa mtoto huyo mlemavu hakuwa na uwezo wowote wa kufanya kazi yoyote katika jamii ya Abagusii. Pia, mtoto huyo mlemavu



alihitaji msaada kutoka kwa watu wengine kufanya shughuli muhimu za maisha kama vile kula, kwenda haja na kulala.

### **2.1.3 Mtoto aliyekuwa yatima**

Mtoto yatima ni yule aliyefiwa na mzazi mmoja au wazazi wote wawili. Hunter (1990) alibainisha kuwa taswira ya mtoto huyo katika jamii wakati mwingine ilikuwa ya kusikitisha. Baadhi ya familia zilizomhurumia mtoto huyo yatima ziliamua kubeba jukumu la kumlea na kumtunza baada ya wazazi wake kuaga dunia. Aidha, shirika la UNICEF (1990) lilibainisha changamoto kadhaa zilizowakumba watoto mayatima katika jamii. Mfano wa changamoto hizo ni kukosa mahali pa kuishi na kushughulikiwa kwa mahitaji yao. Shirika hili limebainisha kuwa wakati mwingine ilibidi mtoto yatima kwenda kuishi kwa familia nyinginezo zilizokuwa changa au kwa mababu zao waliokuwa wamezeeka. Familia hizo changa zilikuwa na changamoto za kuwaelea watoto hao mayatima kwa vile walihitajika pia kushughulikia mahitaji ya watoto wao. Shirika hili la UNICEF (1990) vilevile limebainisha kuwa baadhi ya watoto mayatima walihamishwa na kwenda kuishi kwa mababu zao. Watoto hao mayatima walikosa malezi bora kwa vile mababu hawa nao walitarajia kusaidiwa na watoto wao. Mababu walibaki wameshangaa kwa vile walitwikwa majukumu la kuwalea na kushughulikia mahitaji ya wajukuu wao waliokuwa mayatima.

Bledsoe (1989) vilevile amebainisha kuwa watoto mayatima walikumbwa na changamoto ya kubaguliwa kutoka kwa watoto waliokuwa na wazazi katika baadhi ya familia zilizokubali kuwalea. Licha ya kubaguliwa katika familia, Nalwanga na Sengendo (1987) wamebainisha kuwa baadhi ya watoto mayatima walikosa lishe bora katika familia hizo. Wamefafanua

kuwa licha ya kukosa lishe bora, pia hawakupelekwa katika zahanati au hospitali walipokuwa wagonjwa. Aidha, baadhi ya watoto hao mayatima walikosa kupelekwa shuleni kusoma kwa vile walikosa kulipiwa karo.

Utafiti huu umebainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa mayatima katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto yatima aliyekuwa na shida maishani mwake ni:

*Omwana oyo nigo are entankana egekogera abaibori baye bonsi mbari moyo. Nigo abwate emechando emenge mono tabwati onde okomorera gose komogorera ebinto aganetie kera rituko. Obokong'u abwate nobonge mono egekogera chianga chiaye chiamogoteire ere nigo akobeka amanchanchabe, tari konyora endagera akoria mambia, mobaso gose magoroba. Kera rituko nigo anarete goetanana ase emechi gose nanyore onde oramokonye endagera akoria. Naboigo, nigo aseriwa bwango iga korwa esukuru asengecho tabwati ekalamu, ebitabu, ebikoroto amo ne eyunifomu.*

(Mtoto huyu ni yatima kwa vile wazazi wake wote waliaga dunia. Ana shida nyingi kwa sababu hakuna yeyote anayemtunza na kumnunulia mahitaji yake ya kila siku. Ana shida nyingi sana kama vile nguo zake zimechakaa anavalia matambara, hapokei mlo wa asubuhi, mchana hata jioni. Kila siku ana mazoea ya kurandaranda katika nyumba za watu kutafuta msaada wa vyakula. Pia, alifukuzwa hivi karibuni kutoka shuleni kwa sababu hana kalamu, vitabu, viatu na hata sare za shule).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyekuwa yatima. Taswira ya mtoto

huyo ilijitokeza wazi kutokana na hali yake ya kujishughulisha kupokea mahitaji muhimu ya maisha kama vile vyakula, mavazi na mahali pa kuishi. Aidha, mtoto huyo alizunguka hapa na pale kwa lengo la kutafuta msaada kutoka kwa wanajamii. Taswira ya mtoto huyo pia ilikuwa ya kusikitisha kwa vile alifukuzwa kutoka shuleni kwa vile alikosa karo na sare za shule na vifaa vya kutumia kama vile kalamu, madaftari na vitabu vya kusoma.

Utafiti huu pia ulibainisha kuwa baadhi ya watoto mayatima walikuwa wamefiwa na mzazi mmoja baba au mama. Taswira ya watoto hao mayatima wakati mwingine ilikuwa ya kusikitisha mno katika jamii ya Abagusii. Baada ya watoto hao kuondokewa na wazazi wao wote, walitegemea misaada ya mahitaji muhimu katika maisha yao kutoka kwa watu wa ukoo wake au wanajamii ambao hawakuwa na uhusiano wa karibu nao. Wakati mwingine mtoto yatima aliweza kukosa msaada kutoka kwa wanajamii.

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto mayatima walikuwa na taswira ya kupokea malezi bora baada ya kupata wanajamii waliokuwa na utu waliokubali kubeba mzigo wa kushughulikia mahitaji yao yote ya kila siku. Hata hivyo, utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa baadhi ya watoto mayatima walisumbuka maishani mwao kwa vile waliteswa na kukosa wanajamii ambao walijitolea kuwapa mahitaji yao ya kila siku. Hali ya kuwalea na kuwatunza watoto hawa katika jamii ya Abagusii pia ilizua changamoto nyingi kwao. Mfano wa changamoto hizo ni kuwa waliokosa malezi bora, wengine waliamua kujihusisha na vitendo viovu kama vile ukahaba na kujiunga na magenge ya wezi au watu waliokuwa na kusudi la kutenda mambo mabaya katika jamii ya Abagusii.

#### 2.1.4 Mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini

Taswira ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini huwa ya kuhuzunisha katika jamii. Kwa mujibu wa Huston (1991) na Solley (2005), mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini alikosa mahitaji muhimu ya maisha kama vile chakula, maji safi, huduma za afya, mavazi na nyumba ya kuishi. Utafiti huu ulibainisha baadhi ya wazazi katika jamii ya Abagusii waliishi katika mazingira ya umaskini na watoto wao. Wazazi hao walikuwa na changamoto kadhaa hasa jukumu nzito la kuwalea na kuwatunza watoto wao. Kadhalika, wazazi hao walizoea kuwatuma watoto kwenda kuajiriwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni kama njia ya kupokea mahitaji muhimu ya kila siku. Watoto wengine katika jamii walihusika katika kuzunguka hapa na pale kwa lengo la kuomba msaada kutoka kwa watu wengine katika jamii. Utafiti huu vilevile umebainisha kuwa watoto waliozaliwa katika mazingira ya umaskini walisumbuka kwa vile waliishi maisha ya kusikitisha. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyu ni:

*Omwana oyo nigo ahandegete mono ase engencho bamenyerete obotaka. Nigo akobeka chianga amanchanchabe, mwabo tibabwati endagera bakoria nigo amatuko ande batari koria kende mambia mobaso gose magoroba. Nigo naende abana abwo amo na abaibori babo bamenyete ase enyomba bagotwerwa embura. Abana abwo tibri kogenda esukuru nigo bagoeta aiga naria amo na abaibori babo bakorigia kera rituko gokora egasi ye chikonda gose mbanyore bakore egasi eyio enkong'u gose mbanyore chibesa bagore chindagera aoao amo nebinto binde baganetie.*

(Mtoto huyu anasumbuka sana kwa vile wanaishi katika hali ya umaskini. Anavalia nguo matambara, nyumbani kwao hawana chakula chochote na siku nyinginezo hawali chochote asubuhi, mchana na hata jioni. Tena watoto hao hawaendi shuleni

kwa vile huzunguka hapa na pale pamoja na wazazi wao wakitafuta kazi zozote za vibarua wapate kuajiriwa ili waweze kujinunulia vyakula mbambali pamoja na vitu vinginevyo).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini. Mhimili wa tatu wa nadharia hiyo vilevile ulihusu muktadha wa mahali mawasiliano yalifanyika. Mazingira ya mawasiliano haya yalifanyika nyumbani kwa mtoto h. Taswira yake ilijitokeza wazi kwa vile; yeye alivalia matambara na aliishi katika nyumba iliyokuwa na paa lililokuwa linavuja. Aidha, mtoto huyo aliachishwa kwenda shuleni na kuandamana na wazazi wake, kwenda kufanya kazi za vibarua kwa lengo la kupata pesa za kuwawezesha kushughulikia mahitaji yao ya kila siku. Taswira ya mtoto huyo vilevile ilikuwa ya kusikitisha kwa vile wakati mwingine hawakufanikiwa kupata kazi na kuwalazimu kulala njaa.

Aidha, mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini alilala mahali pa kusikitisha, mfano wa lugha iliyowasilisha taswira yake ni:

*Omwana oyo nigo akorara ase are abe mono. Egetanda kiaye nigo gesirire namagena nabo arabaise kogwa botuko ekeru araire. Amarangeti amo ne ebitambaa nigo bire amanchanchabe. Naende amarengeti amo ne ebitambaa abio mbiana gosibigwa ase amatuko amange. Omwana oyo naende ere nigo akorarera riyo egekogera abaibori baye tibakonyara komogorera omoito. (Mtoto huyu analala mahali pabaya mno. Kitanda chake kimeegemezwa kwa kutumia mawe. Anaweza*

kuanguka chini usiku anapolala. Mablanketi na vitambaa ni matambara. Tena mablanketi na vitambaa hivyo havijaoshwa kwa muda wa siku nyingi. Mtoto huyu pia analalia ngozi kwa sababu wazazi wake hawana uwezo wa kumnunulia mgodoro).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini. Mtoto huyo alilala katika mahali pa kusikitisha. Alilala juu ya kitanda kilichovunjika bila kujifunika blanketi. Alijifunika vitambaa vilivyokuwa matambara na vilivyokuwa havijaoshwa kwa muda mrefu. Vitambaa hivyo vilijawa na wadudu kama vile chawa na kunguni waliomfyonza damu kutoka mwilini mwake wakati wa usiku.

### **2.1.5 Mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya**

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walitumia pombe au dawa za kulevya. Ni hatia kwa watoto kutumia pombe au dawa za kulevya katika jamii Abagusii. Watoto waliotumia pombe au dawa za kulevya wailkuwa na taswira za kutenda vitendo viovu katika jamii. Mfano wa vitendo viovu vilivyotendwa na watoto hao ni: walizua mafarakano katika familia zao, waliwabaka watoto wasichana na walitenda vitendo vya aibu kama vile kwenda haja ndogo hadharani. Aidha, watoto waliotumia pombe au dawa za kulevya walifanya vibaya katika masomo yao shuleni. Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa ulanguzi wa dawa za kulevya ni biashara iliyokita mizizi katika jamii ya Abagusii. Wakati mwingine baadhi ya watoto walitumika na wanabiashara haramu kuwauzia watoto wengine dawa za kulevya kama vile bangi, mirungi, mandrax, heroini na kokeini. Kokeini, ambayo ilipatikana katika hali ya ungaunga uliokuwa mweupe, ilitumiwa kwa njia ya kuvuta kwa pua

au ilichanganywa na maji na kisha kujidunga mwilini kwa kutumia sindano. Heroini pia ilipatikana kama unga mweupe au vipande vidogovidogo vya kahawia vilivyojulikana kama “sukari ya kahawia”.

Pombe na dawa za kulevya zilipatikana katika jamii ya Abagusii. Watoto kamwe hawakuruhusiwa kutumia pombe au dawa za kulevya. Hata hivyo, utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walitumia pombe na dawa za kulevya. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetumia pombe ni:

*Omwana oyo nigo ere akonywa ebusaa gose echang’aa. Ekeru anyure amarwa ayio nigo agotinda orenta eburaburu ase omochie. Nabo akobarwania abaibori baye gose abana bande. Naende tari koba naamasikani gochia ase abanto bande. Nigo akorama abanto bande na gokwana amang’na yokogechia. Amatuko ande nabo akonywa otinda omanya korara ase omotaro goika mambia. Nabo ere anchete gotara nabana bande banchete konywa amarwa. Ekeru anyure amarwa nigo agocha inka agotara kagotinana aiga naria. Naende, nabo ere arakore ebinto biobosoku ase abanto bande buna ogwekonya ase obosio bwa abanto bande. Nigo ere agwekonya ande onsi egekogera tari koinyora buna nemogwenerete kogenda enyomba ya kebara ase eng’echo atindete mono.* (Mtoto huyu hunywa pombe ya aina ya ‘busaa’ au ‘chang’aa’. Wakati amekunywa pombe yeye hulewa na kuanzisha mafarakano nyumbani. Anaweza kupigana na wazazi wake au watoto wengine. Tena hana heshima kwa watu wengine. Huwa anawatusi watu wengine na kuzungumza maneno yanayoleta chukizo. Wakati mwingine hunywa pombe na kulala kwa mtaro hadi asubuhi. Yeye hupenda kutembea na watoto wengine wanaopenda kunywa pombe.

Wakati amekunywa pombe na kulewa anarejea nyumbani huku akitembea mwendo wa kuyumbayumba hapa na pale. Aidha, anaweza kutenda mambo ya aibu mbele ya watu wengine kama vile kujisaidia. Hujisaidia adharani kwa sababu hakumbuki kuwa anastahili kwenda kwa choo kufanya hivyo kwa vile yeye amelewa chakari).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyetumia pombe. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile alikuwa mlevi na alitembea mwendo wa kuyumbayumba hapa na pale. Aidha, alitenda vitendo vya aibu kama vile kwenda haja hadharani, kuwatusi watu kwa maneno ya aibu, kuimba nyimbo zilizotaja maneno ya aibu na kupiga kelele ovyoovyo. Mtoto huyo aliyatenda hayo yote, bila kujali kuwa aliwasumbua watu waliohitaji kuwa na utulivu.

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walitumia dawa za kulevya. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetumia dawa za kulevya ni:

*Omwana oyio nigo agouta esigara, etumbato gose enyasore. Ekeru akorire bo nigo agotioka chisigara, etumbato gose enyasore. Tari ogotioka gwoka ebinto ebi nigo bikomokora oba buna ebarimo. Nigo ere agokora ebinto biokogechia, nabo aranyore omwana omoiseke amotachere inse. Naende nabo agoetanana aiga naria okona kwoga gose gokwana amang'ana yoobosoku.* (Mtoto huyo huvuta sigara, tumbaku na kasumba. Wakati amefanya hivyo yeye hutoa harufu mbaya. Si harufu mbaya pekee pia, yeye huwa kama mwendawazimu. Yeye hutenda vitu ambavyo ni vya



kuhuzunisha, akikutana na mtoto wa kike anaweza kumnajisi. Tena anaweza kuzunguka hapa na pale akipiga kelele au kuongea mambo yanayoleta aibu).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyetumia dawa za kulevya. Taswira yake ilijitokeza wazi jinsi alivyochanganyikiwa akili na kuwa kama mwendawazimu. Alisababisha fujo nyumbani kwao kama vile kuvunja vyombo, kupigana na wazazi wake au watoto wengine. Aidha, aliwatusi wazazi wake pamoja na watu wengine katika jamii. Pia, alirobokwa na maneno ovyoovyo na kutenda vitendo viovu vya kusikitisha katika jamii. Mfano wa vitendo viovu alitenda ni alimnajisi mtoto wa umri mdogo au nyanya wa miaka mingi. Mtoto huyo aliweza pia, kubeba silaha kama vile panga na aliwatishia kuwaua wazazi wake au mtu yeyote aliyekuwa karibu naye.

#### **2.1.6 Mtoto aliyekuwa mwizi**

Baadhi ya watoto walikuwa wezi katika jamii nyingi za bara la Afrika. Tabia ya watoto kuwa wezi kipindi cha karne ya ishirini na moja imezidi kupanda. Cimpric (2010) amebainisha kuwa kiwango cha watoto kushtakiwa kuwa wezi katika jamii nyingi za Kiafrika kinahatarisha maisha yao. Alibainisha pia watoto hao waliamua kuwa na tabia hiyo kwa sababu ya umaskini, kusawishiwa na marafiki zao au walikosa malezi bora kutoka kwa wazazi wao. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa wezi katika jamii ya Abagusii. Watoto hao walikuwa na mazoea ya kuwaibia watu vitu vyao. Mifano ya watoto waliozoea kufanya hivyo katika jamii ya Abagusii ni mayatima, waliorandaranda,

waliotelekezwa na walioishi katika mazingira ya umaskini. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa mwizi katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anchete gokora amang'ana yokogechia. Ere nigo are omobe egekogera are omoibi simbiri. Nigo akogenda ase emechi yaabanto bande obaibera ebinto biabo buna chibesa, amagena yeengoko, chingoko, chianga, chisimi amo nebinto binde aranyare kobogoria bobisi. Naende, ere nabo akogenda ase emegondo yabanto bande obaibera chindagera buna chibando, amatoke, ebitunguo, ching'eni, amo nebimeri binde aranyare kogesa bwango nakoira bobisi.* (Mtoto huyu anapenda kutenda mambo ya kuchukiza. Yeye ni mbaya kwa vile yeye ni mwizi hodari. Anazuru nyumba za watu na kuwaibia pesa, mayai ya kuku, kuku, nguo, rununu na vitu vinginevyo anaweza kubeba kwa siri. Pia, yeye huenda kwa mashamba ya watu wengine na kuwaibia mazao yao kule shambani kama vile; mahindi, ndizi, vitunguu, mboga na mazao mengineyo anaweza kuvuna na kubeba kwa siri).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa mwizi. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile mtoto huyo aliwaibia watu vitu vyao. Aliwaibia vitu kama vile; pesa, rununu, nguo, vitabu, mayai ya kuku, kuku, mbuzi, kondoo, mahindi na vitu vinginevyo angeweza kubeba kwa urahisi. Aidha, taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile mtoto huyo hakuwa na uhusiano mwema na watoto wengine kwa lengo la kuzuia kujulikana kuwa alikuwa mwizi. Mtoto mwizi vilevile alizoea kutoroka kutoka nyumbani kwao au shuleni na kisha alienda kuwaibia watu vitu vyao wakati walikuwa kazini. Pia, mtoto mwizi hakupenda kukaa au kucheza pamoja na watoto wengine, aliamua kujitenga na

kufanya shughuli zake pekee kwa lengo la kuwazuia watoto wengine kugundua kuwa alikuwa mwizi.

Baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walikuwa na taswira ya kunyemelea vitu vya watu wengine. Alivibeba vitu hivyo bila wenyewe kuwa na habari kisha mtoto huyo alitokomea mbali. Wanajamii walipogundua kuwa vitu vyao vilichukuliwa na mtoto asiyejulikana walianza kuvitafuta hapa na pale kwa lengo la kupatikana kwa vitu hivyo kisha kuvirudisha kwa wenyewe. Wizi ni tatizo kubwa katika jamii na hutendwa na watoto, vijana na hata watu wazima. Enzi hizi za ukosefu wa ajira visa vingi huripotwa kila siku kuhusu kupotea kwa vitu mbalimbali katika jamii.

### **2.1.7 Mtoto aliyefanya uasherati**

Kwa mujibu wa TUKI (2004), uasherati ni tabia ya kupenda kuzini. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walijihusisha na uasherati katika jamii ya Abagusii. Watoto hao walifanya uasherati kwa sababu kadhaa kama vile watoto walioishi katika mazingira ya umaskini waliweza kupokea malipo ya pesa au kutimiziwa mahitaji yao ya kila siku baada ya kufanya kitendo hicho. Aidha, watoto wengine walifanya uasherati kwa vile walipitia maisha yaliyokuwa na changamoto nyingi. Shauku ya kutaka kuelewa matokeo ya kufanya uasherati katika maisha ya watoto vilevile ni sababu iliyochangia baadhi ya watoto kujihusisha na kitendo hicho. Marafiki nao walisababisha baadhi ya watoto kufanya uasherati kwa vile waliwashawishi kuwa ni kitendo kizuri kinachoburudisha maisha.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefanya uasherati katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anchete gokora obonyaka. Nigo anarete goika nka sobo kobwairire. Amatuko amange nigo agoika nka sobo kobwairire. Kero kende nigo agotoka ase ebirabu biokoonia amarwa. Ekeru anyure amarwa na gotinda mono nigo agoansa gokora obonyaka amo nabanto bande. Nabo akoba kemobere amo nabanto bande atari koiroka onde bwensi. Boigo, nigo agokora obonyaka kera chingaki atabwati bwoba gose nabo aranyore amarwaire.* (Mtoto huyu anapenda kujihusisha na uasherati. Ana mazoea ya kufika nyumbani kwao akiwa amechelewa. Wakati mwingine hupatikana katika virabu vya kuuza pombe. Wakati amelewa chakari huanza kufanya uasherati na watu wengine. Hufanya ngono na watu wengine bila kumwogopa mtu yeyote. Aidha, anafanya uasherati bila woga kuwa anaweza pata magonjwa ya zinaa).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyefanya uasherati. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile alikuwa akirandaranda ovyoovyo, bila kujali kuhusu mambo aliyotenda katika maisha yake. Aidha, mtoto huyo alijihusisha katika vitendo viovu kama vile kufanya ngono na wavulana kadhaa, bila kujali uwezekano wa kupata mimba au magonjwa ya zinaa. Alikuwa na mazoea vilevile ya kwenda na kukaa katika virabu vya kuuza pombe, kwa lengo la kupata wanaume waliohitaji huduma zake kwa malipo. Pia, alizoea kwenda na kukaa mahali kuna sherehe kama vile za matanga au arusi. Alikuwa na lengo la kutimiza haja yake ya kufanya uasherati na wavulana au wanaume kwa malipo.

Kitendo cha kufanya ngono katika jamii ya Abagusii kimekubalika kwa wale wamehitimu umri wa kuo au kuolewa na wakafunga ndoa kisha wakaanza kuishi kama mke na mume katika familia. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walifanya uasherati. La kusikitisha zaidi ni kuwa baadhi ya watoto waliofanya uasherati walikuwa bado hawajakomaa, walikuwa wenye umri mdogo na walipuuza kutenda mambo muhimu katika jamii kama vile kwenda shuleni kusoma. Watoto hao walifurahia kwenda mahali waliweza kutenda uasherati kama vile vilabu vya kuuza pombe.

### **2.1.8 Mtoto aliyewatusi watoto wengine**

Jay (1996) alidai kuwa baadhi ya watoto, wakati walikuwa shuleni, walitumia lugha isiyostahili kwa watu wengine wakati waliwasiliana nao. Matusi yaliyotolewa na watoto hao yalisababisha mafarakano katika jamii. Bryans na Wolfendale (1981) wamebainisha kuwa chanzo cha watoto kuwatusi watu wengine katika jamii ni kuwa walikosa kufundishwa na wazazi wao lugha iliyostahili kutumika katika mawasiliano. Utafiti huu ulibainisha kuwa wakati watoto waliwatusi watu wengine walikuwa wamejawa na hasira. Aidha, walisababisha vita iwapo waliyemtusi naye alikasirishwa akaamua kuchukua hatua ya kupigana. Mtoto alipogundua kuwa aliyemtusi alimzidi kwa umri alitoroka na kwenda zake huku akiwa amemwacha mtu huyo akiwa ameuadhika. Mtoto huyo alitoroka asipatikane na mtu yeyote kwa vile alielewa kuwa maneno aliyotamka yalikuwa kero kwa watu wengine. Wakati mwingine wanajamii waliungana katika kumwadhibu mtoto huyo na kumshauri awaheshimu watu wengine katika jamii.

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii waliwatusi watoto wenzao, vijana na hata watu wazima. Taswira ya mtoto huyo ilikuwa ya kutoa maneno kinywani mwake yaliyowaudhi watoto wenzake, vijana na watu wazima. Jambo la kusikitisha ni kuwa mtoto huyo aliweza kupokea matusi hayo kutoka kwa marafiki zake au watu wazima katika jamii. Mtoto huyo alipokasirishwa na kusumbuliwa na jambo au wazo lolote, aliweza kutumia lugha hiyo ya matusi kwa watu wengine. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ni:

*Omwana oyo nigo anchete kobarama abana bande. Ere boigo nigo akobarama abasae nyore nabanto abanene. Nigo akobarama abanto bonsi ase amang'ana amabe yobosoku. Nigo naende anchete kobachegia abana bande kera chingaki naende omanyanya gochaka kobarama. Nigo akobarama; ebarimo eye, ebunda eye eng'ondi eye gose esese eye. Omwana oyo tabwati bosooku asengecho ere akobarama abanto bande amang'ana yokogechia mono ase abanto bonsi. (Mtoto huyu anapenda kuwatusi watoto wengine. Anawatusi pia vijana na hata watu wazima. Anawatusi watu wote akitumia lugha ya aibu. Tena anapenda kuwachokoza watoto wengine. Anawatusi watu kuwa wao ni; zuzu, punda, kondoo na mbwa. Aidha, mtoto huyu haoni aibu yoyote anapowatusi watu wengine akitumia lugha ambayo inaleta chukizo kwa wanajamii wote).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyewatusi watu. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kupitia jinsi alivyowatusi watoto wengine na hata watu wazima. Aliwatusi kwa kutumia maneno yaliyozua fedheha kwa wanajamii. Mtoto huyo vilevile

alitumia maneno yaliyohusu sehemu za siri ambazo kwa kawaida hazistahili kutajwa adharani. Mfano wa lugha ya matusi aliyotumia ni *aye namabi* (wewe ni mavi), *aye nebunda* (wewe ni punda) na *aye nesese* (wewe ni mbwa).

### **2.1.9 Mtoto aliyepigana na watoto wengine**

Kupigana kwa mujibu wa Momanyi (1996) kupigana kwa watu katika jamii ya Abagusii ni kitendo kilichosababishwa na ugomvi kati ya watu wawili au zaidi. Amebainisha kuwa baadhi ya watu katika jamii ya Abagusii walikuwa na mazoea ya kujawa na hasira kisha kupigana na watu wengine katika jamii. Utafiti huu umebainisha kuwa hata baadhi ya watoto nao walizoea kupigana katika jamii. Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa watoto waliopigana walifanya hivyo baada ya kukasirishwa na jambo fulani. Watoto hao walikosa kuelewana na kubishana kwa kutumia lugha ya matusi. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa watoto hao walisababisha hasara kwa kuvunja vyombo vilivyokuwa karibu nao. Baada ya kupigana watoto hao vilevile waliweza kuwa na majeraha. Wakati mwingine watoto hao walipigana hadi walipozuiliwa kufanya hivyo na watu wengine.

Utafiti huu ulibainisha sababu kadhaa zilizowafanya watoto kuwa na mazoea ya kupigana. Mtoto aliye na mazoea ya kupigana alifanya hivyo kwa vile alikerwa na jinsi alivyotendewa na watoto wengine. Huenda alitusiwa na mtoto mwingine, alibaguliwa wakati wa kushiriki katika michezo, alisengenywa na watoto wengine, alikisia kuwa kuna mtoto aliyemripoti kwa wazazi wake kuhusu mambo mabaya aliyokuwa akitenda, alipogundua kuwa kuna mtoto aliyemtendea mambo maovu na wakati alikasirishwa kwa njia yoyote na watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyepigana katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo akorwana kera chingaki. Ere nigo are omotindi bore igoro. Abana bande nigo bamwoboete ase engencho bakorwana chisegi nere kera chingaki. Kero kende nigo omwana oyo nigo akobogoria amagena obarutera na kobaaka. Nabo arabarwanie abana bande ase okobogoria ebirwanero aoao buna omoro gose enungu omanyanya kobaminyokia na kobaaka. Goetera okwarwana kwaye omwana oyo nigo anchete goitera amanyinga.* (Mtoto huyu anapigana kila wakati. Anayo hasira ya juu. Watoto wengine wanamwogopa kwa vile anapigana nao kila wakati. Wakati mwingine mtoto huyu hubeba mawe na kuwarushia na kuwaumiza watoto wengine. Anaweza pia kupigana na watoto wengine kwa kubeba silaha mbalimbali kama vile panga au rungu kisha anawakimbiza na kuwachapa. Kupigana kwake kunasababisha umwagaji wa damu).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyepigana na watoto wengine. Taswira yake ilijitokeza wazi kwa vile alizoea kuwachokoza watoto wengine na kuzua rabsha. Baada ya kuzua vurugu alianza kupigana na watoto wengine. Aidha, mtoto huyo alitumia mbinu zozote za kuangamiza adui zake kama vile kubeba mawe na kuwarushia, kubeba silaha kama vile panga na kuwapiga nayo, kuwacharaza viboko kwa kutumia fimbo au kuwagonga kwa kutumia rungu. Mtoto huyo pia alimalizia kuwa na majeraha usoni na hata mwili wake wote kutokana na kupigwa na adui zake. Mtoto huyo vilevile alikuwa na hasira iliyomfanya kuwa mkali na hata kuendelea kurobokwa na matusi kwa watoto wengine.



### 2.1.10 Mtoto aliyekuwa zeruzeru

Kwa mujibu wa Lee (2001), mtoto zeruzeru ni yule asiye na rangi katika ngozi yake, macho au nywele kwa sababu ya upungufu wa madini ya melanini ambayo hutengeneza rangi mwilini. Kazi ya melanini ni kunyonya mionzi hatari ya jua isiunguze na kudhuru mwili. Utafiti wa Mitchel (2004) ulidhihirisha kuwa kuna dhana mbili jinsi mtoto zeruzeru alivyoweza kuzaliwa. Dhana hizo ni kisayansi na kiimani. Kisayansi ni kuwa zeruzeru aliweza kuzaliwa kutokana na chembechembe za urithi kutoka kwa mmoja wa wazazi wa mtoto au sababu nyinginezo zaidi za kisayansi. Dhana ya kiimani imegawanyika katika sehemu mbili kidini na kimila. Imani ni mambo ambayo tumeyakuta tangu enzi za kale katika maandiko au kwa njia ya mazungumzo. Bila shaka dini nyingi huamini kuwa kila kitu kilichomo duniani kiwe kizuri au kibaya kimeumbwa na mwenyezi Mungu jinsi kilivyo na hivyo hakina kasoro wala ubaya wowote. Mila pia huwa na mtazamo wa kisayansi na kidini.

Utafiti huu ulibainisha kuwa watoto zeruzeru walizaliwa katika baadhi ya familia katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa zeruzeru katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omokebaru. Nigo akorokwa boigo ase engencho rinsaku riaye nigo rirabete buna erimosongo. Naende nigo abwate etuki erabete. Nigo abwate obokong'u obongease obogima bwaye. Ekeru omobaso omororo obarete nigo akoromwa mono ase rinsanku riaye. Boigo ekeru kiomogaso omororo tari konyara korora buya. Nigo bakomoroka omosota asengencho rinsanku riaye rirabete ndibwekaini eri abana bande. Abana amo nabanto bande nigo banchete komosuna omwana omokebaru bamanye naki akoigwa. Abanyamesira amo nabanto begenete*

*oborogi nabo bakobabwata bobisi babaita na koburukania chinyama chiabo ase oborogi bwabo. Ase engencho yoborogi bwabo nabo omwana omokebaru akoirwa bobisi na koonigwa chibesa chunyinge mono.* (Mtoto huyu ni zeruzeru. Huitwa hivyo kwa vile ngozi yake ni kama ile ya mzungu. Aidha, nywele yake ni nyeupe. Ana shida nyingi maishani mwake. Wakati kuna jua kali anahisi maumivu makali katika ngozi yake. Pia, wakati wa jua kali hawezi kuona vizuri. Wanamwita zeruzeru kwa vile ngozi yake haifanani na ya watoto wengine. Watoto na watu wengine katika jamii wana mazoea ya kuwachuna watoto zeruzeru ili wagundue anavyohisi. Waganga na watu wanaowamini wachawi wanawakamata watoto zeruzeru kwa siri kisha kuwaua na kuchanganya nyama zao na hirisi zao. Kutokana uchawi huo mtoto zeruzeru anaweza kuuzwa kwa bei ghali katika jamii ya Abagusii.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mwasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyekuwa zeruzeru. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika ngozi yake iliyokuwa nyeupe. Ngozi ya mtoto huyo ilikuwa tofauti na ile ya watoto wengine walioazaliwa katika jamii ya Abagusii. Wakati wa jua kali, mtoto huyo hakuwa na uwezo wa kuona vizuri, ilibidi afunge macho yake ili kuzuia miale ya jua kumletea shida. Aidha, mtoto huyo alihisi uchungu katika ngozi yake wakati wa jua kali. Wanajamii nao walibaki wakishangaa na kumtazama mtoto huyo jinsi ngozi yake ilivyokuwa tofauti. Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa, mtoto zeruzeru alipitia changamoto nyingi kama vile watoto wengine walimdonga sindano ili waweze kufahamu zaidi kuhusu rangi ya damu yake. Aidha, watoto wengine walimchuna mtoto zeruzeru kwa lengo la kubainisha alivyohisi.

### 2.1.11 Mtoto aliyekuwa mzembe

Kwa mujibu wa TUKI (2004), uzembe ni hali ya kufanya jambo bila ya makini. Pia, ni hali ya mtu kufanya jambo kwa ulegevu. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walikuwa wazembe. Watoto hao waliamua kuwa wazembe kwa vile walipata nafasi nzuri ya kutembea hapa na pale na kufanya shughuli zao kama vile kucheza na marafiki, kutazama vipindi mbalimbali katika runinga, kuwatembelea marafiki na kupiga gumzo nao na kushiriki katika sherehe au burudani yoyote iliyoandaliwa katika jamii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa mzembe katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omworo mono tancheti gokora meremo ende yonsi. Nigo anchete goikaransa nse na gotimoka nario atakore meremo ende yonsi. Ekerokomotebia akore meremo ende yonsi ere nigo anchete korwa ebitamero. Nabo agotamera buna ere nigo are omorwaire, takonyara gokora emeremo eyio gose nigo are omorosu nigo aganetie gotimoka. Nigo akoigwa buya koba ase atimogete bosa igo atari gokora meremo ende yonsi. Ekerokomotebia akore meremo ende yonsi na abana bande mbare ang'e nere nigo ere abwate chinsega, akogotebia; tiga omwana onde akore emeremo eyio, gose takona gontebia nkore emeremo nche bweka kera chingaki. Ekerokomwana oyo okomotoma agende kogora gento kende gionsi korwa eduka nigo akaira egeka egetambe tari koirana bwango egekogera nigo ere are omworo.* (Mtoto huyu ni mzembe sana hapendi kufanya kazi yoyote. Wakati unamwambia afanye kazi yoyote yeye hupenda kutoa visingizio vya kutofanya kazi hiyo. Anaweza kusingizia kuwa; yeye ni mgonjwa, hana uwezo wa kufanya kazi hiyo au yeye amechoka anahitaji kupumzika. Yeye hufurahi kuwa mahali ametulia bila kufanya kazi yoyote. Akiombwa kufanya kazi yoyote husingizia kuwa; mtoto

mwengine anaweza fanya kazi hiyo na wala sio yeye, au anaweza jibu kuwa, “wacha kunisumbua kwa kuniambia nifanye kazi pekee kila wakati.” Mtoto huyu ukimtuma aende dukani kununua kitu chochote huchukua muda mrefu bila kurudi haraka kwa sababu yeye ni mzembe).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa mzembe. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile alijifanya kuwa mnyonge kila wakati. Alipotumwa au kuambiwa afanye kazi yoyote alisema kuwa ilikuwa ngumu na hakuwa na uwezo wa kuifanya. Aidha, mtoto huyo hakuwa na moyo wa kufanya kazi yoyote aliyoagizwa kufanya na wazazi wake. Wakati mwingine mtoto huyo alipolazimishwa na wazazi wake kufanya kazi yoyote, alikubali shingo upande na kuitenda polepole. Mtoto huyo pia alipoambiwa kufanya kazi kadhaa, aliamua kufanya moja pekee na kupuuza kazi nyinginezo. Wazazi wake walipomuuliza sababu za kutofanya kazi zote, alitoa visingizio kuwa kazi hizo zilizosalia zitendwe na kaka au dada zake. Mtoto huyo pia, hakuimarika kiakili na kimwili kutokana na uzembe wake.

#### **2.1.12 Mtoto aliyeoa au kuolewa**

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto UNICEF (1990) limebainisha kuwa jamii nyingi za kiafrika zimeendelea kuwaoza watoto wasichana wakiwa bado na umri mdogo. Aidha, shirika hilo limebainisha sababu kuu za jamii hizo kuwaoza watoto wasichana kabla ya kubaleghe ni umaskini, ukosefu wa usalama, mila na desturi potofu pamoja na itikadi za jadi. Kenya ni mojawapo ya nchi ambayo imeathiriwa na idadi kubwa ya watoto wasichana

walioozwa wakiwa na umri mdogo duniani. Ndoa za watoto hawa zimekuwa ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu kwa watoto wa kike ambao wamejikuta wakiharibikiwa na maisha kutokana na kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi wakiwa bado na umri mdogo. Shirika hilo pia limebainisha kuwa wasichana hao walilazimishwa kuolewa na walezi au wazazi wao ili wapate fedha za kujikimu kimaisha na wengine kutokana na mila na desturi potovu.

Bellamy (2004) amebainisha kuwa tabia ya kuwaoza watoto wasichana katika jamii iliwanyima haki yao ya kuendelea na masomo na kuwafanya kuwa katika hali ya kupatwa na magonjwa yaliyotokana na kujifungua wakiwa bado na umri mdogo. Pia, wataalamu wa masuala ya afya ya uzazi wamebainisha kuwa mtoto msichana aliposhiriki katika kitendo cha ngono akiwa na umri mdogo, aliweza kupoteza maisha yake au kuwa mwenye matatizo ya kiafya kutokana na viungo vyake vya uzazi ambavyo bado vilikuwa havijakomaa.

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi watoto wasichana waliolewa katika jamii ya Abagusii japo ni hatia kufanya hivyo. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto msichana aliyeolewa na mwanamume aliyemzidi umri na aliyekuwa tajiri katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo asokera omogaka ore nemiaka emenge komobua bwango iga. Nigo achora kogenda bwoye ase engencho omogaka oyio abwate obotenenku obonge. Boigo, omwana oyo nigo akanigwa nabaibori baye tabaisa gosoka aragenderia amasomo aye akaanga. Naende buna akororekana nigo ebwateranetie. Abaibori baye amo na abana bamwabo nigo batema mono komoirani sobo korende ere bwangire. Nigo akobatebia buna nigo agochandeka kogenda esukuru kera rituko. Naende nigo ere akobatebia tibana komochanda egekogera achorire gosoka kare omoke. Naende nigo akobatebia buna kera omonto naganeirie echorere ere omonyene egiarakore ase*

*obogima bwaye.* (Mtoto huyu aliolewa na mwanamume ambaye anamzidi umri hivi karibuni. Aliamua kuolewa kwa vile mwanamume huyo ni tajiri mno. Aidha, mtoto huyu alikatazwa asiolewe na wazazi wake aendelee na masomo yake akakataa. Tena jinsi inavyoonekana yeye ni mja mzito. Wazazi wake pamoja na ndugu zake wamejaribu kumwambia arudi nyumbani kwao amekataa. Anawaambia kuwa anasumbuka kwenda shuleni kila siku. Tena anawelezea kuwa wasiendelee kumsumbua kwa sababu ameamua kuolewa bado akiwa mwenye umri mdogo. Anawaelezea pia kuwa kila mtu ana haki ya kujichagulia mwenyewe jambo analostahili kutenda katika maisha yake).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyeolewa. Taswira yake ilijitokeza wazi kwa vile aliamua kuacha masomo yake akatoroka kutoka shuleni kisha akaolewa na mwanamume aliyemzidi umri. Alishawishika kufanya hivyo kwa vile mwanamume huyo alikuwa tajiri. Aidha, msichana huyo alikuwa amepachikwa mimba na mwanamume huyo. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya watoto wawili walioamua kuishi pamoja kama mume na mke walioamua kwenda kuishi mbali na wazazi wao ni:

*Omwana oyo omomura nigo ere anyuomete omwana onde omoiseke. Nigo bamenyete amo nyore abaibori babo mbamanyeti. Nigo bakomboete enyomba bakamenya buna omogaka na omong'ina twachire gotema kobasemia tibagenderia gokora bo bangire gotoigwera. Bamenyanire ase emetinyi ebere batari kwegosa gose kende kebe nabo kerababere. Onye tibari gotigana bwango iga, nabo omoiseke oyo akoba morito.*

(Mtoto huyu mvulana, amemwoa mtoto mwengine msichana. Wanaishi pamoja bila wazazi wao kuwa na habari yoyote. Wamekodisha nyumba na kuamua kuishi kama bwana na bibi na tumejaribu kuwashauri wasifanye hivyo wamekataa kutii. Wameishi pamoja kwa muda wa miezi miwili bila kuwa na woga wowote kuwa wanaweza pata shida yoyote. Kama hawatatengana hivi karibuni mtoto huyu msichana atapachikwa mimba).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyeoa. Taswira ya watoto hawa ilijitokeza wazi kwa vile waliamua kutoroka kutoka makwao na kwenda kuishi katika mji wa Kisii. Walikodisha nyumba na kuamua kuishi kama mke na mume. Aidha, mtoto huyo msichana alionyesha dalili za kuwa mjamzito kutokana na kutiwa mimba na mvulana huyo.

### **2.1.13 Mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu**

Ajira ya watoto ni tatizo kubwa katika taifa la Kenya. Kuna baadhi ya watoto walioajiriwa kufanya kazi kwa sababu ya mapato duni katika familia. Kwa mjibu wa shirika la kutetea haki ya wafanyakazi ILO (2011), mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi alinyimwa nafasi yake ya kwenda shuleni. Shirika hilo vilevile limebainisha kuwa sababu ya watoto kuajiriwa kufanya kazi katika jamii ni umaskini. Ajira hizo za watoto zilitumika kama njia ya kuwanyanyasa kwa vile walipewa malipo duni. Aidha, utafiti uliofanywa katika nchi ya Kenya na shirika la ILO (2012) ulibainisha kuwa asilimia 28.8 ya watoto walijajiriwa kufanya kazi za uyaya, kilimo, uvuvi na misitu. Maeneo ya vijijini, asilimia 35.6 ya watoto walijajiriwa kufanya kazi.

Utafiti huo pia ulibainisha kuwa watoto milioni 15 wenye umri wa miaka 5 hadi 17 walijajiwa kufanya kazi. Wavulana walikuwa milioni 7.6 na wasichana milioni 7.4.

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walijajiwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni katika jamii ya Abagusii. Shida kadhaa katika familia zilisababisha watoto wengi kuajiriwa kufanya kazi badala ya kwenda shuleni kusoma. Mashirika kadhaa kama vile UNICEF, UNHCR, CRC na HRW yamejitokeza kutetea haki za watoto katika jamii. Aidha, mashirika hayo yameangazia kwa kina kuhusu mateso na unyanyashaji wa watoto hasa kwa kuajiriwa kufanya kazi katika jamii kwa malipo duni. Kadhalika, mashirika hayo yamependekeza kuwa kila mtoto ana haki ya kupata elimu itakayomwezesha kupokea maarifa na ujuzi wa kumwezesha kujitegemea siku zijazo. Mashirika haya vilevile yamependekeza kuwa kuna haja ya kuzuia kila aina zote za ajira za watoto kupitia kwa kuwahamasisha wanajamii kuhusu athari zake.

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo ere nigo arikire gokora egasi enkong'u mono naende omanyanya koegwa chibesa nchike mono. Nigo agwatia amagena amanene mono erio korosia ekogoto eyegotumeka ase amagacho ye chinyomba chinyinge chikwaagachwa ase egesaku kiabagusii. Boigo omwana nigo agokora emeremo ye chikonda. Ere nigo boigo agosomba amache korwa oroche roro are mono omanyanya kobaretera abanto bande, akoagacha chinyomba, agosomba amagena amo nebinto binde bire ebirito buna esimiti, omonchanga, amatobori, chibao amo nechichuma. (Mtoto huyu ameajiriwa*



kufanya kazi ngumu sana kwa malipo duni. Anapasua mawe makubwa ili kutengeneza kokoto ambayo hutumika katika ujenzi wa nyumba nyingi katika jamii ya Abagusii. Mtoto huyu ameajiriwa kufanya kazi za vibarua. Anaenda mtoni mbali sana kuteka na kuwaletea maji watu wengine, anafanya kazi ya ujenzi, anasomba mawe pamoja na vitu vingine vizito kama vile simiti, mchanga, matofari, mbao, pamoja na vyuma).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile mtoto huyo alikuwa akifanya kazi ngumu kama vile kupasua kuni, kufua nguo, kupika, kuteka maji kutoka mtoni, kubeba mawe au matofari na kubeba miti au mbao. Baada ya kufanya kazi hizo, alipewa malipo duni ya shilingi mia moja kwa siku. Aidha, alifanya kazi hizo bila kupewa chakula chochote na kumfanya kuwa mnyonge. Alipojaribu kuketi na kutulia kwa sababu ya njaa na uchofu alikemewa vikali na kuonywa kutolipwa chochote.

Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walijiriwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni katika jamii ya Abagusii. Ajira ya watoto ni tatizo sugu katika jamii ya Abagusii, sababu kubwa ni mapato duni ya familia. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya wazazi waliwatuma watoto kufanya kazi za vibarua ili wachangie katika kukimu haja za familia zao. Hali hii iliwafanya watoto hao kukosa elimu hasa wakati huu ambapo kuna elimu bila malipo nchini Kenya. Watoto walikosa elimu waliyostahili kupokea kwa manufaa yao siku zijazo. Waajiri wa watoto hao waliwalipa malipo duni. Wazazi wengine pia katika

jamii ya Abagusii hawakujali kuhusu mabadiliko ya afya na tabia ya watoto hao hasa wakati walikuwa kazini.

#### **2.1.14 Mtoto aliyetelekezwa**

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walinyanyaswa kwa kutelekezwa na wazazi wao katika jamii ya Abagusii. Kumnyanyasa mtoto kwa kumtelekeza ni kukosa kumpa mahitaji na huduma muhimu ambazo zinaimarisha maisha yake kama vile vyakula, nguo, malazi na nyumba ya kuishi. Utafiti uliofanywa na shirika la UNICEF (1990) ulidhihirisha kuwa mtoto alitelekezwa na wazazi wake wakati walikosa kumlea na kumtunza. Aidha, mtoto aliyetelekezwa alikosa kupelekwa hospitalini kupokea matibabu au shuleni kusoma. Mtoto pia aliyetelekezwa alifukuzwa kutoka nyumbani kwao na kukosa ulinzi uliostahili kutoka kwa wazazi wake. Cimpric (2010) vilevile amefafanua kuwa watoto waliokisiwa kutenda vitendo viovu kama vile uchawi walitelekezwa na wazazi wao.

Cantwell na Rosenberg (1990) walifafanua kuwa kuna watoto ambao walitelekezwa katika familia nyingi. Wanaeleza kuwa kumtelekeza mtoto ni kuacha kuendelea kumtimizia mahitaji yake ya kimsingi. Wazazi wengine, waliamua kwamba hawatashughulikia watoto wao kutokana na sababu mbalimbali kama vile kupanda kwa gharama ya maisha, iliyosababisha wazazi kushindwa kuwanunulia watoto wao vitu muhimu kama vile vyakula, mavazi na hata kujenga nyumba nzuri ya kuishi. Baada ya wazazi kugundua kuwa hawakuwa na hela za kutumia kuwashughulikia watoto wao waliamua kuwaacha watoto hao nyumbani au njiani bila mtu yeyote wa kuwatunza kisha walikata kauli ya kuhamia sehemu nyinginezo bila watoto wao.

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa watoto wengine waliozaliwa nje ya ndoa walitelekezwa na wazazi wao. Waliamua kufanya hivyo kwa sababu watoto hao walikuwa mzigo kwao. Wazazi walidai kuwa watoto hao waliwapigia kelele na kuwaharibia starehe zao. Wengi waliofanya hivyo ni vijana walioamua kuanzisha ndoa za mapema. Waliposhindwa kujimudu maishani pamoja na watoto wao, waliamua kuwatelekeza kwa kuwapeleka nyumbani kwa nyanya au babu na kuwaacha pale bila yeyote wa kuwasaidia. Baadhi ya watoto waliotelekezwa walisumbuka kwa vile walisalia mikononi mwa akina nyanya na akina babu waloikuwa wamezeeka bila uwezo wowote wa kuwalea na kuwatimizia mahitaji yao.

Utafiti huu ulibainisha kuwa watoto waliotelekezwa walisalia mikononi mwa wanajamii waliojitolea kuwasaidia. Wakati mwingine watoto waliotelekezwa walikosa msaada na kuwafanya kurandaranda na kuombaomba hapa na pale katika miji mbalimbali iliyopatikana katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa tatizo la kuwepo kwa watoto waliotelekezwa katika jamii ya Abagusii lilichangia kuwepo kwa watoto walioitwa ‘chokoraa’. Hawa ni watoto walitoroka kutoka makwao kwa vile walitelekezwa na wazazi wao na kuamua kwenda kuishi mitaani. Wanajamii walipogundua kuwa mtoto alitelekezwa katika familia, walifanya juhudi za kuwatafuta wazazi wake na kuwalazimisha kumlea na kumtunza mtoto wao. Wazazi waliogunduliwa kupuuza majukumu yao katika jamii, hasa kuwatelekeza watoto walishtakiwa mahakamani. Jamii ya Abagusii iliamini kuwa kila mtoto alistahili kuwa na haki ya kuishi na kutimiziwa haja zake zote za kila siku.

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetelekezwa na wazazi wake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo atigire agwo nabaibori baye. Nigo babwate obokong'u obonge korwa abaibori babo bagenda. Tibabwati monto onde okobakonya kobaa endagera. Amatuko ande nigo bakorara nchara batari konyora kende bakoria. Nigo okobanyora kera rituko bakonagoetanana aiga naria bakona gosaberera gose onde nabae kende. Abana aba batigire abwo chianga chiabo chiabagoteire. Nigo bakobeka amanchanchabe. Boigo mbabwati ase agiya bakorara. Nabo okobanyora baraire isiko ye ebisona bie chituka gose ase amakarabati. Asengencho batabwati kende bakoria nigo bakobaibera abanto bande ebinto biabo na gotama. Nabo bakogenda emegondo yabanto bande basaria chindagera chiabo. Tibari kogenda gosoma esukuru egekogera onde taiyo okobagorera eyunifomu ne ebitabu bakorika na gosoma. (Mtoto huyu ametelekezwa na wazazi wake. Ana shida nyingi tangu atelekezwe na wazazi wake wakaenda zao. Hawana mtu yeyote wa kuwapa chakula. Wanalala njaa siku nyinginezo bila chakula chochote. Wanapatikana kila siku wakirandaranda na kuombaomba hapa na pale kama watapata mtu yeyote atakayewapa kitu chotechote. Watoto hawa waliotelekezwa wanavalia nguo zilizochakaa. Wanavalia matambara. Aidha, hawana mahali pazuri pa kulala. Wanapatikana wamelala nje ya maduka au kwa mitaro. Ukosefu wa chakula unawafanya wao kuwaibia watu wengine vitu vyao na kisha wanatoroka. Wanaenda mashamba ya watu na kuharibu mimea yao. Hawaendi shuleni kusoma kwa sababu hakuna yeyote anawanunulia sare za shule, madaftari na vitabu vya kusoma).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyetelekezwa. Taswira ya mtoto

huyo ilijitokeza wazi katika lugha hiyo kwa vile alikosa mahitaji muhimu kama vile vyakula, nguo na mahali pa kuishi. Aidha, mtoto huyo alikosa mtu wa kumlea na kumtunza. Alisalia kuzunguka hapa na pale akitafuta msaada kutoka kwa wanajamii. Alikosa pia, mtu wa kumlipia karo na kumnunulia vitu alivyohitaji shuleni kama vile kalamu, madaftari, vitabu vya kusoma na sare za shule. Mtoto huyo vilevile alivalia matambara na kukosa mahali pazuri pa kulala. Alijihuzisha na vitendo viovu kama vile;kuwaibia watu vitu vyao au kufanya ukahaba kwa lengo la kutafuta hela za kumsaidia kununua vitu muhimu katika maisha.

## **2.2 Lugha chanya iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii**

Lugha chanya pia ilitumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii. Gudgeon (1991) alibainisha kuwa lugha chanya iliyotumiwa kwa mtoto na wanajamii walipoteteleza shughuli zao za kila siku iliibua hisia za furaha na kuchangamka baina ya wazazi, walezi na watoto. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa lugha hiyo ilipotumika kwa mtoto katika jamii ya Abagusii ililenga hasa kuweka wazi hali ya mtoto huyo alipokuwa akitekeleza jambo ambalo lilikubalika na wanajamii wote. Aidha, lugha hiyo ilichangia pakubwa hali ya ukuzaji wa maadili katika jamii ya Abagusii. Mtoto alikuwa katika hali iliyosababisha ushirikiano mwema baina yake na wanajamii wote. Sehemu hii imeshughulikia lugha chanya iliyowasilisha taswira za mtoto zifuatazo; kipaji maalumu, furaha, nidhamu, afya bora, bidii, ujasiri na aliyeishi katika mazingira ya utajiri.

### **2.2.1 Mtoto aliyekuwa na kipaji maalumu**

Kwa mujibu wa Alken (1979), Flynn (2012), Hunt (2011) na Gregory (1995) wamebainisha kuwa mtoto aliyekuwa na kipaji maalumu alikuwa na uwezo wa kufanya mambo kadhaa vyema kuliko watoto wengine. Wataalamu hawa pia wametoa dalili kadhaa za kumtambua mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu katika jamii. Mtoto huyo alikuwa na uwezo wa kufanya hesabu haraka kwa usahihi bila kupewa msaada wowote. Aidha, mtoto huyo aliweza kuwa na vipawa vingine kama vile kuimba kwa sauti nzuri, kubuni mambo kadhaa ya ajabu. Mtoto huyo vilevile aliweza kufikiri kwa haraka na kupata majibu sahihi kwa njia ya kushangaza. Mtoto huyo pia aliweza kuwaongoza watoto wengine kwa kuwaelekeza kufanya wajibu waliopewa kwa ufasaha.

Nao wataalamu wengine Freeman (2010), Gleik (2011) na Kamphaus (2005) walibainisha dalili nyinginezo zilizotumika katika kumtambua mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu ni; alikuwa na uwezo wa juu wa kufikiri kuhusu masuala kadhaa katika jamii, alikuwa na hamu kubwa ya kuelewa kiini cha matukio kadhaa katika jamii, alikuwa na uwezo wa kutumia msamiati sahihi katika mawasiliano. Mtoto huyo vilevile aliweza kuelewa kwa haraka kuhusu dhana mbalimbali bila kurudiarudia. Aidha, alitenda mambo yake kwa ukamilifu na alizoea kuuliza maswali watu waliokuwa mamlakani. Mtoto huyo pia alikuwa na shida kuwasiliana na watoto wengine kwa vile; alipenda vitu tofauti na watoto wengine, alipenda kufanya kazi tofauti na watoto wengine, alitumia msamiati tofauti na watoto wengine katika mawasiliano na maazimio yake yalikuwa tofauti na watoto wengine. Mtoto aliyekuwa na kipawa maalum pia aliweza kujitenga kutoka kwa watoto wengine na kufanya shughuli zake pekee.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu katika jamii ya Abagusii alijaliwa kuelewa na kufanya mambo aliyopewa kwa haraka mno bila kuhitaji msaada wa mtu mwingine. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa mtoto huyo alipendwa sana na wanajamii wote kwa vile alitekeleza majukumu aliyopewa bila maelezo mengi. Mtoto huyo pia aliweza kufikiria na kutenda mambo ambayo yaliwashinda watoto wengine na watu wazima. Pia, mtoto huyo alikuwa na ubunifu wa juu na alifikiria kuhusu mambo kadhaa kwa haraka na kupata majibu kwa njia ya ajabu mno. Aidha, mtoto huyo aliwaongoza watoto wengine kwa vile alijaliwa kuwa na vipaji tofautitofauti kama vile muziki, uigizaji na michezo mbambali.

Mfano wa lugha ilyowasilisha taswira ya mtoto mwenye kipaji maalumu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate ekegwa kiabene. Nigo agotegerera na koigwa bwango ekiganerie gokora. Ekeru okomotebia abange binto binde bionsi nigo agokora bo bwango. Koramoe chisabu akore nigo agochiaka bwango naende ochinyora chionsi. Nigo are nokobua komanya gento kende gionsi omento akorigia omotebia ase kere. Boigo nigo ere abwate okobua komanya ebirengererio bia abaibori baye gose banto bande bonsi bamoetanaine. Nigo boigo akobarorera abana bande amabera baria babwate emechando ende yonsi. Naende ere nigo abwate embua yoogwekorera ebinto biaye ere omonyene atari kogania banto bande bamokonye. (Mtoto huyu ana kipaji maalumu. Huwa anasikiliza na kuelewa mambo anayostahili kutenda kwa haraka. Ukimwambia apange vitu vyovyote yeye hufanya hivyo tena kwa haraka. Tena ukimpa zoezi lolote la hesabu yeye hufanya haraka na kupata zote. Ana uwezo wa kujua kitu chochote ambacho mtu anatafuta na mahali kilipo. Aidha, ana uwezo*

wa kuelewa mawazo ya wazazi wake au watu wanaomzunguka. Huwahurumia watoto wengine walio na shida. Tena yeye ana tabia ya kujitegemea zaidi badala ya kutafuta msaada kwa watu wengine).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na kipaji maalumu. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile alielewa mambo haraka, alipanga vitu kwa njia nzuri, aliweza kuyafahamu mawazo ya watu wengine, aliweza kujua mahali kitu kipo kilichokuwa kinatafutwa, aliwahurumia watoto waliokuwa na shida na kuwasidia na alipata alama zote katika kazi aliyopewa na mwalimu darasani.

### **2.2.2 Mtoto aliyekuwa na furaha**

Tabia ya mtoto kuchangamka na kupenda kucheza imejulikana tangu jadi kuchangia katika ukuaji wa mtoto kimwili, kihisia na kimawazo wakati alishirikiana na watoto wengine katika jamii (Fisher, 1992). Ingawa haijagunduliwa ni michezo ipi iliyochangia zaidi katika kuimarisha maisha ya mtoto kuchangamka katika jamii, Bundy na Skard (2008) wamebainisha kuwa tabia ya mtoto kuzaliwa huku akiwa na mazoea ya kucheza na kuchangamka wakati mwingine ni nzuri kwa vile ilijenga uwezo wa mtoto huyo kuwaza na kuwazua kuhusu michezo iliyostahili kucheza na wakati bora wa kuicheza. Majaribio kadhaa yaliyofanywa kwa watoto waliochangamka na kupenda kucheza kila siku yalidhihirisha kuwa watoto hao walikua na kuimarika (Goodale na wengine, 1999). Aidha, wataalamu Herrington na Studmann (1998) nao walibainisha kuwa watoto waliokuwa na



mazoea ya kuchangamka na kupenda kucheza waliweza kukuza vipawa vyao vya kufikiri na kubuni michezo waliostahili kucheza.

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii walichangamka na kupenda kucheza. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyechangamka na kupenda kucheza katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo asasogete naende ancheta kogosoria. Ere nigo are nomosasoko na kogosoria kera chingaki. Nigo akororekana koba nomogoko ase obosio bwaye. Boigo nigo akogoka amo nabanto bande chingaki chionsi. Naende, omwana oyo nigo akororekana are noomogoko egekogera nigo akonagoseka chingaki chionsi. Kero kende ere nigo agoaka eriogi riomogoko amo nabana bande. Nigo akonakobugia omororia asengencho abwate omogoko, nabo naende akona gotera amatera yomogoko, naboigo ere nabo akoiririata. Nabo chingaki chinde okomonyora omwana oyo okona kogosoria amo nabana bande. Omwana oyo nigo ogogete egekogera nigo akogosoria chigosoria aoao amo nabana bande buna ogocharoka engori, koruterana omopira, gose kominyokania aiga naaria. (Mtoto huyu amechangamka na anapenda kucheza. Huwa mchangamfu pia kwa watu wote. Ana furaha kwa vile anatabasamu kila wakati. Aidha, mtoto huyu ni mwenye furaha kwa vile hucheka wakati wote. Wakati mwingine anapiga kelele za furaha pamoja na watoto wengine. Furaha zake zikizidi yeye hupiga mbinja au anaendelea kuimba nyimbo za furaha, pia anaweza kushangilia. Wakati mwingine utampata akicheza pamoja na watoto wengine. Mtoto huyu ana furaha kwa sababu anacheza michezo mbalimbali na watoto wengine kama vile kuruka kamba, kurushiana mpira, au kukimbizana hapa na pale).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na furaha. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile alipenda kuchezeza na vifaa mbalimbali au na watu wengine, alirukaruka hapa na pale, alikimbia huku na kule, alitabasamu na wakati mwingine aliangua kicheko. Wakati alikosewa na watu wengine, aliendelea kuchangamka. Pia, alichangamka wakati alitumwa au kuagizwa na wazazi wake kufanya kazi yoyote.

Aidha, baadhi ya watoto waliokuwa na furaha walikuwa wacheshi. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto mcheshi katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo agonsekia ekeru okomorigeria buna eboetie, rigereria chianga chiaye nigo chire chitambe mono. Omwana oyo nigo abegeete chianga chinene chitamoisani. Omwana oyo nigo agonsekia buna agokwana ere nigo agokwana buna omwana obwate obotaba. Omwana oyo nigo agonsekia buna agotara ere nigo agotara buna omwana ore ekerema. Omwana oyo nigo agonsekia buna akogosoria ere nigo agocharoka ng'orang'ora ekeru ere akogosoria. Omwana oyo nigo agonsekia buna akoragera ere nigo akoragera bwangobwango naende agosokia endagera eria akoria korwa ase omonwa oye. (Mtoto huyu hunichekesha ninapomtazama jinsi amevalia, nguo zake ni ndefu mno. Mtoto huyu amevalia nguo ambazo ni kubwa mno ambazo hazimtoshi. Mtoto huyu hunichekesha jinsi anavyozungumza kama kigugumizi. Mtoto huyu hunichekesha jinsi anavyotembea kama mtoto mlemavu. Mtoto huyu hunichekesha jinsi anavyocheza yeye huruka polepole. Mtoto huyu hunichekesha jinsi anavyokula. Yeye hula kwa pupa na kutoa mdomoni kile chakula anachotafuna).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa mcheshi. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika maelezo kuwa alifurahi na kuwa mtulivu moyoni mwake. Alipenda kucheka na kuwachekesha watu wengine. Aidha, alibuni visa kadhaa vilivyowafanya watu kutabasamu au kucheka. Mtoto huyo pia aliweza kutumia ishara au vitendo mbalimbali kwa madhumuni ya kuwachekesha watu wengine katika jamii. Mtoto huyo alitambuliwa kwa kutumia mambo yafuatayo; alikuwa mwenye kutabasamu kila wakati, aliangua kicheko hata kabla ya kunena jambo lolote, alizungumzia kuhusu mambo yaliyosababisha mtu kucheka, alivalia mavazi kwa njia ambayo iliweza kusababisha watu kucheka na alitumia ishara ambazo ziliwachekesha watu wengine katika jamii. Mtoto huyo pia aliweza kutenda vitendo ambavyo ni vya kuchekesha. Ishara hizo na vitendo madhumuni yake yalikuwa ni kuchekesha watu wengine katika jamii. Mfano ni jinsi ya kusalimiana. Mtoto mcheshi aliweza kucheza densi huku akiwachekesha watu wengine kutokana na jinsi alivyocheza.

### **2.2.3 Mtoto aliyekuwa na nidhamu**

Nerlove (1969) alibainisha kuwa jamii ya Abagusii ilizingatia kuwa watoto wote walistahili kuwa na nidhamu. Mtaalamu huyo ameorodhesha mambo kadhaa yaliyosababisha watoto kubadilisha tabia zao katika jamii ya Abagusii. Mfano wa mambo hayo ni kukosa kufundishwa na wazazi wake kuhusu maadili yaliyostahili kuzingatiwa katika jamii ya Abagusii. Aidha, marafiki nao walichangia katika kuwashawishi watoto kubadilisha tabia zao. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii. Mtoto aliyekuwa na nidhamu aliwafurahisha wanajamii wote. Jamii ya Abagusii

ilisisitiza umuhimu wa mtoto kuwa na nidhamu katika maisha yake. Umuhimu wa mtoto kuwa na nidhamu ni kuwa ilimwezesha kutenda mambo mema katika jamii kama vile kuwaheshimu watu wengine katika jamii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate amasikani. Ere nigo are omoigweri ase abaibori baye ekeru bakomotoma ande onsi. Amasikani abwate nigo akoyaorokia goetera amakwania. Nigo akobakwania abanto bonsi na amaboko abere kobaorokia nabasigete. Rora buna omwana oyo omoimokeire omonto omonene ekerogo ase engencho ere abwate amasikani. Naboigo omwana oyo nigo abwate amasikani ase enkwana yaye enyororo. Nigo akobakorera abanto bande amang'ana amaya, naende tokomonyora okobakorera ayare amabe. Nigo akobeka chianga chia amasikani chitari komoa bosoku bonde bwensi. Ogotara kwaye nigo kore okuya gotabwati bwerori bonde bwensi ase obogima bwaye. Nigo ere agotenena ekeru abanto abanene bagoeta ang'e nase are. (Mtoto huyu ana nidhamu. Anawatii wazazi wake wakati wanamtuma mahali popote. Nidhamu aliyo nayo huonekana wazi kupitia salamu. Anawasalimu watu wote kwa mikono miwili kuonyesha kuwa anawaheshimu. Tazama vile mtoto huyu amesimama ili mtu mzima aketi kwa vile ana nidhamu. Aidha, mtoto huyu ana nidhamu jinsi anavyozungumza kwa sauti ya upole. Anawatendea watu wengine mambo mema na wala hawatendei yaliyo chukizo kwao. Anavalia nguo nzuri ambazo zinadhihirisha nidhamu yake na wala haziwezi kumwaibisha. Kutembea kwake ni kuzuri kwa sababu hana maringo yoyote maishani mwake. Anasimama anapowaona watu wazima wakipita karibu naye).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na nidhamu. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika lugha hii kwa vile alikuwa mtiifu kwa wazazi wake, alisalimia watu kwa kutumia mikono miwili, alizungumza kwa njia ya upole, alitenda mambo mema, alivalia mavazi yaliyokubalika na alitembea kwa mwendo mzuri bila maringo. Aidha, mtoto huyo alikuwa mnyenyekevu katika maisha yake na alikuwa na tabia nzuri.

#### **2.2.4 Mtoto aliyekuwa na afya**

Mtoto aliyekuwa na afya alistahili kupewa lishe bora kila wakati. Lishe bora ni jumla ya hatua mbalimbali tangu chakula kinapoliwa na jinsi mwili wa mtoto unavyochukua virutubisho vinavyopatikana katika aina mbalimbali ya vyakula ambavyo ni muhimu kuufanya mwili wa mtoto uwe na afya na kua. Afya ya mtoto hutokana na ulaji unaofaa, yaani chakula cha kutosha, chenye mchanganyiko wa virutubisho vyote katika uwiano unaotakiwa. Virutubisho hivyo vimegawanywa katika makundi matano makuu. Makundi hayo ni kabohaidreti, mafuta, protini, vitamini na madini. Afya ya mtoto ilijumuisha kutokuwepo kwa magonjwa hasa yale ya kuambukiza kusababisha mtoto kuwa mwenye siha ya mwili na akili vilivyochangia katika kuboresha ufyonzaji na matumizi ya virutubisho mwilini.

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa na afya katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na afya katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo tabwati borwaire bonde bwonsi egekogera are buya ase omobere oye. Nigo ere abwate obogima obuya ase engencho akoegwa ebinto bionsi aganetie na abaibori baye. Nigo ere akoria chindagera chingiya mono kera rituko chiokwagacha omobere oye. Naende boigo omwana oyo nigo amenyete ase are agiya mono. Tabwati bokong'u bonde bwensi ase obogima bwaye nonya ng'ake. Ekeru okomorigereria buya nigo anorete, anchete kona kogosoria amo nabana bande. Boigo omwana oyo agwesibia kera rituko na kweboyia chianga chindabu. Nigo omwana oyo akorara ase are agiya mono. Nyore nebirarero biaye nigo bigosibigwa kera chingaki tabaisa konyora borwaire bonde bwensi. (Mtoto huyu hana ugonjwa wowote kwa vile ni mwenye afya. Anaishi maisha mema kwa vile anashugkulikiwa mahitaji yake yote na wazazi wake. Hupokea vyakula vizuri kila siku vya kujenga mwili wake. Aidha, anaishi mahali pazuri mno. Hana shida yoyote katika maisha yake. Ukimtazama kwa makini yeye ni mnene, anapenda kucheza na watoto wengine. Mtoto huyu pia anaoga kila siku na kuvalia nguo ambazo zimevuliwa. Mtoto huyu hulala mahali pazuri mno. Hata mablanketi pamoja na vitambaa anavyolalia viwe vinafuliwa kila mara ili asipatikane na maradhi yoyote).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na afya. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kupitia kwa maelezo kuwa hakuwa na ugonjwa wowote, alikula vyakula vilivyojenga mwili, alivalia mavazi safi na aliishi na kulala mahali pazuri. Aidha, mtoto huyo alichangamka, alicheza na watoto wengine na alikuwa na mawazo yaliyokuwa yametulia kwa vile alitimiziwa mahitaji yake yote na wazazi wake.

### 2.2.5 Mtoto aliyekuwa na bidii

Kwa mujibu wa TUKI (2004), bidii ni ari ya kufanya jambo. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walifanya bidii katika shughuli zao zote walizotekeleza katika jamii ya Abagusii. Baadhi ya watoto walifanya bidii kwa vile walitaka kufanikiwa maishani mwao. Hata shuleni watoto wote walihimizwa kutia bidii katika masomo yao na shughuli nyinginezo kama vile michezo. Watoto waliojitahidi katika kazi yoyote, walipewa tuzo na wanajamii kama njia ya kuwapa moyo. Pia, walitumika kuwa vielelezo kwa watoto wengine ili nao wafanye jitihada kwa kazi walizopewa. Aidha, shuleni watoto waliofanya bidii walitumika na walimu kuwaelezea marafiki zao jinsi ya kuzoa alama za juu na kuwahimiza kufanya juhudi ili waweze kufaulu katika mitihani waliyopewa na walimu wao. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na bidii katika jamii ni:

*Omwana oyo nigo are nomokia ase emeremo yaye agokora, naende ere nigo agosaseria ase emeremo yaye. Omwana oyo nigo anchete gosoma amo na abana bande kera chingaki nario aranyare goeta amatemu aye. Omwana oyo ere nigo anchete gosoma kera chingaki. Nigo okomonyora ere esiekererete nyomba ekero agosoma abanto tibamwakera eriogi rinde rionsi. omwana oyo nigo abwate omokia ase egasi yaye naende ere nigo agokora nenchinguru chiaye chionsi egasi ende yonsi akoegwa buna okorema mogondo, okorabi obonyansi, okoruga ndagera ende yonsi, nyore gosibia ebinto ao ao ase enka. (Mtoto huyu ni mwenye bidii katika kazi anayotenda, pia hung'ara katika kazi zake. Mtoto huyu anapenda kusoma pamoja na watoto wengine kila wakati ili aweze kupita mitihani yake. Mtoto huyu anapenda kusoma kila wakati. Unampata amejifungia ndani ya nyumba ameketi akisoma ili watu wasimpigie kelele zozote. Mtoto huyu ana bidii katika kazi yoyote anayofanya*

tena yeye anaifanya kwa nguvu zake zote kazi yoyote anayopewa kama vile kulima shambani, kufyeka nyasi, kupika chakula chochote na hata kuosha vitu mbalimbali katika familia).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mawasiliano huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na bidii. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika maelezo kuwa alijitolea kwa vyovyote vile kufanya shughuli yoyote iliyomhusu kwa bidii. Alipendwa pia, na wazazi wake kwa vile alifanya kazi yake kwa bidii. Hakupenda kamwe maishani mwake kuzembea kazini. Mtoto huyo vilevile, aliweza kufanya kazi kwa haraka. Mtoto huyo pia, alikuwa kielelezo kwa watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Aidha, alifanya kazi yake kwa bidii huku akiwa na nia ya kumaliza haraka kisha aende kutenda mambo mengine. Kazi ni nyingi alitenda kwa bidii kama vile kulima shambani, kutayarisha vyakula jikoni, kubeba mizigo kama vile mavuno kutoka shambani hadi nyumbani, kukata nyasi, kufua nguo, kusoma shuleni na kazi nyinginezo.

#### **2.2.6 Mtoto aliyekuwa na ujasiri**

Ujasiri ni hali ya kukabili jambo bila ya hofu. Ni uhodari au ushujaa wa kufanya jambo (TUKI, 2004). Watoto katika jamii ya Abagusii walishahuriwa kuwa wenye ujasiri. Walihimizwa kuwa mashujaa katika kutetea mila na desturi katika jamii ya Abagusii. Aidha, walifundishwa mambo kadhaa ya kuzingatia kama vile nidhamu, bidii na uadilifu yaliyowawezesha kuwa mashujaa wa kutajika. Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa wenye ujasiri katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na ujasiri ni:



*Omwana oyo nigo abwate oboremu naende tari kogoseka chingaki chionsi na ng'ana ende yonsi gose monto onde bwensi. Nigo abwate oboremu ase obogima bwaye bwensi. Nyore tabwati oyokomokonya ebinto aganetie buna andagera, chianga gose enyomba nyore karemeire ere nigo are omoremereria. Boigo ekeri okomotebia omwana oyo atenene bosio bwa omoganda bwa abanto ere tari kwoboa ase engecho are omoremu. Naende nabo agotenena bosio bwa abanto abange; atere ogotera, aire risairi, aegie egosorio, atebie abande omogano, abakwanere abanto abange na kobaa obosemia bonde bwonsi. (Mtoto huyu ni mwenye ujasiri na hawezi kutishwa nyakati zote na jambo lolote au mtu yeyote. Ana ujasiri wa kutosha katika maisha yake hata kama hana mtu yeyote wa kumsaidia mahitaji yake kama vile chakula, nguo na nyumba. Hata kama ana upungufu huu, yeye ni mvumilivu na ana ujasiri wa kutosha kustahimili haya yote. Aidha, mtoto huyu anaweza kusimama mbele ya umati wa watu bila kuwa na haya kisha; aimbe wimbo, akariri shairi, aigize mchezo, atoe hadithi, awashauri watu, awazungumzie watu na kuwapa mawaidha yoyote).*

Mhimili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila mawasiliano huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyekuwa na ujasiri. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi katika maelezo kuwa hakuogopa kitu chochote katika maisha yake. Mtoto huyo alizaliwa akiwa na ujasiri na hakushtuliwa na mtu au kitu chochote. Mtoto huyo vilevile, aliweza kufanya mambo kadhaa bila woga. Pia, mtoto huyo alionyesha umahiri wake wakati alishughulikia majukumu mbalimbali katika jamii. Aliweza kuyatenda majukumu hayo kwa bidii na moyo wa kufanikiwa. Hata wakati alipewa kazi ngumu kalijitolea kwa nguvu zake zote. Mifano iliyobainishwa katika utafiti huu iliyodhihirisha

kuwa mtoto alikuwa na ujasiri ni; alitembea gizani bila woga, hakuhtuliwa na mnyama au kitu chochote, hakulia japo alikuwa na maumivu mwilini mwake, alivumilia mateso ya kila aina na aliweza kusimama mbele ya watoto wengine na kuwahutubia bila kuogopa hadhira yake.

### **2.2.7 Mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri**

TUKI (2004), wamebainisha kuwa utajiri ni hali ya kuwa na mali nyingi. Mfano wa mali yaliyomilikiwa na watu matajiri ni mabilioni ya pesa, magari ya kifahari, mashamba mengi na makubwa, majengo ya gorofa, vyakula vya kila aina na wanyama wengi waliofugwa kama vile ng'ombe na mbuzi. Baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii waliishi katika mazingira ya utajiri. Watoto hao walifurahia maisha kwa vile walitimiziwa haja zao za kila siku bila shida yoyote. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri ni:

*Omwana oyo nigo amenyete ase enka ya abanda. Nigo ere arendire buya ase obogima bwaye. Nigo akoegwa ebinto binde bionsi aganetie ase obogima bwaye. Nigo akoria endagera engiya naende egwansa nigo akoria mbaka ere oigota. Nabo ere agosaba gento kende gionsi abaibori baye bamogorera kiagera bakwenyara. Nigo omwana oyo akoboigwa buya naende ere nigo akobekerwa ebinto bierigori mono. Chianga nabo aranchencherigwe ara gatato ase rituko. Nigo akobeka ebikoroto ebiya naende bie rigori ria igoro. Omwana oyo nigo akorara ase agiya mono. Nigo akorera omoito omuya, bwebisia amarangeti ne ebitambaa bibwate riberera. Nigo akoirwa esukuru nakoiranigwa nka ase egari naende boigo nigo*

*agosoma esukuru ya abana abanda. Nigo okonyora amatuko amange are nomogoko egekogera taremeirie na gento kende gionsi ase obogima bwaye.* (Mtoto huyu anaishi katika familia ya matajiri. Anatumzwa vizuri sana katika maisha yake. Huwa anapewa vitu vyovyote anavyohitaji maishani mwake. Hula vyakula vizuri tena vitamu hadi akashiba. Huomba kitu chochote na kupewa kwa vile wazazi wake wana uwezo wa kuvinunua. Mtoto huyu anavalishwa vizuri na huvalishwa vitu vya bei ya juu. Anaweza kubadilishiwa nguo mara tatu kwa siku. Anavaa viatu vya bei. Mtoto huyu hulala mahali pazuri mno. Analalia mgodoro mzuri, anajifunika mablanketi na vitambaa vyenye joto. Huchukuliwa shuleni na kurudishwa nyumbani kwa gari tena yeye husoma shule ya matajiri. Siku nyingi yeye huwa mwenye furaha kwa sababu anatumiziwa mahitaji yake yote na wazazi wake).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawsiliano ulihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ilikuwa mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri. Taswira ya mtoto huyo ilijitokeza wazi kwa vile aliishi katika nyumba ya kifahari, wazazi wake pia walikuwa na magari kadhaa, alitumiziwa mahitaji yake yote. Aidha, mazingira ya utajiri yalikuwa na mandhari ya kupendeza. Aidha, mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri alivalia mavazi ya kupendeza na wazazi wake walikuwa na uwezo wa kumnunulia mavazi mazuri ya bei ya juu. Walimnunulia mavazi hayo ishara tosha kuwa walimpenda mtoto wao. Mtoto huyo naye aliyabadilisha mavazi hayo kila mara. Mtoto huyo pia alivalia viatu miguuni mwake. Aidha, mtoto huyo alilala katika kitanda kizuri cha bei ya juu. Kitanda hicho kilikuwa na godoro, vitambaa na mablanketi ya rangi za kupendeza. Vyote hivi vilimwezesha wakati alijifunika kuwa na joto. Pia, kitanda hicho kilizingirwa na

chandarua ili kumkinga asishambuliwe na mbu. Mtoto huyo vilevile, alipewa lishe bora katika maisha yake. Hali hii ya kupewa lishe bora asubuhi, mchana na jioni ilimwezesha mtoto huyo kuwa na afya. Mtoto huyo vilevile alipewa fursa ya kujichagulia vyakula vya kupikiwa.

### **2.2.8 Mtoto aliyependa kucheza**

Michezo huchangia katika ukuaji wa mwili, akili, hisia na ushirikiano wa mtoto na watoto wengine katika jamii (Fisher, 1992). Ingawa watafiti hawajagundua ni michezo gani huchangia zaidi katika ukuaji wa taswira ya mtoto katika jamii, Bundy na Skard (2008) walihoji kuwa hali ya mtoto kuzaliwa akiwa na mazoea ya kucheza hapa na pale ilimwezesha mtoto huyo kuimarisha kipawa chake cha kufikiria kuhusu michezo aliyostahili kucheza na wakati mwafaka wa kuicheza. Aidha, utafiti uliofanywa na wataalamu Herrington na Studmann (1998) ulidhihirisha kuwa watoto waliozoea kucheza walikuza vipawa vya kubuni, kushirikiana na hata kuwa wachangamfu wakati wote. Madai hayo yalishabihiana na utafiti wa O'Brien (2000) na Stepenson (2003) walidai kuwa michezo hukuza vipawa vya watoto vya kufikiria jambo lililostahili kutekelezwa wakati walikuwa wakicheza. Pawson na Tranter (2001) walishangaa kuwa baadhi ya wazazi waliwazuia watoto wao kwenda kucheza. Wazazi hao walifanya hivyo kwa vile walihofia usalama wa watoto wao wakati walikuwa wakicheza na watoto wengine. Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyependa kucheza katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anchete kogosoria chigosori aoao. Naende, nigo anchete kona kominyokania amo nabana bande aiga naria. Chingaki chinde nigo agoaka omopira bwa amagoro amo nabasani baye. Chigosori chinde anchete kogosoria amo nabana*

*bande akeru babwate ribaga nogotuma, onyuro, ogocharoka engori na korwana enyameni. Nigo akobeka chigori chinyinge ekeru bakogosoria amo nabana bande asengecho amanyete goaka omopira bwa amagoro buya. (Mtoto huyu anapenda kucheza michezo mbalimbali. Anapenda kukimbizana hapa na pale wakiwa na watoto wengine. Wakati mwingine, anacheza kandanda na marafiki zake. Michezo mingine anayopenda kucheza pamoja na watoto wengine wakati wana nafasi ni kuruka, kurushiana mpira, kuruka kamba na miera. Anafunga mabao mengi wakati wanacheza na watoto wengine kwa vile ana umahiri wa kucheza mchezo huo).*

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ilihusu kila mazungumzo huwa na mada. Mada ya mfano wa lugha hii ni mtoto aliyependa kucheza. Mfano wa lugha unafafanua kuwa moto huyo alicheza michezo mbalimbali na marafiki zake. Maelezo zaidi ni kuwa mtoto huyo alipata fursa nzuri ya kuimarisha kipawa chake kucheza. Ujuzi wake wa kucheza mchezo wa kandanda ulimwezesha kufunga mabao mengi. Aidha, mtoto huyo alipenda michezo wa kuruka kamba na kurushiana mpira na watoto wengine. Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa mtoto huyo alipendwa na watoto wengine kwa vile alicheza vizuri na kuwafurahisha wanajamii wote. Wazazi wa mtoto huyo pia walimiminiwa sifa tele kwa vile mtoto wao alikuwa na kipawa cha kucheza mchezo wa kandanda.

### **2.3 Hitimisho**

Sura hii ya pili imeshughulikia maelezo ya kimsingi kuhusu lugha hasi na chanya iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Lugha hasi iliyobainishwa na kuchanganuliwa ni ya mtoto: mgonjwa, mlemavu, yatima, aliyeishi katika mazingira ya

umaskini, aliyetumia pombe na dawa za kulevya, mwizi, aliyefanya uasherati, aliyewatusi watu wengine, aliyepigana na watoto wengine, zeruzeru, mzembe, aliyeolewa, aliyeoa, aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu na aliyetelekezwa. Aidha, lugha chanya iliyobainishwa na kuchanganuliwa ni ya mtoto aliyekuwa na: kipaji maalumu, furaha, nidhamu, afya, bidii, ujasiri na aliyeishi katika mazingira ya utajiri. Sura ifuatayo imeshughulikia dhima za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

## **SURA YA TATU**

### **DHIMA ZA LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO KATIKA JAMII**

#### **YA ABAGUSII**

##### **3.0 Utangulizi**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii imejadiliwa katika sura ya pili. Lugha hiyo ilibainishwa kwa njia ya maelezo. Lugha hasi na chanya ilitumiwa katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Sura hii, imeshughulikia dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Uchanganuzi wa dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii uliongozwa na nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano.

Mhimili wa mada ulimwezesha mtafiti kubainisha mada mbalimbali zilizozungumziwa katika lugha hiyo na kisha kutambua dhima yake. Mhimili mwingine wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliotumika katika uchanganuzi huu ni ule uliohusu muhtadha wa mazungumzo. Mazingira ya mtoto au mahali ambamo mawasiliano yalikuwa yakifanyika na hata jinsi mambo yalivyotendwa na wazazi na walezi wa watoto yaliwawezesha kuteua lugha mwafaka iliyowasilisha dhima ya ujumbe wao kwa mtoto aliyezungumziwa.

Aidha, mhimili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliohusu wahusika ulitumika katika kubainisha dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mhusika aliyezungumziwa ni mtoto na wahusika wengine waliomzungumzia ni; wazazi wake, walezi wa watoto na watu wengine walioishi na mtoto. Ufanisi wa kutambua kuhusu

dhima ya lugha iliyotumika kwa mtoto yeyote katika jamii ya Abagusii ulitegemea umahiri wa mzungumzaji kuteua lugha iliyostahili kuwasilisha taswira ya mtoto husika

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliohusu sababu za mawasiliano ulimwezesha mtafiti kuchanganua dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mazungumzo yoyote yaliyoelekezwa kwa mtoto na wazazi, walezi wa mtoto au watu walioishi naye, yalikuwa na sababu maalumu ya kufanya hivyo. Sababu hiyo ilimwezesha mtafiti kubainisha dhima ya lugha hiyo kwa mtoto aliyezungumziwa. Dhima zilizodhihirika wazi katika mazungumzo kwa mtoto na zimechanganuliwa katika sura hii ni kuelimisha, kukuza maadili, kuonya, kurekebisha tabia, kuwasiliana, kutia motisha, kusifu, kufariji, kulinganisha, kushauri na kukemea.

### **3.1 Kuelimisha**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika katika kumwelimisha mtoto katika jamii ya Abagusii. Elimu ilikuwa muhimu kwa mtoto yeyote katika jamii ya Abagusii. Aidha, lugha hiyo ilitumika kama chombo cha kupitisha maarifa kutoka kwa watu wazima hadi kwa watoto. Elimu hiyo vilevile iliwapa watoto ujuzi na stadi za kutenda mambo mbalimbali katika jamii. Pia, lugha hiyo ilitumiwa kuwaelekeza watoto jinsi ya kuwa na mielekeo bora katika jamii. Lugha hiyo iliwahimiza watoto wawe na mazoea ya kutenda mambo mema kama vile kukuza maadili na adabu, Watoto pia walielimishwa wachukie vitendo viovu kama vile ufisadi. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu tabia, jinsi ya kufanya kazi na umuhimu wa kutia bidii katika masomo.



### **3.1.1 Kumwelimisha mtoto kuhusu tabia**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimwelimisha mtoto kuhusu alivyostahili kuwa na tabia nzuri. Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyezoea kutumia pombe au dawa za kulevya tazama 2.1.5 alielimishwa kuhusu madhara yake na kuhimizwa kuwa mwenye tabia nzuri. Aidha, mtoto aliyekuwa na mazoea ya kupigana na watoto wengine tazama 2.1.9 alielimishwa kujiepusha kupigana na kuwa mwenye tabia ya kuwapenda watoto wengine. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimwelimisha mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya vilevile umuhimu wa kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

#### **3.1.1.1 Kumwelimisha mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyotumika kumwelimisha mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo, nekogwenerete otige konywa amarwa na amariogo yogotindia nario orabe omwana ore nechimbua chingiya gochia ase abanto bande ase egesaku Kiomogusii. Boigo, manya buna amariogo agotindia nigo agosaria obongo na ebimo biomobere. Naende, amariogo yogotindia nabo akogera abanto babe noborwaire, baetane gose korwana amo nabanto bande. (Mtoto huyu, unastahili kujiepusha kunywa pombe na dawa za kulevya kisha uwe mwenye tabia nzuri kwa watu wengine katika jamii ya Abagusii. Aidha, dawa za kulevya zinaharibu ubongo na vinevyo vya mwili. Pia, dawa za kulevya zinaweza sababisha mtu kuwa mgonjwa, kukosana au kupigana na watu wengine).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano katika lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa mtoto aliyezungumziwa alielimishwa kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii. Elimu hiyo iliweza kumsaidia mtoto huyo kubadilisha tabia yake na kuacha kutumia pombe na dawa za kulevya. Aidha, elimu hiyo iliwasaidia watoto wengine kuwa macho wasije wakaanza kutumia pombe na dawa za kulevya katika maisha yao.

### **3.1.1.2 Kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kuwapenda watu wengine**

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyotumika ni:

*Omwana oyo, tiga kona kobachegia na korwana amo na abana bande manya buya nabo orabaake na kobaita gose kobatigera chingoma ase emebere yabo. Boigo, manya gokobaita gose kobakorera kende kebe, nigo naye okoimoikerigwa egetambokero ekenene. Gokwanga koigwa obosemia bwane rirorio aye nigo okoragererigwa na abagagaka ase obogima bwao bwonsi. (Mtoto huyu, jiepushe kupigana na watoto wengine fahamu kuwa unaweza kuwapiga na kuwaua au kuwasababishia majeraha katika miili yao. Aidha, fahamu kuwa ukiwapiga na kuwatendea mabaya, unaweza kuchukuliwa hatua kali. Ukiyapuuza mawaidha yangu utalaaniwa na wazee katika maisha yako yote).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnogarafia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya lugha hii ni kuwa kumwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kuwapenda watu wengine katika jamii. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa mtoto aliyekuwa na taswira ya kupigana na watoto wengine alielimishwa kuhusu umuhimu wa kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Lengo hasa la elimu hiyo ilikuwa kujenga uhusiano na ushirikiano baina ya watoto, ili wasaidiane katika kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii ya Abagusii. Aidha, elimu hiyo ilipunguza visa kadhaa viovu vilivyotendwa na watoto kama vile kuchukiana na kutusiana.

### **3.1.2 Kumwelimisha mtoto jinsi ya kufanya kazi**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa lugha hiyo ilimwelimisha mtoto kuhusu jinsi alivyostahili kufanya kazi kwa bidii. Mfano ni mtoto mzembe tazama 2.1.11 alielimishwa kuacha uzembe wake na kuwa na mazoea ya kufanya bidii katika kazi aliyotenda. Mifano ya lugha hiyo ni ile iliyomhimiza mtoto kufanya bidii katika masomo yake shuleni na katika kazi mbalimbali alizoambiwa kutekeleza katika jamii ya Abagusii. Mifano ya mambo aliyoelimishwa mtoto ni kufanya kazi bila kunung'unika, kufanya kazi kwa bidii na kuwa na ari ya kufanya kazi katika jamii ya Abagusii.

#### **3.1.2.1 Kumwelimisha mtoto kufanya kazi bila kunung'unika**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika kumwelimisha kuhusu kufanya kazi bila kunung'unika ni:

*Nabo omwana oyo agokora omokia ase emeremo ende yonsi ogotebigwa gokora nonde bwensi otari kwemurungania. Naende boigo, nabo ogotema gokora emeremo eyio ase omoroberio obene, bwango naende buya erio nario orabagokie abanto boni. (Mtoto huyu hufanya kazi yoyote anaagizwa kufanya na mtu yeyote bila kunung'unika. Aidha, jaribu kufanya kazi kwa mpango maalumu, haraka tena vizuri ili kuwafurahisha watu wote).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano katika lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto huyo umuhimu wa kufanya kazi bila kunung'unika. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimwelimisha mtoto huyo kufanya kazi bila manung'uniko yoyote. Elimu hiyo ilimpa mtoto huyo moyo wa kufanya kazi kwa bidii katika jamii ya Abagusii. Pia, elimu hiyo ilimsaidia mtoto huyo kujishughulisha na kufanya kazi yoyote kwa lengo la kuongeza mapato katika familia.

### **3.1.2.2 Kumwelimisha mtoto kufanya kazi kwa bidii**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha kuhusu kufanya kazi kwa bidii katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo agokora egasi ende yonsi akoegwa ase omokia yagera okora bwango na koinoka korwa mogondo. Naboigo goetera omokia abwate nigo tokomoa naende emeremo ende egekogera nigo agokora atari kwemurungania. (Mtoto huyu anafanya kazi yoyote anayopewa kwa bidii inamfanya anamaliza kwa haraka na*

kutoka shambani. Kupitia kwa bidii zake anapewa kazi nyingine kwa sababu yeye hufanya kwa bidii bila kulalalmika).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu za mawasiliano katika lugha hii ni kumwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kutenda kazi yoyote aliyoagizwa kufanya kwa bidii. Pia, lugha hiyo ilimwelimisha mtoto huyo kufanya kazi vizuri bila kupewa maagizo kila mara na mtu mzima.

### **3.1.2.3 Kumwelimisha mtoto kuwa na ari ya kufanya kazi**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha kuhusu kupenda kufanya kazi katika jamii ya Abagusii ni:

*Nigo okomonyora omwana oyo chingaki chionsi atari kogosoria amo nabana bande.*

*Nigo ere anchete gokora emeremo agotebigwa gokora nabaibori baye nomokia. Bono*

*iga oisire gotabokia agende gokora emeremo ende araegwe nabaibori baye.*

(Unampata mtoto huyu kila wakati hachezi na watoto wengine. Anapenda kufanya kazi anayoagizwa kufanya na wazazi wake kwa bidii. Sasa hivi tazama amekaribia kukamilisha sehemu yake aende kufanya kazi nyingine atakayoambiwa kufanya na wazazi wake).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mawasiliano katika lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto umuhimu wa kuwa na ari ya kufanya kazi. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu kuwa na moyo wa kufanya kazi. Aidha, mtoto huyo alielimishwa kuhusu umuhimu wa kupenda kufanya kazi katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo vilevile, ilimwelimisha mtoto mzembe kufanya kazi kwa bidii katika jamii ya Abagusii.

### **3.1.3 Kumwelimisha mtoto umuhimu wa kutia bidii katika masomo**

Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimwelimisha umuhimu wa kutia bidii katika masomo yake. Mtoto alipokea fursa ya kueleza jinsi ya kufaulu na kuendeleza masomo yake, jinsi ya kuwasidia watoto wengine kuendeleza masomo yao na mambo muhimu yaliyostahili kuzingatiwa ili mtoto aweze kupita mitihani yake yote.

#### **3.1.3.1 Kumwelimisha mtoto jinsi ya kufaulu mitihani na kuendeleza masomo**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha jinsi ya kufaulu na kuendeleza masomo yake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo agokora omokia ase amasomo aye, nario oraete na kogenderera gosoma amasomo ande ase ekerasi kende gekobwatia. Nigo agokora omokia, atari gokonywa na monto onde bwensi, amatuko agocha nigo arabe enamba eyemo na kobatang'anera abana bonsi bagosoma nere. Boigo, negwenerete omwana oyo koiraneria amaborio buya naende koenekia buna oiranerie amaborio onsi*

*koreng'ana na amachiko aeire.* (Mtoto huyu hufanya bidii katika masomo yake, ili aweze kufaulu na kuendelea na masomo zaidi katika darasa linalofuata. Anafanya bidii bila kupewa msaada wowote na mtu yeyote, siku zijazo atakuwa wa kwanza na kuwatangulia watoto wote wanaosoma naye. Aidha, anastahili kuwa macho wakati wa kujibu maswali na kuhakikisha kuwa amejibu maswali yote kulingana na maagizo).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano katika mfano wa lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto huyo kuhusu jinsi ya kufaulu katika mitihani na kuendeleza masomo yake. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha kuhusu mbinu mbalimbali za kutumia ili aweze kufaulu katika mitihani yake. Wanajamii vilevile walitumia lugha hiyo kumwelimisha mtoto kuhusu mbinu zilizomwezesha kufaulu katika masomo yake. Mfano wa mbinu hizo ni kuyajibu maswali kwa uangalifu na kuhakikisha kuwa alijibu maswali yote kulingana na maagizo aliyopewa.

### **3.1.3.2 Kumwelimisha mtoto umuhimu wa kuwasaidia watoto wengine kuendeleza masomo**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha kuhusu jinsi ya kuwasaidia watoto wengine kuendeleza masomo yao katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are nomokia ase amasomo aye. Omokia abwate ogerire are nokobua kobakonya abana bande ase okobaorokereria chinchera bagwenerete*

*kobwatia erio banyare gokora amang'na ande onsi amakong'u ase amasomo abo.*  
(Mtoto huyu anafanya bidii katika masomo yake. Bidii zake zimemwezesha kuwa na uwezo wa kuwapa msaada watoto wengine kwa kuwaonyesha njia za kutumia kusuluhisha mambo magumu katika masomo yao).

Mhimili wa tano wa nadaharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano katika mfano wa lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto kuhusu umuhimu wa kuwasidia watoto wengine kuendeleza masomo yao katika jamii. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha kuhusu umuhimu wa kuwasaidia watoto wengine katika kuendeleza masomo yao. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kushirikiana na watoto wengine. Watoto walishauriwa kushirikiana na watoto wengine wakati walitenda kazi yoyote katika jamii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumwelimisha mtoto jinsi ya kuondoa ubinafsi na kujenga uhusiano wa kushirikiana na watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

### **3.1.3.3 Kumwelimisha mtoto mambo muhimu ya kuzingatia kufaulu mitihani**

Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha kuhusu mambo muhimu aliyostahili kuzingatia maishani mwake ili aweze kufaulu mitihani yake yote katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo okorire omokia ase amasomo aye. Omokia abwate ogerire ere goeta amatemwa aye onsi. Omokia oye boigo ogerire abeire bweritang'ani ase abana riga erimo bakorete amatemwa amo nere.*(Mtoto huyu amefanya bidii katika masomo



yake. Bidii zake zimemwezesha kufaulu katika mitihani yake yote. Aidha, bidii zake zimemwezesha kuwa wa kwanza miongoni mwa watoto mia moja waliofanya mitihani hiyo pamoja naye).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia ili aweze kufaulu katika mitihani yake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kupita mitihani yake shuleni.

### **3.2 Kukuza maadili**

Dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni ile ya kukuza maadili. Maisha ya mtoto yalizungukwa na mambo kadhaa. Mtoto alistahili kuelewa na kuzingatia maadili katika maisha yake. Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa maadli yaliyozungumziwa katika lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ni uaminifu, heshima, mavazi yaliyostahili kuvaliwa na umuhimu wa kuwapenda watu wengine katika jamii ya Abagusii.

#### **3.2.1 Uaminifu**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilichangia pakubwa katika kukuza uaminifu katika maisha ya mtoto. Mtoto mwaminifu ni yule aliyezoea kusema ukweli kwa kila jambo. Mtoto huyo alipewa amana za watu kuzitunza hadi wakati zilihitaajika

kutumika na wenyewe. Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto mwaminifu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omoegenwa. Ekeru okomotoma akogorere kende gionsi korwa etuka, kerabe oiranerigwe chibesa chinde, nigo agokoa chionsi tari kobisa chinde chionsi. Naende nigo anarete goteba ekeene. Tabwati embwa yokong'ainereria ase obogima bwaye. Boigo, asengencho are omoegenwa nigo akoegwa ebinto aoao buna chibesa gochigacha goika ekeru chikoganerigwa.* (Mtoto huyu ni mwaminifu. Ukimtuma kununua kitu chochote kutoka kwa duka, anahakikisha kuwa pesa zilizosalia amekuletea, bila kuchukua kiasi chochote. Aidha, yeye husema ukweli wakati wote. Hana tabia ya kudanganya katika maisha yake. Pia, kwa vile yeye ni mwaminifu hupewa vitu mbalimbali kama vile pesa kuziweka hadi wakati zitahitajika).

Mhimili wa tano wa Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya Mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto huyo umuhimu wa kuwa mwaminifu. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwelimisha jinsi ya kuwa mwaminifu. Aidha, lugha hiyo ilimwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kujenga kiwango chake cha uaminifu katika maisha yake na watu wengine katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo vilevile ilitumika katika kupunguza udanganyifu miongoni mwa watoto katika jamii ya Abagusii.

### 3.2.2 Nidhamu

Mtoto alistahili kuwaheshimu watu wote katika jamii. Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika kumwelezea jinsi alivyostahili kudumisha heshima wakati wote. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate amasikani gochia ase abanto bonsi. Nigo aikaransete ase ekerogo korende ochia korora omonto omobwete emiaka, nigo atenena omokwania ase amaboko abere, naende oimoka bwango na komotigera ekerogo. Erio ere nigo agenda goikaransa inse ase obonyansi.* (Mtoto huyu anawaheshimu watu wote. Alikuwa amekalia kiti, kisha alipomwona mtu anayemzidi umri, alisimama kwa haraka na kumsalimu kwa mikono miwili na kumwomba akalie kiti hicho. Aameamua kwenda kuketi chini ya nyasi).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kuwa na nidhamu. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumweleza umuhimu wa kuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumwelimisha mtoto kuhusu mila na desturi zilizostahili kuzingatiwa na mtoto alipoendelea kuishi katika jamii ya Abagusii.

### 3.2.3 Upendo

Mojawapo ya vitu muhimu katika jamii ni kuwa na upendo. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimhimiza kuwapenda watu wote katika jamii ya

Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyewapenda watu wengine katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate obwanchani gochia ase abana bande. Nigo botambe anchete kobaika ang'e. Boigo, nigo anchete kogosoria nabarabwo, obaira mwabo baragera amo na obakonya ekeru babwate emechando.* (Mtoto huyu anawapenda watoto wengine. Kila wakati anakaa karibu nao. Pia, anapenda kucheza pamoja nao, anawapeleka nyumbani kwao wanakula pamoja na anawasaida wakati wanakumbwa na shida yoyote).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwelimisha mtoto huyo umuhimu wa kuwa na upendo katika jamii. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ilimwelekeza jinsi ya kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Aidha, lugha hiyo ilimfafanulia mtoto umuhimu wa kuwapenda watu wengine katika jamii ya Abagusii. mfano wa umuhimu huo ni wanajamii waliopendana walishirikiana katika kutatua shida na changamoto mbalimbali zilizowakumba katika jamii ya Abagusii.

### **3.3 Kuonya**

Kumwonya mtoto ni kumweleza kuhusu mambo mbalimbali alistahili kuzingatia katika maisha yake ili ajiepushe na shida zilizoweza kumkumba katika maisha yake. Mtoto aliyeonywa kisha akayapuuza aliyoambiwa alikumbana na shida kadhaa maishani mwake. Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika kumwonya mtoto kujiepusha kutenda

vitendo viovu katika jamii ya Abagusii kama vile kuwa mwizi, kutumia pombe na dawa za kulevya, kuwa jambazi na kuwatusi watu wengine.

### **3.3.1 Kumwonya mtoto asiibe**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwonya mtoto asiwe na tabia ya kuwaibia watu vitu vyao. Mfano ni katika lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa mwizi katika jamii ya Abagusii tazama 2.1.6 alionywa kwa kutumia lugha:

*Omwana oyo nekogwenerete gotiga embua yao yokobaibera abanto bande ebinto biabo, onye gokogendera gokora boigo, rituko erimo nigo orabwatwe maiso marore na gosambwa. Nabo gose orabwatwe nakoirwa egotini kogambiwa ekina, nagosibwa echera ase emiaka emenge.* (Mtoto huyu unastahili kujiepusha na tabia yako ya kuwaibia watu vitu vyao, ukiwa na mazoea ya kufanya hivyo, siku moja utashikwa hadharani na kuchomwa. Aidha, unaweza kutiwa mbaroni na kushtakiwa kortini, baada ya kesi kufungwa gerezani kwa miaka mingi).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa ni kumwonya mtoto huyo asiibe. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwonya mtoto asiibe vitu vya watu wengine.. Wanajamii walitumia lugha hiyo kumwonya mtoto aliyewaibia watu vitu vyao. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuwa na mazoea ya kuwaomba watu vitu vyao badala ya kuvichukua kwa siri.

### 3.3.2 Kumwonya mtoto asitumie pombe na dawa za kulevya

Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika kumwonya mtoto aliyezoea kunywa pombe au kutumia dawa za kulevya katika jamii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwonya asitumie pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii ni:

*Okonywa amarwa gose amariogo agotindia negento ekebe mono ase obogima bwao, amo nabanto baria momeneyete amo nabarabwo. Buna aye gwachorire konywa echang'a amo namariogo yogotindia, obogima bwao kwasarekire. Nigo kogokurera buna otige gochakera rero iga tiga konywa amarwa ande onsi. Boigo, otige konywa amariogo yogotindia ase obogima bwao. Gokwanga koigwera obosemia bwane buna omoibori oo, rirorio nkwenyora ore ase obokong'u obonene aseobogima bwao, buna koba namaote amange ase omobere oo amo namwaraire otanyare kogwenia buna enyamoreo. (Matumizi ya pombe au dawa za kulevya jambo baya katika maisha yako, pamoja na wale wote mnaishi nao. Vile umeamua kunywa pombe ya chang'aa na dawa za kulevya, maisha yako yameharibika. Ninakutahadharisha kuwa ujiepushe kwanzia leo kuacha kunywa aina yoyote ya pombe. Vilevile, usitumie dawa za kulevya katika maisha yako. Ukiyapuza mawaidha kutoka kwa mzazi wako, utakumbwa na shida nyingi maishani mwako, kama vile kuwa na majeraha mengi mwilini mwako na magonjwa yasiyo na tiba kama vile ukimwi).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwonya mtoto huyo asitumie pombe na dawa za kulevya. Mfano wa lugha hii

ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwonya mtoto asitumie pombe au dawa za kulevya katika maisha yake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto kuhusu madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii.

### **3.3.3 Kumwonya mtoto asiwe jambazi**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii pia ilitumika katika kumwonya mtoto asijiunge wala kushirikiana na magenge ya majambazi. Lugha hiyo ililenga hasa kumshauri mtoto huyo kuwa na tabia nzuri katika jamii na wala si kuwasumbua wanajamii kwa kuwapiga na kuwanyang'anya vitu vyao wakati wa usiku. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomtahadharisha asiwe jambazi ni:

*Omwana one nigo nkogosemia buna nekogwenerete orende tobaisa koba ekebago.*

*Omwana ore ekebago nigo akobwatana amo nebibago binde ase okobachanda*

*abanto chinsa chia botuko. Nigo bakobuna chinyomba babaita na kobaura abanto*

*abwo ebinto biabo. Tobaisa koganyerera abanto nakobaita chinsa chiamagoroba.*

*Onyorekane kogokora ayio, nigo oraimokerigwe egatambokerio ne eserekari.*

*Naboigo, koramanyekane buna aye nekebago ore, nigo oraitwe na gokwa.*

(Mwanangu ninakushauri kuwa unastahili kuwa makini usiwe jambazi. Mtoto aliye jambazi anajiunga na magenge ya majambazi kwa lengo la kuwasumbua watu wengine wakati wa usiku. Wanavunja nyumba za watu kisha wanawapiga wote waliomo na kuwanyang'anya vitu vyao. Usitubutu kuwangojea watu wakati wa jioni kwa lengo la kuwapiga na kuwanyang'anya vitu vyao. Ukipatikana unatakeleza hayo,

utachukuliwa hatua na serikali. Aidha, ukijulikana kuwa wewe ni jambazi utapigwa na watu wengine hadi kifo).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwonya mtoto asiwe jambazi. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwonya mtoto huyo asiwe jambazi. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumwonya mtoto huyo kujiepusha na kutenda vitendo viovu katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu yale yangempata iwapo aliamua kupuuza mawaidha hayo.

### **3.3.4 Kumwonya mtoto asiwatusi watoto wengine**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ilitumika katika kumwonya mtoto aliyezoea kuwatusi watu wengine tazama 2.1.8. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwonya asiwatusi watu wengine katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo tiga kona kobarama abanto bande. Renda mono ekiogokwana korwa monwa oo. Amang'ana onsi ogokwana, abe yokoagacha tari ayagotagora. Ekerokobarama abanto bande, nabo oranyore okoragereriwa ase obogima bwao. Naende, ogenderere nembua eyio, nabo morarwane noria kwarama. Naende, abanto bakomanya buna naye kware omochege nigo bagogoita ebiranya ebiroro. (Mtoto huyu jiepuche na tabia ya kuwatusi watu wengine. Chunga sana kile unachonena kutoka kinywani mwako. Maneno yote unayonena yanastahili yawe ya kujenga na wala si ya kubomoa. Unapowatusi watu wengine, unaweza kupokea laana katika*



maisha yako. Aidha, ukiendelea na tabia hiyo, mnaweza kupigana na uliyemtusi. Watu wakigundua kuwa wewe ndiwe mchokozi, watakucharaza viboko kadhaa).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumwonya mtoto asiwatusi watu wengine. Mfano wa lugha hii ulionyesha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumwonya mtoto asiwatusi watoto wengine. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto kuhusu yale yangempata iwapo alipuuza mawaidha hayo. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kuwasiliana na watu wengine bila kutumia matusi.

### **3.4 Kurekebisha tabia**

Mtoto wakati mwingine alizoea kutenda kinyume na alivyoyostahili kufanya katika jamii ya Abagusii. Hivyo basi, Abagusii walitumia lugha iliyowasilisha taswira yake ili kumrekebisha tabia yake. Wanajamii walitumia lugha hiyo kurekebisha tabia za watoto hasa waliotenda mambo yaliyosababisha mafarakano katika jamii. Mambo waliyofanya ni yale yaliyokuwa kinyume na maadili ya jamii ya Abagusii. Taswira ya mtoto aliyelengwa kurekebishwa tabia ni yule aliyekuwa na mazoea ya kutenda mambo kama vile uasherati, uzembe na ukosefu wa nidhamu.

### **3.4.1 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyefanya uasherati**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyefanya uasherati tazama 2.1.7 aliombwa kurekebisha tabia yake. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika kumrekebisha tabia mtoto aliyefanya uasherati katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one nagosabire otige goetanana aiga naria korigia abamura na koba amo nabarabwo. Tuguta are embua eyio embe nakoba omwana obwate embua engiya.*

(Mwanangu ninakuomba ukomeshe kuzurura hapa na pale ukiwatafuta wavulana na kufanya uasherati nao. Tupilia mbali tabia hiyo mbaya na kuwa msichana aliye na tabia nzuri).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kurekebisha tabia ya mtoto aliyeamua kufanya uasherati. Mfano wa lugha hii ulitumika kutoa maelezo kuhusu madhara ya kufanya uasherati katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuzingatia masomo yake kwanza kisha kuolewa au kuoja alipofuzu na kufikisha umri uliokubaliwa katika jamii ya Abagusii.

### **3.4.2 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyekuwa mzembe**

Aidha, mtoto aliyekuwa mzembe tazama 2.1.11 aliombwa kufanya bidii katika kazi zozote aliagizwa kufanya. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika kumrekebisha tabia mtoto aliyekuwa mzembe katika jamii ni:

*Omwana oyo nigo are omworo. Obworo obwo bwao bwagerire obwate emechando emenge ase obogima bwao. Tema buna oranyare gokora egasi ende yonsi nomokia. Korakore egasi ase omokia, rirorio aye nigo orasesenigwe ase obogima bwao naende amatuko are bosio nigo orache koba omotenenku.* (Mtoto huyu ni mzembe. Uzembe wako umekufanya wewe kuwa na shida nyingi katika maisha yako. Jaribu kadri ya uwezo wako kufanya kazi yoyote kwa bidii. Ukifanya kazi kwa bidii, utabarikiwa maishani mwako na kuwa tajiri siku za usoni).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kurekebisha tabia ya mtoto aliyekuwa mzembe katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu manufaa ya kufanya kazi kwa bidii. Mfano wa lugha hii ulitoa maelezo kuhusu manufaa ya kufanya kazi kwa bidii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri mtoto huyo kuhusu watu kadhaa waliofaulu maishani katika jamii ya Abagusii kwa kufanya kazi kwa bidii.

### **3.4.3 Kurekebisha tabia ya mtoto aliyekosa nidhamu**

Mtoto aliyekosa nidhamu katika maisha yake alishauriwa na wazazi wake kuwa na nidhamu. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika kumrekebisha tabia mtoto aliyekosa nidhamu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one tobwati masikani gochia ase abanto bande. Nigo agokwana nobotindi amang'ana yobosoku gochia ase abanto bonsi. Nagosabire otige embua eyio embe na koba namasikani gochia ase abanto bande.* (Mwanangu huna nidhamu kwa watu

wengine. Unazungumza kwa ukali maneno ya aibu mbele ya watu wote. Ninakuomba ujepushe na tabia hiyo mbaya na kuwa na nidhamu kwa watu wote).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kurekebisha tabia ya mtoto aliyekosa nidhamu. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kurekebisha tabia ya mtoto huyo kwa kumweleza kuhusu umuhimu wa kuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walimweleza mtoto huyo kuhusu matokeo ya kukosa kuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii.

### **3.5 Kuwasiliana**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika katika mawasiliano. Lugha hiyo ilitumika kupeleka na kupokea habari kutoka kwa wazazi, walezi wa watoto na watu wengine wazima katika jamii hadi kwa watoto. Lugha hiyo ilipitisha ujumbe kwa mtoto kuhusu mila na desturi za Abagusii ambazo zilistahili kuzingatiwa na watu wote. Aidha, lugha hiyo ilitumika kumwelezea mtoto kuhusu matukio muhimu katika jamii yaliyotokea miaka ya mapema kabla ya kuzaliwa kwake. Aidha, lugha hiyo ilitumika kuwasiliana kwa mtoto kuhusu majukumu aliyostahili kutekeleza katika jamii. Mtoto huyo pia aliweza kupokea habari kuhusu jinsi alivyostahili kujikinga kutokana na hatari yoyote iliyomkabili maishani mwake. Mawasiliano hayo ni muhimu kwa vile yalipitisha ujumbe muhimu kuhusu mila na desturi za Abagusii zilizohusina na unyago, harusi, kuzaliwa kwa mtoto na hata mazishi. Mawasiliano baina ya mtoto na wote waliohusika katika kumlea na kumtunza, yalimsaidia mtoto huyo kwa vile yalimweleza njia

aliyostahili kufuata ili afanikiwe maishani mwake. Mfano wa matumizi ya lugha hiyo yalidhihirika wazi katika mawasiliano yaliyolenga majukumu ya kufanya, maadili ya kuzingatia na vipawa vya mtoto katika jamii ya Abagusii.

### **3.5.1 Kuwasiliana kuhusu majukumu ya mtoto**

Kuna majukumu kadhaa yaliyotekelezwa na mtoto katika jamii ya Abagusii. Lugha iliyowasilisha taswira ilitumika kumpa mtoto maagizo mbalimbali na kazi tofautitofauti zilizostahili kutendwa na mtoto. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika katika kuwasiliana kuhusu majukumu ya mtoto katika jamii ya Abagusii kama vile kufanya kazi kwa bidii tazama 2.2.5 ni:

*Bwakire buya rero, bogoria ekebuyu oraminyoka roche ondetere amache ebibuyu bitano. Kogookora, obogorie obokombe ogende mogondo koburugera chibando. Omoerio, nigo okogenda ang'e na rooche bwatie amagena. Korakore ayio onsi nagochikire gokora rero, rirorio ninkoe endagera orie naende ningoakane chisiringi emerongo etano. (Kumepambazuka vyema siku ya leo, beba mtungi kisha kimbua mtoni ulete maji safari tano. Ukimaliza, beba jembe uelekee shambani kupalilia maindi. Mwisho, utaenda kupasua mawe kule karibu na mto. Ukifanya hayo yote nimekuagiza kufanya leo, nitakupa chakula ule na malipo ya shilingi hamsini).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kuwasiliana kwa mtoto kuhusu majukumu mbalimbali aliyostahili kufanya katika

jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kuwasiliana kwa mtoto kuhusu umuhimu wa kufanya kazi mbalimbali kwa bidii katika jamii ya Abagusii.

### **3.5.2 Kuwasiliana kuhusu maadili**

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto, ilitumika katika kuwasiliana kwa mtoto kuhusu maadili aliyostahili kuzingatia katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto msichana aliyezingatia maadili tazama 2.2.3 katika jamii ya Abagusii ni:

*Amasikani negento kiengecho ase obogima. Omwana one, nagosabire obe namasikani gochia ase abanto bande. Ekeru okobakwania abanto abanene, bakwanie namaboko abere, kobaorokia buna nobasigete. Naende, kerabe nigo oinkaransete ase ekerogo na mbareo bakobwete emiaka bateneine, tenena na komoboria omonoto omonene ainkaranse ase ekerogo ekio. Aye nabo oratenene gose oinkaranse inse ase obonyansi. Naende boigo, nigo ogwenerete koiraneria amaborio kwaborigwe nabanto bande ase enchera yobwororo. (Nidhamu ni kitu muhimu katika maisha. Mwanangu ninakuomba uwe na nidhamu kwa watu wengine. Ukiwasalimia wakubwa wako, wasalimie kwa mikono miwili, kuonyesha kuwa unawaheshimu. Pia, iwapo umekalia kiti na kuna wale wanaokuzidi umri, simama na kumwomba mtu mzima kukalia kiti hicho. Unaweza kusimama au kuketi chini nyasi. Vilevile, ukiulizwa swali lolote na mtu yeyote, unastahili kumjibu kwa njia ya upole).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa kumweleza mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili katika jamii ya

Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kuwasiliana kuhusu yaliyotokea kwa mtoto huyo alipokosa kuzingatia maadili katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumfundisha mtoto huyo mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu nidhamu katika jamii ya Abagusii

### **3.5.3 Kuwasiliana kuhusu vipawa vya mtoto**

Utafiti huu vilevile umebainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto vilevile ilitumika katika kumwelimisha mtoto kuhusu vipawa vyake katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomwelimisha kuhusu umuhimu wa kuwa na kipawa maalumu tazama 2.2.1 katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana nigo tagete komoegeria buna nabwate ekeegwa kiabene. Ebinto bikoorkia nore nekeegwa kiabene nabio ebi: ogotegerera nakoigwa bwango, nabo okobanga bwango ebinto, nigo okonyora chisabu chionsi, okomanya egento kende gionsi ase kere, okobakonya abana bande gosoma gose goaka chisabu chibasinyire boigo nabo ogokora emeremo yao buya otaganetia bokonyi bonde korwa ase monto onde bwensi.*

(Ninamwelimisha mtoto huyu kuwa ana kipawa maalumu. Dalili zinazoonyesha kuwa una kipaji maalumu ni: unasikiliza na kuelewa mambo haraka, unaweza kupanga vitu haraka, unapata hasabu zote, uajua mahali kila kitu kipo, unawasaidia watoto wengine kusoma na kufanya hasabu ngumu na unafanya kazi yako vizuri bila msaada wowote kutoka kwa watu wengine).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii

ilikuwa kuwasiliana kwa mtoto kuhusu vipawa. Wanajamii walitumia lugha hiyo vilevile katika kumfahamisha mtoto huyo kuhusu vipawa kadhaa vya watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Pia, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu manufaa ya vipawa mbalimbali katika jamii ya Abagusii.

### **3.6 Kutia motisha**

Dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ni kuwa ilimtia motisha ya kufanya shughuli zake kwa bidii. Lugha hiyo ilimhimiza mtoto afanye kazi au shughuli zozote kwa bidii katika jamii ya Abagusii. Wazazi na walezi walitumia lugha ya kumtia mtoto motisha walipogundua kuwa alikuwa na udhaifu fulani wa kutekeleza kazi alizoagizwa kufanya. Aidha, lugha hiyo ilitumika katika kumhimiza mtoto kubadilisha tabia yake. Lugha hiyo vilevile ilitumika katika kumhimiza mtoto aliyepitia changamoto mbalimbali za maisha kama vile magonjwa na mateso katika jamii. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyomtia mtoto motisha ilitumika kumwezesha kufanya kazi kwa bidii, kuwa na tabia nzuri na mgonjwa kupokea nafuu.

#### **3.6.1 Kumtia mtoto motisha ya kufanya kazi kwa bidii**

Mtoto mzembe aliyezoea kula na kukaa bila kufanya jambo lolote, alihimizwa kufanya kazi kwa bidii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyotumika kumtia mtoto aliyekuwa mzembe motisha tazama 2.1.11 ya kufanya kazi kwa bidii katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one aye nigo ore omworo. Nigo aye omanyete buya koragera kwamanya goikaransa otari gokora kende gionsi. Nagosoroire, otige koba omwana omworo na*



*gokora emeremo ende yonsi oratebigwe gokora nomokia. Naende, nogwenerete komanya buya buna, omokia oo noro oragokonye ase amatuko are bosio.* (Mwanangu wewe ni mzembe. Wafahamu vyema kula kisha unaketi bila kufanya kazi yoyote. Ninakusihi, ukome kuwa mtoto mzembe na kufanya kazi yoyote utaambiwa kufanya kwa bidii. Aidha, unastahili kufahamu vyema kuwa bidii zako ndizi zitakuwezesha kuimarika siku zijazo.

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumtia mtoto huyo mzembe motisha ya kufanya kazi kwa bidii. Mtoto huyo baada ya kupokea motisha hiyo, aliimarika katika maisha yake na kuinua mapato ya familia na jamii yake.

### **3.6.2 Kuntia mtoto motisha ya kuwa na tabia nzuri**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyekuwa na tabia mbaya alihimizwa kuwa na tabia nzuri katika jamii ya Abagusii. Wazazi wake walimtia motisha ya kujiepusha kutenda vitendo viovu kama vile kuwatusi au kupigana na watu wengine, badala yake mtoto huyo alihimizwa kuwa na tabia nzuri katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ilitumika kumtia mtoto huyo motisha ya kuwaheshimu watu wengine, kuwapenda watu wengine na mgonjwa kupata nafuu.

### **3.6.2.1 Kuntia mtoto motisha ya kuwaheshimu watu wengine**

Mfano wa matumizi ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilimhimiza mtoto aliyewatusi watu wengine tazama 2.1.8 kuacha tabia hiyo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one, nigo bwanchete gochegia na korama abana bande amang'ana are amabe naende yobosoku. Nagosoroire motangi one, otige korwa rero iga kobarama abana bande na koba omwana omuya.* (Mwanangu, unependa kuwatusi watoto wengine kwa maneno mabaya tena ya aibu. Ninakusihhi kifungua mimba wangu, kutoka leo ukome kabisa tabia ya kuwatusi watoto wengine).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ilitumika katika kumhimiza mtoto kuacha tabia ya kuwatusi watoto wengine. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumshawishi mtoto huyo kuwa na tabia nzuri. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kutumia lugha nzuri na iliyokubalika katika jamii ya Abagusii.

### **3.6.2.2 Kuntia mtoto motisha ya kuwapenda watu wengine**

Mtoto aliyezoea kupigana na watoto wengine tazama 2.1.9, alihimizwa na wazazi wake kuacha tabia hiyo. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyepigana na watoto wengine iliyotumika kuntia mtoto huyo motisha ya kukoma kufanya hivyo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one, nomanyete buya buna kwanarire kobachegia na kobarwania abana bande. Nagosoroire otige embua eyio embe. Gokogenderera gokora boigo, nabo ngotiga gochia gokogorera ebikoroto.* (Mwanangu, unaelewa vyema kuwa umezoea kuwachokoza na kupigana na watoto wengine. Ninakusihi uache tabia hiyo mbaya. Ukiendelea kufanya hayo, sitakununulia viatu).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumhimiza mtoto huyo aliyezoea kupigana na watoto wengine kuacha tabia hiyo. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshawishi mtoto huyo aweze kubadilisha tabia yake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza kuhusu umuhimu wa kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

### **3.6.3 Kuntia mtoto mgonjwa motisha ya kupata nafuu**

Mtoto aliyekuwa mgonjwa tazama 2.1.1 aliyekosa hamu ya chakula aliyelia kila wakati kutokana na maumivu, alihimizwa kula chakula na kuvumilia maumivu hayo. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetiwa motisha kwa vile alikuwa mgonjwa katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one nyore kore omorwaire, naende tobwati rang'o ende yonsi yokoria endagera, gaki nabo okwebetereria koria endagera nkeigo. Naende, gaki nagosoroire nyore gokoromwa mono ase enda yao, remereria naende takorera nogwene bwango iga.* (Mwanangu hata kama wewe ni mgonjwa, tena huna hamu ya

kula chakula chochote, nakusihi ujilazimishe kula hata kidogo, tena ninakusihi hata kama unaumwa na tumbo lako, vumilia na usilie utapona hivi karibuni).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumtia mtoto aliyekuwa mgonjwa motisha ya kuwa hai. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumshawishi mtoto huyo kuvumilia maumivu yaliyokuwa yakimsumbua. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumpa mtoto huyo tumaini la kupona siku za mbeleni.

### **3.7 Kusifu**

Kusifu vilevile ni dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Kumsifu mtoto ni kutumia lugha iliyoeleza yale mazuri yote aliyoyatenda katika jamii. Kulikuwa na mazoea ya kumsifu mtoto pale alipofanya mambo mema. Hali hii ya kumsifu mtoto ilikuwa ishara ya kumpa moyo ili aweze kutenda mambo mema zaidi. Baadhi ya watoto waliosifiwa waliweza kujigamba kwa watoto wengine eti wao ni bora na hata kuhisi kuwa wao walipendwa ukiwalinganisha na watoto wengine katika familia.

Utafiti huu ulibainisha mifano kadhaa ya matumizi ya lugha iliyomsifu mtoto baada ya kutenda kitendo cha kufurahisha wanajamii. Mtoto huyo alimiminiwa sifa tele na watu wote katika jamii kwa vile yeye alitenda mambo ya kufurahisha na yaliyokubalika na wanajamii wote. Mfano wa lugha hiyo ambayo ilidhihirika wazi katika utafiti huu ni:

### **3.7.1 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu**

Watoto waliokuwa na vipaji maalumu katika jamii ya Abagusii walisifiwa. Baadhi ya vipawa hivyo ni; kukimbia, kuimba, kucheza mpira, kuruka, kuchora, kusoma, kughani mashairi, kuandika kwa hati nzuri, kupika vyakula na kufanya kazi kama vile kulima, kufyeka, kufua nguo na kazi nyinginezo.

#### **3.7.1.1 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuimba**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuimba alimiminiwa sifa tele. Alisifiwa kwa vile aliimba nyimbo kwa njia ya kupendeza. Aidha, mtoto huyo alipata fursa ya kualikwa na kuwatumbuiza watu katika sherehe mbalimbali kama vile; siasa, arusi, matanga, kupeana tuzo na ibada. Mfano wa lugha ya sifa iliyotumika kuwasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuimba ni:

*Omwana oyo nigo mwanchete, ere nigo abwate ekegwa kiogotera. Nigo agotera ase eriogi riororo, rigiya naende riokogokia abanto bonsi.* (Mtoto huyu ninampenda, kwa sababu yeye ana kipaji cha kuimba. Anaimba kwa sauti nyororo, nzuri ya kuwafurahisha watu wote).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuimba. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumsifu mtoto huyo ili kuboresha kipawa chake cha kuimba nyimbo. Aidha, wanajamii

walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kukuza kipawa chake kuimba nyimbo.

### **3.7.1.2 Kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuchora**

Mtoto aliyekuwa na kipawa maalumu tazama 2.2.1 kama vile kuchora alisifiwa kwa vile alikuwa na uwezo wa kuchora vitu tofautitofauti vilivyopatikana katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomsifu kwa vile alikuwa na kipawa maalumu cha kuchora katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omuya, gekogera ere nigo abwate ekegwa kiabene kiogochora ebinto aoao. Nabo agochora buya ebinto aoao buna bikororekana, buya naende ase enchera yokogokia.* (Mtoto huyu ni mwema kwa vile ana kipaji maalumu cha kuchora aina mbalimbali za vitu. Ana uwezo wa kuchora vitu mbalimbali jinsi vilivyo, vizuri na kwa njia ya kupendeza).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumsifu mtoto aliyekuwa na kipawa cha kuchora. Wanajamii walimsifu mtoto huyo kama njia ya kumwezesha kuimarisha kipawa chake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza kuhusu umuhimu wa kukuza kipawa chake cha kuchora.

### **3.7.2 Kumsifu mtoto aliyetenda mema**

Aidha, mtoto aliyetenda mema katika jamii naye alisifiwa. Kuna mambo kadua mema yaliyotendwa na watoto katika jamii ya Abagusii. Baadhi ya mambo hayo ni; kufaulu katika mitihani, kuwasaidia watu wengine kubeba mizigo, kuwashughulikia wagonjwa kwa kuwapa misaada waliyohitaji. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ni:

#### **3.7.2.1 Kumsifu mtoto aliyefaulu katika mitihani**

Mtoto aliyefaulu katika mitihani yake na kuibuka wa kwanza alisifiwa katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomsifu mtoto aliyefaulu katika mitihani yake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo okorire buya ase amatemwa eya onsi. Nigo abatang'anerera abana bonsi ase esukuru yaye. Nigo aeta amatemwa aye ase engecho are omwana omoigweri, omwororo, ogosoma nomokia. Naende, nigo anchete kobaika ang'e abarimu baye erio bamokonye ase ataigweti buya. (Mtoto huyu amefanya vizuri katika mitihani yake yote. Ametangulia wanafunzi wote katika shule yake. Amepita mitihani yake kwa vile yeye ni mtoto mtiifu, mpole, anasoma kwa bidii. Aidha, anawakaribia walimu wake ili wamsaidie kufahamu vizuri sehemu zilizo ngumu).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumsifu mtoto aliyefaulu katika mitihani yake. Azma ya wanajamii kutumia lugha hiyo ni mtoto kumpa motisha ili aweze kuendelea kufanya vyema katika masomo yake. Aidha,

wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumashauri mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kutia bidii na kuibuka wa kwanza katika darasa lake.

### **3.7.2.2 Kumsifu mtoto aliyewasaidia watu**

Watoto waliokuwa na mazoea ya kutoa msaada kwa watu wengine katika jamii ya Abagusii walisifiwa kwa kufanya hivyo kama njia ya kuwapa motisha watoto wengine kutoa msaada pale ulihitajika. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyesifiwa kwa kuwasaidia watu wengine kubeba mizigo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anchete gokonya abanto bande. Nigo akobabogoreria ebinto biabo bosa atari kobasaba besa ende yonsi. Naende, ere nigo abwate chinguru yagera akobogoria ebinto ebirito.* (Mtoto huyu anapenda kuwasaidia watu wengine. Anawabebea mizigo yao bure bila kuwaomba pesa zozote. Aidha, yeye ana nguvu za kumwezesha kubeba mizigo mizito).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumsifu mtoto aliyewasaidia watu kubeba mizigo. Wanajamii walitumia lugha ya kumsifu mtoto kwa lengo la kumpa moyo wa kuendelea kuwasaidia watu wengine bila kuitisha malipo yoyote. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri mtoto ajitolee kuwasaidia watu wengine katika jamii kwa vile angebarikiwa kwa kufanya hivyo.



### 3.8 Kufariji

Dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni kufariji. Kumfariji mtoto ni kumliwaza hasa alipokumbwa na jambo lolote baya katika jamii. Lugha ya kufariji ilitoa faraja kwa mtoto aliyekuwa anapitia changamoto fulani katika maisha yake kama vile aliteswa, mgonjwa au kifo cha mtu wa karibu.

#### 3.8.1 Kumfariji mtoto aliyeteswa

Baadhi ya watoto waliteswa katika jamii ya Abagusii. Kuna sababu kadhaa zilizosababisha watoto hao kusumbuliwa na wazazi au walezi wao katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefarijiwa kwa vile alitelekezwa na wazazi wake tazama 2.1.14 aliyeishi kwa babu yake aliyemtesa katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abaibori baye bamotiga aiga bakagenda komenya Bosongo. Bono iga nyore omenyete na sokoro yaye nigo amochandete. Nigo kera rituko akomotebia akore chigasi aoao buna; gochia roche, korema na korisia chiombe korwa mambia goika magoroba. Sokoro yaye tari komoa kende okoria bono nigo are omogoyu. Nagosabire ogenderere koremereria emechando eyio yonsi, nabo mosuko abaibori bao barache bakoire ochie komenya amo nabarabwo. (Mtoto huyu ametelekezwa na wazazi wake walioenda kuishi mji wa Kisii. Hivi sasa mtoto huyu anaishi na babu yake anayemtesa. Kila siku anamwambia afanye kazi mbalimbali kama vile; kwenda mtoni, kulima na kupeleka ng'ombe malishoni kutoka asubuhi hadi jioni. Babu yake hampi chakula chochote hivyo basi yeye ni mnyonge. Ninakuomba uendelee kuvumilia shida hizo zote, siku moja wazazi wako watajitokeza wakupeleke uende kuishi nao).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ulikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ilitumika katika kumfariji mtoto aliyeteswa na wazazi wake. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumwomba mtoto huyo aendelee kuvumilia maisha, japo wazazi wake walimtesa. Pia, walitumia lugha hiyo kumweleza mtoto huyo njia mbalimbali zilizostahili kuzingatiwa ili aweze kujinasua kutoka kwa shida hizo.

### **3.8.2 Kumfariji mtoto aliyekuwa mgonjwa**

Baadhi ya watoto walishambuliwa na magonjwa kadhaa katika jamii ya Abagusii. Waliweza kuugua kwa muda mrefu kwa vile wengine wao walikosa kupokea matibabu ya haraka kutoka zahanati au hospitali zilizokuwa karibu na makwao. Magonjwa hayo yaliwasumbua watoto pamoja na kuwafanya wazazi au walezi wao kusumbuka wakiwashughulikia wakati wa mchana na usiku. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyegua ugonjwa wa ukimwi tazama 2.1.1 alifarijiwa kwa lugha:

*Omwana oyo kwarwarire ase engaki etambe. Remereria ase obororo ogoetera. Namanyire nigo ogwatigwa omotwe, ogosaa na koroka. Ebio bionsi tibikogosa egekogera oise konywa amariogo kwaerwe na abanyagitari, bwango iga kogwena ore ogende gotiena amo nabana bande. (Mtoto huyu ameugua kwa muda mrefu. Vumilia kwa makali unayopitia. Naelewa kuwa unaumwa kichwa, unahara na kutapika. Hayo yote yasikutishe kwa vile ukitumia dawa ulizopewa na daktari, utapona hivi karibuni uende kucheza na watoto wengine).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe katika mawasiliano huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumfafariji mtoto aliyekuwa mgonjwa. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumwomba mtoto huyo kuvumilia maumivu ya ugonjwa uliokuwa ukimsumbua. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumpa mtoto huyo matumaini ya kuwa hai hata kama alikuwa na maumivu kutokana na maradhi yaliyomshambulia.

### **3.8.3 Kumfariji mtoto aliyekuwa yatima**

Baadhi ya watoto walikuwa mayatima katika jamii ya Abagusii. Vifo vya wazazi vilivyotokea katika baadhi ya familia vilisababisha watoto wengine kuwa mayatima. Watoto hao baada ya kuwa mayatima walitarajia kupewa msaada kutoka kwa watu wengine katika jamii ya Abagusii. Mtoto aliyefiwa na wazazi wake katika jamii ya Abagusii na kusalia yatima tazama 2.1.3 alifarijiwa kwa mfano wa lugha:

*Nagosoroire nyore abaibori bao bonsi basirire gwatigaire entankana, remereria amakweri ayio. Tobaisa kona gweitia buna naki toramenye, nki torarie gose naki toreboyie. Nyasae narete amalaika aye abarende kera rituko nakobaa bionsi moganetie ase obogima obo. Komoraba na bokong'u bonde bwensi, nimbe ang'e nainwe kobasira ase konyara. (Ninakusihhi hata kama wazazi wako wote wameaga dunia na umebaki yatima, vumilia vifo hivyo. Usijisumbue kuwa tutaishije, tutakula nini au tutavaa vipi. Mungu ataleta malaika zake wawalinde kila siku na kuwatimizia haja zenu katika maisha haya. Mkikumbwa na shida yoyote, nitakuwa karibu nanyi kuwasaidia kadri ya uwezo wangu).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumfariji mtoto aliyefiwa na wazazi wake. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumfariji yatima huyo na kumwomba aweze kuwa mvumilivu katika maisha ingawa wazazi wake wote walikuwa wameaga dunia. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumweleza yatima huyo jinsi ya kukabiliana na maisha bila wazazi.

#### **3.8.4 Kumfariji mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu**

Kuna baadhi ya familia zilizoishi katika maisha ya umaskini. Familia hizo zilikosa uwezo wa kupata mahitaji muhimu ya kila siku. Ilibidi watoto kutoka familia hizo waajiriwe kufanya kazi ngumu kwa malipo duni katika jamii ya Abagusii tazama 2.1.13. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefarijiwa kwa kuajiriwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one nagosoroire oremererie ase egasi enkongu ogokora na koegwa chibesa chinke.* (Mwanangu nakusihi uvumilie kwa kazi ngumu unayoifanya na kupokea malipo duni).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu za mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumfariji mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu kwa malipo duni. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo jinsi ya kuwa mvumilivu ingawa

alikuwa akisumbuliwa. Wanajamii vilevile, walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto kuhusu mambo aliyostahili kuzingatia ili kusuluhisha shida zilizokuwa zikimwaandama katika maisha yake.

### **3.8.5 Kumfariji mtoto aliyefiwa**

Wakati mwingine baadhi ya watoto walipokea habari za kuhuzunisha katika jamii ya Abagusii. Ilibidi wanajamii kuwatembelea watoto hao na kuwafariji. Mfano wa lugha iliyotumika kumfariji mtoto aliyepokea habari kuwa wazazi wake pamoja ndugu zake waliaga dunia walipokuwa wakisafiri kutoka mji wa Kisii wakielekea mji wa Keroka katika jamii ya Abagusii ni:

*Nyore amang'ana atoikeire buna abaibori bo omwana oyo amo nabana bamwabo banyorire omobasokano bwebara na bonsi bakure, nigo tokogosemia otige korera kera chingaki, twagosoroire oremereia amakweri ayio. Nigo torasirane ase okoenekia buna gwakaneirwe efisi na kwanyorire ebinto binde bionsi oganetie kera rituko. Naende, nigo togosaba Nyasae agosesenie ase amatuko agocha. (Japo tumepokea habari kuwa wazazi wa mtoto huyu pamoja na ndugu zake wamehusika katika ajali ya barabara na wote wameaga dunia, tunakushauri kuwa usilie kila wakati, tunakusihii uvumilie maafa hayo. Tutashirikiana katika kuhakikisha kuwa umelipiwa karo ya shule na umepokea mahitaji yako ya kila siku. Aidha, tunamwomba Mungu akubariki siku za usoni).*

Mhimili wa tano wa Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbea huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii

ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumfariji mtoto aliyehuzunika katika maisha. Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyefarijiwa ni yule aliyepokea habari za kuhuzunisha kuwa wazazi wake pamoja na ndugu zake walihusika katika ajali ya barabarani na wakaaga dunia. Hali hii ya kumfariji mtoto huyo ilimsaidia kukabiliana na hali ngumu ya maisha siku za usoni. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumweleza mtoto huyo jinsi ya kuishi japo wazazi wake na ndugu zake waliaga dunia.

### **3.9 Kulinganisha**

Dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ni kuwa ilitumika katika kulinganisha watoto katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ilitumika kulinganisha pale ambapo kulikuwa na hitaji la kuweka bayana sifa za watoto wawili au zaidi ili kuona kama walilingana. Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyelinganishwa na mwingine ni yule aliyekuwa na; tabia nzuri na tabia mbaya, alifanya bidii na mzembe, afya na mgonjwa, aliyeishi mazingira ya utajiri na mazingira ya umaskini.

#### **3.9.1 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia tabia zao**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kuwalinganisha taswira ya mtoto aliyekuwa na tabia nzuri na yule yule aliyekuwa na tabia mbaya. Mfano wa lugha iliyowalinganisha watoto hao katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omuya gekogera ere nigo are omwororo, agokora emermo yaye buya na abwate amasikani gochia ase abanto bande. Tokomobwekania nomwana obwate chimbua chimbe buna oboibi, obokebago, okorama na kobarwania*

*abantu bande.* (Mtoto huyu ni mzuri kwa vile yeye ni mpole, anafanya kazi yake vizuri na ana nidhamu kwa watu wengine. Huwezi kumlinganisha na mtoto aliye na tabia mbaya kama vile wizi, ujambazi, kutusi na kupigana na watu).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ni ilitumika katika kulinganisha. Mfano ni kulinganisha mtoto aliyekuwa na tabia nzuri na mtoto aliyekuwa na tabia mbaya. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kuwalinganisha watoto hao kwa lengo la kuwaeleza kuhusu umuhimu wa kufanya uamuzi ulio bora katika maisha yao.

### **3.9.2 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia bidii zao**

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia bidii zao walipofanya shughuli tofautitofauti wakati walikuwa shuleni au makwao. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomlinganisha na watoto wengine kwa kuzingatia bidii zao katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo agokora buya ase amasomo aye asengecho abwate omokia ase ogosoma kwaye. Tokomobwekania omwana oria ogokora bobo ase amatemwa aye egekogera ere nigo are omworo ase ogosoma kwaye.* (Mtoto huyu anafanya vyema katika masomo yake kwa vile anafanya bidii katika kusoma kwake. Huwezi kumlinganisha na mtoto yule anayefanya vibaya katika mitihani yake kwa vile yeye ni mzembe katika kusoma kwake).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumlinganisha mtoto aliyefanya bidii na mtoto aliyekuwa mzembe katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo ya kuwalinganisha watoto hao kwa lengo la kuwaeleza kuhusu jinsi walistahili kufanya uamuzi mwema katika maisha yao.

### **3.9.3 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia afya zao**

Utafiti huu pia ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kulinganisha mtoto aliyekuwa mgonjwa tazama 2.1.1 na mtoto aliyekuwa na afya tazama 2.2.4. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomlinganisha na watoto wengine kwa kuzingatia afya zao katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana nigo are omorwaire. Nigo areete, tari koria ndagera ende yonsi, agwatiwa omotwe, agosaa na koroka. Tokomobwekani omwana oyo otabwati borwaire bonde bwonsi egekogera nigo abwate. Nigo ere abwate omosasoko chingaki chionsi egekogera akoegwa ebinto bionsi aganetie.* (Mtoto huyu ni mgonjwa. Amekonda, hali chakula chochote, anaumwa kichwa, anahara na kutapika. Huwezi kumlinganisha na mtoto yule aliye na afya. Anachangamka wakati wote kwa vile anatimiziwa haja zake zote).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu za mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika



kumlinganisha mtoto aliyekuwa na afya na mtoto aliyekuwa mgonjwa katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo ya kuwalinganisha watoto hao, kwa lengo la kuwaeleza kuhusu mabadiliko ya afya ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

#### **3.9.4 Kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia mazingira waliyoishi**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii vilevile ilitumika katika kuwalinganisha watoto kwa kuzingatia mazingira waliyoishi. Mfano wa lugha iliyolinganisha taswira ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini tazama 2.1.4 na yule aliyeishi katika mazingira ya utajiri tazama 2.2.8 katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo amenyete ase obotaka. Tibabwati endagera ende bakoria, bakweboyia chianga amachanchabe na bamenyete enyomba bagotwerwa. Tokomobwekani omwana omenyeta ase obotenenku. Barabwo nigo babwate endagera enyinge bakoria, chianga chingiya bakobeka na enyomba engiya bamenyete.* (Mtoto huyu anaishi katika mazingira ya umaskini. Hawana chakula chochote wanaweza kula, wanavalia nguo za matambara na wanaishi katika nyumba wananyeshewa. Huwezi kumlinganisha na mtoto anayeishi katika mazingira ya utajiri. Wao wana chakula kingi cha kutosha, wanavalia nguo za kupendeza na wanaishi katika nyumba nzuri).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumlinganisha mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini na mtoto aliyeishi katika

mazingira ya utajiri. Wanajamii walitumia lugha hiyo kuwaliwalinganisha watoto hao kwa lengo la kuwaeleza kuhusu jinsi wanavyoishi kwa shida au kubarikiwa katika maisha yao katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto kuhusu umuhimu wa kupendana, kushirikiana na kusaidiana katika maisha ingawa waliishi katika mazingira tofauti.

### **3.10 Kushauri**

Kushauri pia ni dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Kumshauri mtoto ni kumpa maoni au nasaha kuhusu jambo fulani katika maisha yake. Mfano wa lugha iliyomshauri mtoto katika jamii ya Abagusii ilijitokeza wazi katika lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na nidhamu tazama 2.2.3 na mtoto aliyetia bidii katika masomo yake shuleni tazama 2.2.5.

#### **3.10.1 Kumshauri mtoto kuwa na nidhamu**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha ya kushauri ilitumika kwa mtoto aliyekuwa na nidhamu. Mtoto huyo alishauriwa kuendelea kuwa na nidhamu katika maisha yake kwa watu wote katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyotumika kumshauri mtoto aliyekuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one nagosabeire amaya naende nagosoroire buna ogenderere koba nechimbua chingiya kera engaki gochia ase abanto bonsi.* (Mwanangu nakuombea mema tena nakusihi kuwa uendeleo kuwa na nidhamu kila wakati kwa watu wote).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumshauri mtoto aliyekuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri huyo aendelee kuwa na nidhamu katika maisha yake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri kuhusu umuhimu wa kuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii.

### **3.10.2 Kumshauri mtoto kutia bidii katika masomo**

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa lugha ya kushauri ilitumika kwa mtoto aliyefanya vyema katika masomo yake. Mtoto huyo alishauriwa kutia bidii katika masomo yake ili aweze kufaulu katika mitihani yake. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomshauri kutia bidii katika masomo yake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one nagosoroire ogenderere gokora omokia ase amasomo ao. Boigo, genderera konyora amagisi aigoro ase amatemwa ao. Tobaisa kweba koba oyobweritang'ani ase ekerasi kiao.* (Mwanangu nakusihi uendelee kufanya bidii katika masomo yako. Pia, endelea kuzoa alama za juu katika mitihani yako. Usisahau kuwa wa kwanza darasani mwako).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ni ilitumika katika kumshauri mtoto aliyefanya vyema katika mitihani yake. Wanajamii walitumia lugha hiyo katika

kumshauri mtoto huyo aendelee kufanya vizuri katika mitihani yake na kuibuka wa kwanza katika darasa lake. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kutia bidii katika masomo yake kule shuleni.

### **3.11 Kukemea**

Kumkemea vilevile ni dhima nyingine ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Kukemea mtoto ni kumsema kwa kutumia lugha ya ukali. Wazazi na wote waliohusika katika kumlea mtoto wakati mwingine walilazimika kutumia lugha iliyomkaripia mtoto wakati alijihusisha na vitendo vibaya katika jamii. Mtoto aliweza kukemewa wakati alitenda jambo ambalo lilisababisha kero, chukizo au fedheha kwa watu wengine katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha ya kukemea ilitumika kwa mtoto; aliyetumia pombe na dawa za kulevya, aliyekuwa mwizi, aliyefanya uasherati, aliyewatusi watu wengine, aliyepigana na watoto wengine, aliyekuwa mzembe na aliyeoa au kuolewa.

#### **3.11.1 Kumkemea mtoto aliyekuwa mzembe**

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikuwa wazembe tazama 2.1.11. Mfano wa lugha iliyomkemea mtoto kwa vile alikuwa mzembe katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one, tiga koba omworo ekeru okorema mogondo. Boigo, tiga koba omworo ekeru ogokora emeremo ende yonsi ogotebigwa okore buna; okorabi obonyansi, okorisia chiombe, kogenda roche kwoyia amache na korosia endagera. (Mwanangu wacha kuwa mzembe wakati unalima shambani. Aidha, wacha kuwa mzembe wakati*

umeambiwa kufanya kazi yoyote kama vile; kufyeka nyasi, kupeleka ng'ombe malishoni, kwenda mtoni kuteka maji na kupika chakula).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto aliyekuwa mzembe katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ilitumika kumkemea mtoto huyo kama njia ya kumwonyesha kuwa uzembe ulistahili kutupiliwa mbali. Mtoto huyo alihimizwa na wazazi wake kufanya bidii katika kazi yoyote aliyoagizwa kufanya. Pia, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumweleza mtoto huyo kuhusu hasara ya kuwa mzembe katika jamii ya Abagusii.

### **3.11.2 Kumkemea mtoto aliyekuwa mwizi**

Aidha, baadhi ya watoto waliwaibia watu vitu vyao tazama 2.1.6. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomkemea kwa vile alikuwa mwizi katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one tiga gochanda, aye nigo ore nyamoibi simbiri. Nigo onarete kobaibera abanto bande ebinto biabo. Tiga kegima embua eyi. Korange obosemia bwane nakogenderera koba omoibi, ngoitwa gose ngonsambwa ore nabanto bande. Naende, nabo baragosoere ase ekegambero ekina gekoera osibwe echera emiaka emenge.*

(Mwanangu wacha kunisumbua, wewe ni mwizi hodari. Unazoea kuwaibia watu vitu vyao. Acha kabisa tabia hiyo. Ukiyapuuza mawaidha yangu na kuendelea kuwa

mwizi, utapigwa au kuchomwa na watu wengine. Pia, wanaweza kukushtaki mahakamani na baada ya kesi utahukumiwa kwenda kukaa gerezeni miaka mingi).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto aliyekuwa mwizi katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ilimkemea mtoto huyo kwa lengo la kumfanya aelewe kuwa tabia hiyo ya kuwaibia watu vitu vyao iliwakasirisha wanajamii wote. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumshauri mtoto huyo umuhimu wa kuwaomba watu vitu vyao badala ya kuwaibia.

### **3.11.3 Kumkemea mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya**

Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walitumia pombe na dawa za kulevya tazama 2.1.5. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomkemea kwa vile alitumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one namanyire embua yao nembe. Tiga, naende nkoirora kogotobia tiga konywa amarwa na amariogo yogotindia ase obogima bwao. Rigereria buna aye kwabeire risiesie, tori gwesibia omobere na kobeka chianga chindabu, enyomba okorara nigo ebwate eubi enyinge. Bwango iga nigo gwachaka kona kwegambia aye, bweka, kwabeire buna ebarimo.* (Mwanangu nimegundua kuwa tabia tabia yako ni mbaya. Acha, tena ninarudia kukuambia kuwa acha kutumia pombe na dawa za kulevya katika maisha yako. Hebu tazama jinsi umekuwa mtu bure, huogi wala kuvalia mavazi safi, chumba chako cha kulala kina uchafu mwingi. Hivi karibuni

umeanza kuzungumuza mambo mengi ukiwa peke yako, umekuwa kama mwendawazimu).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto aliyetumia pombe au dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumkosoa mtoto huyo na kumwonyesha kuwa alifanya kitendo ambacho kiliwachukiza wanajamii na alistahili kurekebisha tabia hiyo.

#### **3.11.4 Kumkemea mtoto aliyewatusi watoto wengine**

Baadhi ya watoto walikuwa na tabia ya kuwatusi watu wengine. Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha iliyomkemea mtoto kwa vile alizoea kuwatusi watoto wengine katika jamii ya Abagusii ni:

*Embua yao yokona korama abana bande nembe. Naende nigo okobarama ase amang'ana amabe naende yobosoku akogechia abanto bonsi. Rero iga, tiga kobarama abana bande, gwakana amang'ana amaya gochia ase abanto bande.*

(Tabia yako ya kuwatusi watoto wengine ni mbaya. Pia, unawatusi kwa kutumia lugha ya aibu inayozua fedheha na chukizo kwa watu wengine. Hivi leo, koma kuwatusi watoto wengine, zungumza lugha nzuri kwa watu wengine).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu za mawasiliano ya mfano wa lugha hii

ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto aliyezoea kuwatusi watoto wengine katika jamii ya Abagusii. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumfahamisha mtoto huyo kuwa kitendo hicho kilisababisha mafarakano katika jamii ya Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kumshauri mtoto huyo kujiepusha na tabia ya kuwatusi watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

### **3.11.5 Kumkemea mtoto aliyepigana na watoto wengine**

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walipigana na watoto wengine katika jamii ya Abagusii tazama 2.1.10. Mfano wa lugha iliyotumika kumkemea mtoto aliyepigana na watoto wengine katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one tiga embua yokobarwania abana bande. Kwanarire kera ritiko kobarwania abana bande. Rituko erimo ngochia ore kobanga kogenda kobarwania, omanyeye goakwa osinywe gotara aiga naria. (Mwanangu, wacha kupigana na watoto wengine. Umezoea kupigana na watoto wengine kila wakati. Siku moja utapanga kwenda kupigana nao, kisha utapigwa na kutembea hapa na pale).*

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto aliyepigana na watoto wengine. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumwonyesha mtoto huyo kuwa kitendo hicho hakikubaliki katika jamii ya



Abagusii. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo kumshauri mtoto huyo kuhusu umuhimu wa kuwapenda watoto wengine katika jamii ya Abagusii.

### **3.11.6 Kumkemea mtoto aliyeoa au kuolewa**

Utafiti huu pia ulibainisha kuwa kuna baadhi ya watoto walioa au kuolewa katika jamii ya Abagusii tazama 2.1.12. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto iliyomkemea msichana kwa vile aliolewa na mwanamume aliyemzidi umri katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one, kondetera ore obosoku ase ngoeta egekogera aye gwachorire gotiga gosoma na gochora konyuomwa na omogaka omogotu bwe emiaka emerongo etano ebere.* (Mwanangu, unaniletea aibu mahali popote nipitapo kwa sababu umeamua kuacha kusoma na kuamua kwenda kuolewa na mzee wa miaka sabini).

Mhimili wa tano wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na sababu za mawasiliano. Sababu ya mawasiliano ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ilitumika katika kumkemea mtoto msichana aliyeolewa. Wanajamii walitumia lugha hiyo kwa lengo la kumweleza mtoto huyo kuwa kuolewa kabla ya kufikisha umri uliokubalika ni chukizo kwa wazazi wake na jamii nzima. Aidha, wanajamii walitumia lugha hiyo katika kutoa ushauri kwa mtoto huyo kurudi kwao na kuendelea na masomo yake.

### **3.12 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia dhima za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Dhima zilizobainishwa na kuchanganuliwa ni: kuelimisha, kukuza maadili,

kuonya, kurekebisha tabia, kuwasiliana, kubembeleza, kusifu, kufariji, kulinganisha, kuhimiza, na kukemea. Sura inayofuata imechunguza athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

## **SURA YA NNE**

### **ATHARI ZA LUGHA ILIYOWASILISHA TASWIRA YA MTOTO KATIKA JAMII**

#### **YA ABAGUSII**

#### **4.0 Utangulizi**

Katika sura ya tatu, dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii imejadiliwa, huku mifano kadhaa ikitolewa. Sura hii imebainisha athari ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Uchanganuzi huu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Mihimili ambayo ilichangia katika ubainishaji wa athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ni pamoja na mada iliyozungumziwa. Mada mbalimbali zilizozungumziwa na wanajamii kwa mtoto zilisababisha athari kadhaa kwa mtoto kama vile kukasirishwa kwa mtoto. Mtoto huyo aliyekuwa na hasira aliamua kutenda vitendo ambavyo vilizua chukizo kwa wanajamii kama vile kuhama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi kwa majirani au marafiki zake. Aidha, mada zilizozungumziwa zilisababisha mtoto kutenda mambo mazuri katika jamii kama vile kuwa na tabia nzuri iliyowafurahisha wanajamii. Mada zilizohusu tabia zilishughulikia jinsi mtoto alivyostahili kuwa na nidhamu katika jamii.

Mhimili mwingine wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliochangia katika kubainisha athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ni ule uliohusu muktadha wa mazungumzo. Ikiwa kwa mfano kifo cha mzazi kilitokea katika familia, athari yake ilikuwa mtoto huyo alihuzunika. Aidha, mtoto huyo aliweza kuomboleza kifo hicho kwa kulia au kuwaza na kuwazua kuhusu maisha ya siku za baadaye. Wanajamii walitumia

lugha ya faraja kama njia ya kumnasua mtoto huyo kutoka kwa athari hiyo ya kuhuzunika maishani mwake.

Mhimili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliohusu wahusika katika mazungumzo pia ulitumika katika kubainisha athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Wahusika waliozungumza walikuwa vijana au watu wazima katika jamii. Mhusika aliyezungumziwa alikuwa mtoto katika jamii. Aidha, mhusika aliyedhihirisha athari za lugha iliyowasilisha taswira yake ni mtoto aliyehusika katika mawasiliano hayo. Mhimili uliohusu wahusika ulichangia pakubwa katika kuchunguza jinsi watoto walivyozungumziwa na kubainisha athari zilizoibuka kutokana na mawasiliano hayo.

Sababu za mawasiliano pia ni mhimili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano uliotumika kubainisha athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mhimili huu ulichangia pakubwa katika kubainisha sababu kadhaa za mazungumzo kwa mtoto katika jamii ya Abagusii. Mfano wa mtoto aliyekuwa mgonjwa, wanajamii waliwasiliana na mtoto huyo kwa lengo la kufahamu alivyohisi katika maisha yake. Baada ya mawasiliano hayo, wanajamii waliweza kubainisha athari zake. Mfano wa athari ya lugha hiyo ni kuwa mtoto aliweza kukata tamaa ya kuishi katika dunia.

Athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii zilizobainishwa katika utafiti huu ni za mtoto: kuhama kutoka nyumbani kwao, kutelekezwa, kubaguliwa, kukata tamaa, kuchanganyikiwa akili, kuwa na tabia mbaya, kupendwa, kukubalika, kuchangamka na kuwa na tabia nzuri.

## **4.1 Kuhama**

Kutokana na matumizi ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii, utafiti huu ulibainisha kuwa watoto kadhaa walihama kutoka makwao na kwenda kuishi kwingineko. Sababu ni kuwa walihisi kuwa lugha iliyotumika kwao iliwasababishia aibu na matatizo mengi. Mfano wa lugha hiyo katika jamii ya Abagusii ni mtoto aliyehama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi; katika mji wa Kisii, kwa majirani, kwa makao ya kutunza watoto wasiojiweza na kwa marafiki zake.

### **4.1.1 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi katika mji**

Mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya katika jamii ya Abagusii tazama 2.1.5 alikemewa na kisha aliamua kuhama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika mji wa Kisii. Mfano wa lugha iliyosababisha kuhama kwake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anchete konywa amarwa kera rituko. Naende, goetera ase okonywa amarwa kare omwana, ere nigo akoreta eburaburu ase enka, ere tamenyeti mwabo, nigo amenyete orwao ase omochie Obosongo.* (Mtoto huyu anapenda kunywa pombe kila siku. Pia, mazoea yake ya kunywa pombe bado akiwa mtoto, yalisababisha mafarakano nyumbani kwao kisha akaamua kuhama na kwenda kuishi katika mji wa Kisii.

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawsiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya ni aliamua kuhama kutoka nyumbani kwao na kwenda

kuishi katika mji wa Kisii. Mtoto huyo aliamua kufanya hivyo baada ya kukemewa na wazazi wake kuwa aliwasumbua na kusababisha vurugu nyumbani kwao.

#### **4.1.2 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi kwa jirani**

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto yatima tazama 2.1.3 aliyekuwa akiishi na mjane, pia mamake wa kambo, alihama na kwenda mahali pengine baada ya lugha iliyowasilisha taswira yake kumkera. Mfano wa lugha iliyosababisha mtoto kuhama na kwenda kuishi kwa majirani katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo entakana otabwati baibori baye ere mbosa. Gekogera tari gokora meremo ende yonsi, ere tankonyeti gento kende. Mbuya nakwa, imotindeke na kweba tamenyeti ense eye. Kobua komenya amo nere akona koria endagera yane nkogora chibesa chinyinge.* (Mtoto huyu yatima ambaye hana wazazi wake ni bure kabisa hapa nyumbani. Sababu ni kuwa hafanyi kazi yoyote wala hanisaidii chochote. Ni heri afe, nimzike na kusahau kuwa hayuko duniani. Kuliko kuishi naye kwa vile yeye hula chakula kingi kinachonighalimu pesa nyingi).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto yatima alipokemewa na mama yake wa kambo ni aliamua kuhama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi kwa majirani. Mtoto huyo yatima aliamua kufanya hivyo baada kuteswa kwa muda mrefu na mama yake wa kambo. Hatua ya mtoto huyo yatima kwenda kuishi kwa majirani zake ilimwezesha kupokea malezi bora.

#### **4.1.3 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi katika makao ya watoto**

Mtoto aliyekuwa yatima tazama 2.1.3 aliyekasirishwa na lugha iliyowasilisha taswira yake, alimua kuhama na kwenda kuishi katika makao ya kuwalea na kuwatunza watoto wasiojiweza karibu na mji wa Kisii. Mfano wa lugha iliyosababisha kuhama kwake kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika makao ya kuwalea na kuwatunza watoto katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo entakana nigo are omorwaire mono. Nigo anchandete aiga inka egekogera nigo agosaa na koroka. Naende, ere nigo are omoreu mono, nigo ngosaba nakwa mbuya erio ngoke na koigwa buya na gotimoka egekogera tindi korara botuko.* (Mtoto huyu yatima ni mgonjwa sana. Ananisumbua hapa nyumbani kwa sababu yeye anahara na kutapika. Aidha, amekonda sana ni heri afe nifurahi na kupumzika kwa sababu ananisumbua hata sipati lepe la usingizi usiku).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto mgonjwa ni alihama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika makao ya kuwalea na kuwatunza watoto wasiojiweza karibu na mji wa Kisii. Mtoto huyo aliamua kufanya hivyo baada ya kuwa mgonjwa kwa muda mrefu bila kupokea matibabu yoyote. Aidha, mtoto huyo aliamua kuishi katika makao hayo ya kuwalea na kuwatunza watoto kwa vile alihitaji kupokea matibabu. Mtoto huyo vilevile alitarajia kupokea malezi bora na msaada kutoka kwa watu wengine katika jamii ya Abagusii.

#### **4.1.4 Mtoto aliyehama nyumbani kwao na kuishi kwa rafiki**

Mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini tazama 2.1.4 aliamua kwenda kuishi na marafiki zake walioishi katika mazingira ya utajiri. Mtoto huyo aliamua kuhama kutoka kwao baada ya kuzungumziwa kwa lugha iliyowasilisha taswira yake kuwa aliishi katika mazingira ya umaskini. Mfano wa lugha iliyosababisha kuhama kwake kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi kwa marafiki zake walioishi katika mazingira ya utajiri katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo amenyete ase enka ebwate obotaka. Nigo achandegete ase obogima bwaye egekogera akobeka amanchanchabe na nigo areete egekogera tari konyora endagera akoria. Boigo, enyomba bamenyete yaisire kobagwera.* (Mtoto huyu anaishi katika mazingira ya umaskini. Anasumbuka katika maisha yake kwa sababu anavalia matambara na amekonda kwa vile anakosa lishe inayostahili. Aidha, nyumba wanayoishi hivi karibuni itawaangukia).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii ilikuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyeishi katika mazingira ya umaskini ni alihama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi kwa marafiki zake. Mtoto huyo aliamua kuhama na kuishi na marafiki zake walioishi katika mazingira ya utajiri. Aidha, mtoto huyo aliamua kufanya hivyo alipogundua kuwa waliishi katika mazingira ya umaskini. Marafiki zake walimsaidia vitu mbalimbali kama vile nguo, vyakula, mahali pazuri pa kulala na nyumba nzuri ya kuishi.



## 4.2 Kutelekezwa

Kuna baadhi ya watoto waliotelekezwa katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu ulibainisha kuwa mojawapo ya sababu iliyosababisha wao kutelekezwa ni lugha iliyowasilisha taswira yao katika jamii ya Abagusii. Mfano uliodhihirika wazi ni mtoto zeruzeru aliyetelekezwa na wazazi wake. Wazazi hao walishikilia msimamo kuwa walikuwa wameandamwa na laana kutoka kwa mababu wao. Aidha, baadhi ya familia ziliwatelekeza watoto waliokuwa walemavu. Wazazi waliomtelekeza mtoto mlemavu waliamini kuwa kama waliendelea kuishi na mtoto huyo wangepata shida nyingi wakati wa kumlea na kumtunza. Utafiti huu ulibainisha kuwa watoto waliotelekezwa katika jamii ya Abagusii ni zeruzeru, mlemavu na mgonjwa.

### 4.2.1 Mtoto zeruzeru aliyetelekezwa na wazazi wake

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto zeruzeru alitelekezwa na wazazi wake katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo tazama 2.1.10 iliyosababisha kutelekezwa kwake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo taikeraneti ase risanku riaye. Nigo are omobariri burure buna omosongo. Naende risanku riaye tirimwameti buna eriabana bande. Ekeri kiomobaso, nigo agosinywa korora buya. Boigo, nigo akweyagia chingaki chiomobaso. Bwango iga, abarogi na abanyamesira nigo bakobagora babaita na chinyama chiabo chiarosigwa amariogo. Abaibori bande nigo bakobaira are babatiga aroro bare nobwoba na gosemeria buna eyio nenchera yogoseria ebirecha ebibe bikobachanda korwa ase enka. (Mtoto huyu ana kasoro katika ngozi yake. Yeye ni mweupe kama mzungu. Ngozi yake si nyeusi kama ya watoto wengine.*

Wakati wa jua kali, anakuwa na shida ya kuona vizuri. Aidha, anajikuna wakati wa jua kali. Hivi karibuni, wachawi na waganga walihitaji zeruzeru kwa vile wanawaua na kutumia nyama zao kutengeneza hilisi. Wazazi wengine wanawapeleka mbali, wakiwa na woga kisha kuwatelekeza watoto hao kwa vile wanaamini kuwa wanaleta laana katika familia na ni njia mojawapo ya kufukuza mapepo wanaowasumbua).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto zeruzeru ni alitelekezwa na wazazi wake. Mtoto huyo alitelekezwa kwa vile ngozi ya mwili wake ilikuwa tofauti na ya watoto wengine. Aidha, jamii ya Abagusii iliamini kuwa mtoto huyo zeruzeru aliwaletea laana katika jamii ya Abagusii. Wazazi wa mtoto huyo zeruzeru nao waliamini kuwa kumtelekeza mtoto wao zeruzeru ni hatua nzuri ya kujiepusha na laana ambazo ziliwaandama siku za baadaye.

#### **4.2.2 Mtoto mlemavu aliyetelekezwa na wazazi wake**

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa, baadhi ya watoto walemavu walitelekezwa katika jamii ya Abagusii. Wazazi waliomtelekeza mtoto mlemavu waliamini kuwa ni laana kwa familia yao kwa vile alikuwa na kasoro katika viungo vya mwili wake. Aidha, wazazi wake waliamini kuwa kumtelekeza mtoto huyo mlemavu ni uamuzi bora kwa vile walijipumzisha kutokona na majukumu ya kumlea na kumtunza. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto mlemavu aliyetelekezwa katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are aremarete tari buna abana bande. Nigo aretwa na abaibori baye bakamotiga ase ng'ina moke bakagenda komenya orwao. Nigo bateba omwana*

*obo nigo akobaretera obosoku obonene ase abanto bande. Naende boigo, ase enka yabo nigo barabwo bagoteba buna baragereriwe goetera ase omwana obo koba ekerema. Abaibori baye bachorire komotiga na batebire ng'a tibatageti komenya amo nere.* (Mtoto huyu ni mlemavu hafanani na watoto wengine. Aliletwa na wazazi wake kisha wakamwacha kwa shangazi yake wakaenda kuishi mahali kwingine. Walisema kuwa mtoto wao amewaletea aibu kubwa kwa watu wengine. Aidha, wao wanasema kuwa mtoto mlemavu anawaletea laana katika familia yao. Wazazi wake waliamua kumtelekeza na hawataki kuishi naye).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto mlemavu ni alitelekezwa na wazazi wake. Wazazi wa mtoto huyo mlemavu walimtelekeza kwa vile viungo vya mwili wake vilikuwa tofauti na vya watoto wengine. Aidha, wazazi wake walimtelekeza kwa vile waliamini kuwa mtoto huyo aliwaletea laana katika familia yao. Wazazi wa mtoto huyo vilevile waliamua kumtelekeza mtoto huyo mlemavu kwa sababu walipitia changamoto nyingi za kumlea na kumtunza.

#### **4.2.3 Mtoto mgonjwa aliyetelekezwa na wazazi wake**

Pia, wazazi wa mtoto mgonjwa tazama 2.1.1 walimtelekeza mtoto wao kwa vile waliona kuwa aliwasumbua hasa kumshughulikia kila wakati. Walilalamika kuwa wao walitumia wakati wao mwingi kumshughulikia. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto mgonjwa aliyetelekezwa katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo omorwaire tari gotokonya kende gionsi ase enka. Ere nigo atochandete nigo tokona komobogoria gochia ase atagete. Nigo ere buya komoira are nakomotiga aroro erio nario toratimoke korwa chigurube chinyinge chiokomorera na komorenda ase enka yaito.* (Mtoto huyu hatusaidii kitu chochote hapa nyumbani. Anatusumbua kwa vile hubebwa hapa na pale. Ni vyema kumchukua mbali na kumwacha pale ili tupumzike kutokana na majukumu mengi ya kumlea na kumtunza katika familia yetu).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto mgonjwa ni alitelekezwa na wazazi wake. Alitelekezwa na wazazi wake walioamua kufanya hivyo kwa vile mtoto huyo alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu. Aidha, wazazi wa mtoto huyo waliamua kufanya hivyo kama njia ya kujiepusha naye ili wasiendelee kumshughulikia kila siku. Wazazi wake vilevile waliona wazo hilo kuwa nzuri kwa vile iliwapunguzia mzigo wa kununua dawa za bei kila siku.

### **4.3 Kubaguliwa**

Vilevile utafiti huu ulibainisha kuwa, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha baadhi ya wazazi kuwabagua watoto wao. Ubaguzi huo ulijitokeza wazi pale walezi wa watoto hao na wazazi waliwabagua watoto kwa kuzingatia lugha hasi na chanya iliyotumika katika kuwasilisha taswira zao. Mifano iliyobainika wazi katika utafiti huu ni kubaguliwa kwa mtoto kwa kuzingatia walivyofanya kazi, mazingira waliyoishi na walivyofaulu katika mitihani.

#### **4.3.1 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia bidii**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii iliwabagua watoto kwa kuzingatia bidii walipofanya kazi. Mtoto aliyekuwa na bidii tazama 2.2.5 alibaguliwa kutoka kwa mtoto aliyekuwa mzembe tazama 2.1.11. Mfano wa lugha iliyowasilisha ubaguzi huo katika jamii ya Abagusii ni:

*Morusie omwana oyio ogokora omokia ase egasi yaye agokora korwa ase omwana omwabo ore omworo. Bamochanie babe amo, nigo aramoite omoyo erio takora emeremo yaye nomokia buna enaretie botambe.* (Mtenge mtoto huyo mwenye bidii kutoka kwa ndugu yake aliye mzembe. Wakiendelea kukaa pamoja, atamkatiza moyo wa kufanya kazi yake kwa bidii kama alivyo mazoea ya kufanya kazi yake kwa bidii).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefanya bidii ni alibaguliwa kwake kutoka kwa watoto wengine waliokuwa wazembe katika jamii ya Abagusii. Sababu ya ubaguzi huo ni kumkinga asije akashawishika kuwa mzembe kama wao katika jamii ya Abagusii.

#### **4.3.2 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia mazingira aliyoishi**

Aidha, utafiti huu ulibainisha ubaguzi kati ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri tazama 2.2.8 na mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini tazama 2.1.4. Mfano wa lugha iliyowasilisha ubaguzi huo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyio nigo amenyete ase enka ere yobotenenku, moatanane tabaisa gosanga nabana bande bamenyete buya egekogera barabwo nigo bare abataka batabwati*

*kende*. (Mtoto huyo anaishi katika mazingira ya utajiri, mtenganishe asishirikiane na watoto wanaoishi vizuri kwa vile yeye anaishi katika mazingira ya umaskini na hata kwao hawana kitu chochote).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya utajiri ni kubaguliwa kwake kutoka kwa watoto wengine walioishi katika mazingira ya umaskini. Mtoto huyo alibaguliwa kutoka kwa watoto wengine kwa vile aliishi katika mazingira ya kupendeza. Shabaha ya ubaguzi huo ilikuwa kumtenga mtoto huyo asishirikiane na watoto walioishi katika mazingira ya umaskini kwa vile wangemsumbua kutafuta msaada kutoka kwake.

#### **4.3.3 Mtoto aliyebaguliwa kwa kuzingatia matokeo ya mitihani**

Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa watoto walibaguliwa kwa kuzingatia matokeo ya mitihani. Mtoto aliyekuwa mwerevu alibaguliwa kutoka kwa mtoto aliyekuwa mjinga. Watoto hao walibaguliwa kwa kuzingatia walivyofaulu katika mitihani yao. Mfano wa lugha iliyobainisha ubaguzi huo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana one aye kore omong'aini, naende okoigwa bwango, nigo kogosemia buna tobaisa konara kogosoria amo na abana abariri. Gokogosoria na kobuta amo nabarabwo, nigo orabe omwana omoriri buna barabwo.* (Mwanangu wewe ukiwa mwerevu, tena unaelewa mambo haraka, ninakushauri kuwa usiwe na mazoea ya kucheza na watoto wajinga. Ukicheza na kukaa nao, nawe pia utakuwa mtoto mjinga kama wao).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliyowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefanya vizuri katika mitihani ni kubaguliwa kutoka kwa watoto wengine. Mtoto huyo mwerevu alibaguliwa kutoka kwa watoto waliokuwa wajinga kwa sababu alifanya vizuri katika mitihani yake. Aidha, mtoto huyo mwerevu alibaguliwa kutoka kwa watoto wajinga kwa vile hawakuwa na uwezo wa kutoa mchango wowote wa kusuluhisha tatizo lolote pia walifanya vibaya katika mitihani yao. Wanajamii vilevile waliamini kuwa kama mtoto mwerevu aliendelea kushirikiana na watoto wajinga naye angeshawishika kuwa kama wao.

#### **4.4 Kukata tamaa**

Utafiti huu ulibainisha kuwa baadhi ya watoto walikata tamaa maishani mwao kutokana na matumizi ya lugha iliyowasilisha taswira zao. Mtoto alikata tamaa kwa vile lugha iliyowasilisha taswira yake ilimkera. Mfano wa lugha hiyo ulibainika wazi katika lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekata tamaa ya kuishi duniani, aliyekata tamaa ya kuendeleza masomo yake shuleni na aliyekata tamaa ya kupata nafuu baada ya kuwa mgonjwa kwa muda mrefu.

##### **4.4.1 Mtoto aliyekata tamaa ya kuishi**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini tazama 2.1.4 alikata tamaa ya kuishi katika dunia. Mtoto huyo alikata tamaa kwa vile alikosa vyakula, mavazi na mahali pazuri pa kuishi katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekata tamaa maishani mwake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo amenyete ase enka ebwate obotaka. Tibabwati ndagera ende yonsi bararie kera rituko, tibamenyeti ase enyomba engiya naboigo nigo akobeka amanchanchabe. Nigo akororekana buna bwerusirie moyo. Nigo akona gosaba buna nakwa mbuya erio atimoke korwa ase emechando emenge emonchokanaine. (Mtoto huyu anaishi katika mazingira ya umaskini. Hawana chakula chochote wanaweza kula kila siku, hawaishi katika nyumba nzuri na vilevile anavalia nguo zilizo matambara. Anaonekana kuwaamekata tamaa ya kuishi. Anaendelea kuomba kuwa ni vizuri akate roho ili apumzike kutoka kwa shida nyingi zinazo mzingira).*

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini ni alikata tamaa ya kuishi katika dunia. Mtoto huyo aliamua kukata tamaa kwa vile aliishi katika mazingira ya umaskini. Aidha, aliamua kufanya hivyo kwa vile alisumbuka kupata mahitaji muhimu ya maisha. Mtoto huyo aliomba kuwa ni heri kufa badala ya kuendelea kuishi katika dunia hii akiandamwa na shida za kuishi katika mazingira ya umaskini katika jamii ya Abagusii.

#### **4.4.2 Mtoto aliyekata tamaa ya kuendeleza masomo**

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyefanya vibaya katika mitihani yake alikata tamaa ya kuendeleza masomo yake shuleni. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo ere nigo agokora bobbe ase amasomo aye. Ekero bagokora amatemwa ase ekerasi kiaye ere nigo akoba bwomoerio. Ere mbosa naende nigo akondetera*



*obosoku, emeremo amanyete buya nokoria endagera Atari gokora omokia ase amasomo aye.* (Mtoto huyu anafanya vibaya katika masomo yake. Darasani wanapofanya mitihani huwa wa mwisho. Yeye ni bure na ananiletea aibu, kazi anayotenda vyema ni kula chakula bila kutia bidii katika masomo yake).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefanya vibaya katika mitihani ni alikata tamaa ya kuendeleza masomo shuleni. Mtoto huyo alikata tamaa kwa vile alipata alama za chini katika mitihani yake. Aidha, mtoto huyo alikosa matumaini yoyote katika maisha yake kwa alikemewa na wazazi wake kuwa alifanya vibaya katika masomo. Utafiti huu ulibainisha kuwa wazazi wake walipoendelea kumtusi mtoto huyo, aliamua kutenda vitendo vilivyosababisha kero katika jamii ya Abagusii kama vile kujinyonga. Mtoto huyo vilevile alikata tamaa kwa sababu aliona kuwa hakuna haja ya kuendelea kuishi kwa shida duniani. Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto huyo alipoambiwa kufanya kazi alikubali shingo upande. Aliamini kuwa hakuna umuhimu wowote wa kufanya kazi ambayo haitamsaidia kitu chochote maishani mwake.

#### **4.4.3 Mtoto aliyekata tamaa ya kupona**

Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyekuwa mgonjwa kwa muda mrefu alikata tamaa ya kupona. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa mgonjwa kwa muda mrefu aliyekata tamaa ya kupata nafuu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are omorwaire mono. Orwarire ase emiaka emenge. Abanyagitari aoao batemire komorwaria basinyirwe. Natemire komoa amariogo aoao nyore emete*

*yorosana bwangire kogwena. Buna akororekana, okure omoyo buna takogwena korwa ase oborwaire bokomochanda.* (Mtoto huyu ni mgonjwa sana. Ameugua kwa miaka mingi. Madaktari mbalimbali wamejaribu kumtibu wameshindwa. Nimejaribu kumpa dawa kadhaa hata ya miti shamba bado hajapona. Yamkini, amekata tamaa ya kupona kutoka kwa maradhi yanayomsumbua).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasilino ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto mgonjwa ni alikata tamaa ya kupona. Mtoto huyo alikata tamaa ya kupona kwa sababu aliugua kwa muda mrefu bila kupata nafuu. Japo mtoto huyo alihudumiwa na madaktari mbalimbali na kupewa dawa za kienyeji, afya yake ilizidi kudhoofika. Maisha hayo ya kuugua kwa muda mrefu yalisababisha mtoto huyo kukata tamaa ya kupata nafuu.

#### **4.5 Kuchanganyikiwa akili**

Utafiti huu vilevile ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha baadhi ya watoto kuchanganyikiwa katika akili zao. Mfano ni lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetenda mambo yaliyoleta chukizo katika jamii kama vile kupigana tazama 2.1.9 au kuiba tazama 2.1.6. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyechanganyikiwa akili katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo agokora ebinto bikogechia abanto bande. Nigo abwate embua na enaro yokobarwania abana bande, naboigo nigo akobaibera abanto ebinto biabo. Omwana oyo nakwa nigo ndagoke egekogera ochandire emiaka emenge. Nomokurera atige chisegi na oboibi tari koigwa.* (Mtoto huyu anatenda mambo

yanayoleta chukizo kwa watu wengine. Ana tabia na mazoea ya kupigana na watoto wengine, vilevile anawaibia watu vitu vyao. Mtoto huyu akifa nitafurahi kwa vile amenisumbua kwa miaka mingi. Hata ukimwonya asipigane wala kuiba hakubali kufanya hivyo).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Eyhnografia ya mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyechanganyikiwa akili ni alitenda mambo mabaya katika jamii ya Abagusii. Mtoto huyo aliyechanganyikiwa akili alitenda mambo kama vile aliwatusi watoto wengine, alipigana na watoto wengine na alisababisha mafarakano. Utafiti huu ulibainisha kuwa kuwa mtoto huyo alichanganyikiwa akili kwa vile hakuzingatia mila na desturi za jamii ya Abagusii.

Aidha, utafiti ulibainisha kuwa watoto kadhaa nao walichanganyikiwa katika akili zao kwa vile wazazi wao walitumia lugha ya matusi katika kuwasilisha taswira zao katika jamii ya Abagusii. lugha hiyo ya matusi ilichangia pakubwa katika kuchanganyikiwa akili baadhi ya watoto katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha hiyo ya matusi iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekataa kufanya kazi katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo ogosire ase ogotakora emeremo namotebetie. Negechigwe nere, ekeru okomorigereria nigo anga omorogi.* (Mtoto huyu amekosea kwa kutofanya kazi niliyomwagiza kufanya. Nimekasirishwa naye ukimtazama yeye ni kama mchawi).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii ya matusi iliyotumika kwa

mtoto huyo, ilimfanya kuchanganyikiwa katika akili yake. Alichanganyikiwa akili wakati alifananishwa na mtu mchawi katika jamii ya Abagusii. Mchawi ni mtu aliyetenda vitendo viovu wakati wa usiku kama vile kuwaroga watu. Aidha, mtoto huyo alitenda vitendo vya ajabu kama vile kukusanya takataka ovyoovyo, kurobokwa na maneno ovyoovyo na kuzungumza kwa sauti akiwa peke yake.

#### **4.6 Tabia mbaya**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii, ilisababisha mtoto aliyekuwa na tabia nzuri kuibadilisha na kuwa mbaya. Baadhi ya wazazi na walezi wa watoto walitumia lugha ya matusi katika mazungumzo yao ya kila siku. Mfano wa mtoto aliyebadilisha tabia yake ni yule aliyeishi na wazazi waliozoea kutumia lugha ya matusi kwa watoto waliotenda mambo mabaya katika familia.

##### **4.6.1 Mtoto aliyekuwa na tabia nzuri aliyemua kuwa na tabia mbaya**

Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyekuwa na tabia nzuri alishawishika kuwa na tabia ya kuwatusi watoto wengine. Mfano wa lugha ya matusi iliyotumiwa na wazazi kwa mtoto aliyetanda mambo mabaya kama vile wizi na kupigana na watoto wengine iliyosababisha mtoto aliyekuwa na tabia nzuri kuibadilisha na kuwa na tabia mbaya katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate chimbua chingiya agwo ritang'ani. Nyuma yogohegigwa nabana bande, bwango iga nigo ere abarama amang'ana yobosoku naende akabogoria amagena na kobaruta obwate obororo obonge.* (Mtoto huyo alikuwa na tabia nzuri hapo awali. Baada ya kuchokozwa na watoto wengine, aliamua kuwatusi

kwa kutumia maneno ya aibu na pia alibeba mawe na kuwarushia akiwa na uchungu mwingi).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyekuwa na tabia nzuri ni aliibadilisha na kuwa mbaya. Mtoto huyo aliyewapenda watu wengine na kuwasiliana nao kwa lugha nzuri, alibadilisha tabia yake na kuwa na tabia mbaya ya kuwatusi na kuwapiga watoto wengine. Mtoto huyo alibadilisha tabia yake baada ya kuiga lugha hiyo ya matusi kutoka kwa wazazi wake kisha naye akaitumia kwa marafiki zake.

#### **4.6.2 Mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini aliyeamua kuwa mwizi**

Aidha, mtoto aliyeishi katika mazingira ya umaskini, japo alikuwa na tabia nzuri, alilazimika kuwa mwizi kwa vile alikosa vitu kadhaa nyumbani kwao. Mfano wa lugha iliyowasilisha tabia yake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo amenyete ase enka ebwate obotaka. Tari konyora endagera akoria kera rituko. Boigo, tabwati chianga chingiya, nigo akweboyia amanchanchabe. Nabo are omwana omuya, otatiga obotaka babwate ase enka yabo bwagerire ochakire kobaibera abanto bande ebinto biabo.* (Mtoto huyu anaishi katika mazingira ya umaskini. Hapokei mlo wake wa kila siku. Aidha, hana nguo nzuri, anavalia matambara. Yeye ni mtoto aliye na tabia nzuri, ingawa umaskini walio nao katika familia yao umechangia yeye kuwaibia watu vitu vyao).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyeishi katika mazingira ya umaskini ni alimua kuwa mwizi. Mtoto huyo aliamua kufanya hivyo kwa vile alikosa mahitaji muhimu ya kila siku. Japo mtoto huyo alikuwa mwaminifu mwanzoni, alilazimika kubadilisha tabia hiyo na kuwa mwizi. Alianza kuwaibia watu vitu vyao kama njia mojawapo ya kujinasua kutoka kwa maisha ya umaskini.

#### **4.7 Kupendwa**

Pia, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii athari yake ilikuwa mtoto alipendwa na wazazi wake. Mtoto huyo alipendwa na wazazi wake kwa vile alifanya mambo yaliyowafurahisha wanajamii. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na kipaji maalumu tazama 2.2.1 ilimfanya mtoto huyo kuipendwa na wanajamii na kusifiwa. Mtoto huyo alipendwa na kusifiwa na wanajamii kwa vile alikuwa na kipawa maalumu cha kuelewa na kufanya mambo haraka alipolinganishwa na watoto wengine katika jamii. Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyependwa kwa vile alikuwa na kipaji maalumu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo tomwanchete mono egekogera ere nigo abwate ekegwa kiabene. Ekeru okomobwekani amo nabakegoria kiaye, ere nigo akoigwa bwango ase egiotagete agokorere. Naende nigo agokora kende gionsi okomotebia bwango kobua abana bande. Naende boigo, nigo tomwanchete egekogera ere nigo akobatang'anera abana bande ase amasomo. (Mtoto huyu tunampenda sana kwa vile ana kipawa maalumu. Ukiemlinganisha na watoto wengine wa rika yake, utagundua kuwa darasani yeye anaelewa mambo kwa haraka kazi yoyote anayoambiwa kufanya na*

mwalimu wake. Vilevile mtoto huyu tunampenda kwa sababu anaelewa haraka darasani anawatangulia wanafunzi wengine).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliyowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo ni alipendwa na wanajamii. Mtoto huyo alipendwa katika jamii kwa vile alikuwa na kipawa maalumu cha kuelewa mambo haraka. Aidha, mtoto huyo alisifiwa na wanajamii kwa vile alikuwa na kipawa maalumu cha kuelewa mambo haraka alipolinganishwa na watoto wengine waliokuwa na umri sawa na mtoto huyo.

#### **4.8 Kukubalika**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto vilevile athari yake ilikuwa mtoto alikubalika katika familia na jamii yake. Mtoto huyo alikubalika kwa vile alitenda mambo mema yaliyowafurahisha wanajamii wote. Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha hiyo ilizungumzwa kwa upole na wazazi na walezi. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekubalika ulidhihirika wazi katika mtoto aliyekuwa na nidhamu tazama 2.2.3 katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo ilimfanya mtoto huyo kukubalika katika familia yake na jamii ya Abagusii.

##### **4.8.1 Mtoto aliyekubalika katika familia**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto aliyekuwa na afya kukubalika katika familia. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na afya tazama 2.2.4 iliyosababisha mtoto huyo kukubalika katika familia yake ni:

*Omwana oyo nigo are nomosasoko chingaki chionsi, asengencho abwate omobere ore omoikeranu. Naende boigo, omwana oyo nigo are nomogoko, anchete kona goseka chingaki chionsi. Nabo omwana oyo tomorendete buya. Nigo tokoenekia kera chingaki narendire buya tabaisa koba na bokong'u bonde bwensi ase obogima bwaye. (Mtoto huyu ni mchangamfu kila wakati, sababu ni kuwa ana afya na mwili uliokamilika. Aidha, mtoto huyu ana furaha, anapenda kutabasamu kila wakati. Tunamtunza vizuri ili asipatwe na madhara yoyote katika maisha yake).*

Mhimili wa pili wa nadharia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyekuwa na afya ni alikubalika katika familia yake. Aidha, mtoto huyo alijawa na furaha kwa vile alitimiziwa haja zake zote na wazazi wake. Mtoto huyo vilevile alichangamka kwa vile alitunzwa kwa njia nzuri na wazazi wake.

#### **4.8.2 Mtoto aliyekubalika katika jamii**

Aidha, mtoto aliyekuwa na nidhamu tazama 2.2.3 alikubalika katika jamii ya Abagusii. Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo are umuya ase egesaku giaito. Nigo are omwana obwate amasikani gochia ase abanto bande. Naende, nigo tomoigwerete buya koba nere ase enka yaito, egekogera chimbua chiaye nigo chire chingiya mono chikogokia abanto bonsi. Nigo tokomokorera kende gionsi atagete ase engecho are nechimbua chiokogokia. (Mtoto huyu ni mzuri katika jamii yetu. Yeye ni mtoto aliye na nidhamu kwa watu wote. Aidha, tunamfurahia kuwa naye hapa nyumbani mwetu, kwa vile ana*



tabia nzuri inayowafurahisha watu wote. Tunamtendea yote anayohitaji kwa vile tabia yake ni ya kupendeza).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyekuwa na nidhamu ni alikubalika katika jamii ya Abagusii. Mtoto huyo alikubalika kwa vile alikuwa na nidhamu. Aidha, wanajamii walimfanya mtoto huyo kuwa kielelezo katika jamii. Wanajamii waliwahimiza watoto wengine kuiga mfano wake.

#### **4.9 Kufurahi**

Pia, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto kuwa na furaha. Mtoto huyo alifurahi kwa vile alitenda mambo mema yaliyokubalika katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto aliyefalu katika mitihani yake alifurahi. Pia, mtoto aliyekuwa na nidhamu alifurahi baada ya kusifiwa na wanajamii wote.

##### **4.9.1 Mtoto aliyefurahi kwa kufaulu katika mitihani**

Utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefaulu katika mitihani yake ilisababisha mtoto huyo kuwa mchangamfu. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyechangamka kwa vile alifaulu katika mitihani yake katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo okorire buya ase amatemwa aye onsi. Ere nigo aba oyobweritang'ani ase ese esukuru yaye. Boigo, nigo akora buya ase amatemwa aye nakoba bweritang'ani ase chisukuru chionsi chigotoka ase ekaunti ya Kisii. Nigo aichire nomogoko na omosasoko omonge ase engencho aeta buya ase amatemwa aye. (Mtoto*

huyu amefanya vizuri katika mitihani yake yote. Alikuwa mwanafunzi wa kwanza katika shule yake. Aidha, alifanya vyema katika mitihani yake akawa wa kwanza katika shule zote zinazopatikana katika kaunti ya Kisii. Amejawa na furaha na kuchangamka tele kwa kufaulu kwake katika mitihani).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyefaulu katika mitihani yake ni alifurahi. Mtoto huyo alifurahi baada ya kufaulu katika mitihani yake. Pia, mtoto huyo alijawa na furaha tele baada ya kumiminiwa sifa kutoka kwa wanajamii. Wanajamii vilevile walifurahishwa na mtoto huyo kwa sababu alikuwa mwenye nidhamu.

#### **4.9.2 Mtoto aliyefurahi kwa kuwa na nidhamu**

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyekuwa na nidhamu tazama 2.2.3 katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto huyo kufurahi. Mfano wa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyefurahi kwa vile alikuwa na nidhamu katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo abwate amasikani gochia ase abanto bonsi ase agesaku kiabagusii. Nigo agotogigwa nabanto bonsi ase engecho yechimbua chiaye chingiya. Nigo asasogete na kogoka chingaki chionsi ase engencho agotogigwa ande onsi agoeta. (Mtoto huyu ana nidhamu kwa watu wote katika jamii ya Abagusii. Watu wote wanamsifu kwa sababu ya tabia yake nzuri. Amechangamka na kufurahi kila wakati kwa vile anamiminiwa sifa tele kila mahali anapita).*

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto huyo aliyekuwa na nidhamu ni alifurahi. Mtoto huyo alifurahi kwa vile alikuwa na nidhamu. Alipendwa na kumiminiwa sifa tele kutoka kwa wanajamii hali iliyosababisha mtoto huyo kufurahi katika maisha yake. Aidha, mtoto huyo alitumika kama kielelezo kwa watoto wengine waliohimizwa kuiga tabia yake.

#### **4.10 Tabia nzuri**

Lugha ilyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto huyo kuacha tabia yake mbaya na kuwa na tabia nzuri. Utafiti huu ulibainisha kuwa hiyo ilifanyika pale mtoto aliyezungumziwa na walezi wake aliamua kubadilisha mwenendo wake. Mfano wa lugha hiyo ni ile iliyotumika kwa mtoto aliyeamua kuolewa tazama 2.1.12 katika jamii ya Abagusii. Mfano wa lugha iliyomshawishi atoke kwa mvulana aliyemwoa na kurudi kwao katika jamii ya Abagusii ni:

##### **4.10.1 Mtoto aliyerudi nyumbani kwao baada ya kuolewa**

Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ilisababisha mtoto msichana aliyeolewa na mwanamume aliyemzidi umri tazama 2.1.12 kurudi kwao na kuendelea na masomo yake shuleni. Utafiti huu ulibainisha kuwa mfano wa lugha hiyo katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo atiga kogenda esukuru agachora konywomwa. Abaibori baye batemire buna bakonyara komosemia buna ere nomwana omoke otaraika emiaka agwenerete gosoka. Boigo, nabo arabaise koba morito gose anyore oborwire buna enyamoreo kare omoke. Nyuma yogosemiwa na abaibori baye, ere bwanchire airane*

*sobo. Naende, bwancheranire kogendereria namasomo aye. Ochorire boigo koba nechimbua chingiya naende ababoririe abaibori baye bamwabere.* (Mtoto huyu aliacha kwenda shuleni na kuamua kuolewa. Wazazi wake wamejaribu kumshauri kuwa yeye ni mtoto mdogo ambaye hajafikisha umri wa kuolewa. Pia, mtoto huyu anaweza kuwa mjamzito au kupokea ugonjwa wa ukimwi akiwa na mdogo. Baada ya kushauriwa na wazazi wake, amekubaliana nao kuwa atarudi kwao. Aidha, ameamua kuendelea na masomo yake. Aameamua vilevile kuwa na tabia nzuri na kuwaomba wazazi wake msamaha).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografi ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyeolewa ni aliamua kuwa na tabia nzuri. Mtoto huyo alibadilisha tabia yake kwa kuamua kurudi nyumbani kwao baada ya kuolewa na mwanamume aliyemzidi umri. Aidha, mtoto huyo alimua kurudi shuleni na kuendeleza masomo yake.

#### **4.10.2 Mtoto aliyeacha tabia ya kuiba**

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto aliyekuwa mwizi tazama 2.1.6 kuacha tabia hiyo ya kuwaibia watu vitu vyao. Mfano wa lugha iliyotumika katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo arenge nyamoibi simbiri. Nigo anarete kobaibera abanto bande ebinto biabo. Boigo, nigo anarete kogenda ase emegondo yabanto bande obaibera ebimeri biabo. Nyuma yabaibori baye komosemia, rero iga otigire kobaibera na koba omwana omuya. Ekeru atagete gento kende gionsi nigo akobasaba abanyene.* (Mtoto

huyu alizoea kuwa mwizi hodari. Alizoea kuwaibia watu vitu vyao. Aidha, alizoea kuiba mazao kutoka mashamba ya watu. Baada ya kushauriwa na wazazi wake, hivi leo ameacha kuwa mwizi na kuwa mtoto aliye na tabia nzuri).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ulihusu kila uwasilishaji wa ujumbe huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto mwizi ni aliamua kuwa na tabia nzuri. Mtoto huyo aliyezoea kuwaibia watu vitu vyao aliamua kuacha tabia hiyo na kuwa mwenye tabia nzuri. Aidha, mtoto huyo alishauriwa kuwa alipokuwa na haja ya kitu chochote maishani mwake, alistahili kumwomba mwenyewe na wala si kukichukua kwa siri.

#### **4.10.3 Mtoto aliyeacha tabia ya kupigana na watoto wengine**

Pia, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ilisababisha mtoto aliyezoea kupigana na watoto wengine tazama 2.1.9 kuacha tabia hiyo. Mfano wa lugha iliyotumika katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo arenge omochege bwanchete korwania abana bande ase esukuru agosoma. Boigo, nyore ninka sobo nabo anarete kobarwania abana bamwabo. Nyuma yabaibori baye komosemia atige embua eyio, bwanchire bono iga koba omwana omuya. Nomoaka gose komorama tari gokora kende nigo agokira kiri. Reroiga obeire omwana omuya tari korwania onde bwensi.* Mtoto huyu alikuwa mchokozi na aliyependa kupigana na watoto wengine shuleni. Aidha, alizoea kupigana na ndugu zake nyumbani kwao. Baada ya kushauriwa na wazazi wake kuwa aiache tabia hiyo, amekubali kuwa mtoto aliyea na tabia nzuri. Ukimchapa au

kumtusi hafanyi jambo lolote anakimya tu. Hivi leo amekuwa mtoto aliye na tabia nzuri hapigani na mtu yeyote.

Mhimili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe uliowasilishwa huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliye pigana na watoto wengine ni aliamua kuwatendea mema. Mtoto huyo aliyezoea kupigana na watoto wengine aliamua kuwapenda. Pia, utafiti huu ulibainisha kuwa mtoto huyo aliamua kuwapenda watu wengine katika jamii ya Abagusii. Watoto wengine walipomchokoza aliamua kutojibu asije akapigane nao tena.

#### **4.10.4 Mtoto aliyeacha tabia ya kutumia pombe na dawa za kulevya**

Vilevile, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ilisababisha mtoto aliyezoea kutumia pombe na dawa za kulevya tazama 2.1.5 kuacha tabia hiyo. Mfano wa lugha iliyotumika katika jamii ya Abagusii ni:

*Omwana oyo nigo anarete konywa amarwa na gotinda. Boigo, nigo anarete gotumia amariogo yogotindia ase engaki etambe nakogera oreta eburaburu ase enka yabo.*

*Nyuma ya abaibori baye komosemia, rero iga otigire konywa amarwa na amariogo yogotindia. Obeire omwana omuya otabwati buraburu ende yonsi ase enka yabo.*

(Mtoto huyu alizoea kunywa pombe na kulewa. Aidha, alizoea kutumia dawa za kulevya kwa muda mrefu na kusababisha ghasia nyumbani kwao. Baada ya kushauriwa na wazazi wake, hivi leo ameacha kunywa pombe na kutumia dawa za kulevya. Amekuwa mtoto mwenye tabia nzuri ambaye hasababishi ghasia yoyote nyumbani kwao).

Mhimili wa pili wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ulihusu kila ujumbe huwa na athari. Athari ya mfano wa lugha hii iliyowasilisha taswira ya mtoto aliyetumia pombe na dawa za kulevya ni aliamua kuacha kutumia pombe na dawa za kulevya. Mtoto huyo aliyekuwa na tabia mbaya aliamua kuwa na tabia nzuri. Pia, mtoto huyo aliamua kuishi bila kuwasumbua watu katika jamii ya Abagusii.

#### **4.11 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Athari zilizobainishwa na kuchanganuliwa ni mtoto: kuhama, kutelekezwa, kubaguliwa, kukata tamaa, kuchanganyikiwa akili, kuwa na tabia mbaya, kupendwa, kukubalika, kufurahi na kuwa na tabia nzuri. Sura inayofuata ni hitimisho la utafiti huu na imeshughulikia muhtasari, matokeo, changamoto, mchango na mapendekezo ya utafiti huu.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO**

#### **5.0 Utangulizi**

Sura hii ni muhtasari wa mchakato wote wa utafiti. Imetoa muhtasari wa utafiti kwa kuzingatia; suala la utafiti, malengo, mbinu za utafiti, matokeo, maoni na mapendekezo ya tafiti za baadaye ambazo misingi yao ni utafiti uliofanywa. Mapendekezo hayo yanaweza kuwapa watafiti wengine ari ya kutafakari na kuona iwapo wanaweza kuendeleza tafiti mbalimbali. Sura hii imechanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Matokeo yamehusisha vigeu vyote vya utafiti huu. Azma ya utafiti huu ni kuchunguza dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Sura hii basi imepanga data katika makundi kuambatana na madhumuni yanayohusiana na lugha ambayo imetumika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Data imechanganuliwa na mtafiti ili kuondoa utata wowote. Uchanganuzi umefanywa kwa kutumia maelezo ili kuweka mada wazi.

#### **5.1 Muhtasari**

Utafiti huu umelenga kubainisha dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Ili kubainisha lugha hiyo, taswira mbalimbali za mtoto zimechanganuliwa na kuangaza jinsi zimechangia katika ukuaji wa mtoto. Aidha, dhima na athari za lugha hiyo zimechanganuliwa. Kupokea data ya utafiti huu, mtafiti aliwahoji watu sabini na wawili (72). Mtafiti alitumia mbinu ya kimakusudi kuwateua na kuwahoji watu wawili kutoka kila kikundi; watoto, vijana, watu wazima, naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto kutoka kila wodi sita (6) zifuatazo; Bobaracho, Kisii ya Kati,



Keumbu, Kiogoro, Birongo na Ibeno kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache linalopatikana katika ugatuzi mdogo wa Kisii ya Kati, Kaunti ya Kisii kuwakilisha jamii pana ya Abagusii.

Mbinu

Kwa kutumia mihimili yote ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano, mtafiti aliweza:

- i) Kutambua lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
- ii) Kubainisha dhima za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.
- iii) Kuchunguza athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Tasnifu hii imewasilishwa kwa sura tano. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa utafiti imeshughulikia mada ya utafiti, maswali na malengo ya utafiti pamoja na kueleza kuhusu sababu zilizomchochea mtafiti kufanya utafiti huu. Vilevile, upeo na mipaka ya utafiti imebainishwa. Kisha mtafiti amejadili yaliyoandikwa kuhusu mada na kueleza jinsi tafiti hizo zimechangia katika kufanikisha utafiti huu. Aidha, mtafiti amejadili kuhusu nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano iliyoongoza utafiti huu na jinsi mihimili yote ya nadharia hiyo imechangia katika kufanikisha utafiti huu. Sura imehitimishwa kwa kuangazia mbinu za utafiti zilizotumika katika kutekeleza utafiti huu.

Sura ya pili imeshughulikia lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Imebainika wazi kuwa lugha hasi na chanya zilitumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Lugha hasi na chanya iliyobainishwa imefafanuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Lugha hasi imejadiliwa kwanza kisha lugha chanya imejadiliwa baadaye. Mifano kadhaa ya

matumizi ya lugha hasi na chanya iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii imetolewa.

Sura ya tatu imeshughulikia ubainishaji wa dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Dhima iliyobainishwa imefafanuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Imebainika wazi kwamba lugha hiyo imetumika katika kuwasilisha taswira ya kila mtoto katika jamii ya Abagusii. Aidha, imebainika wazi katika utafiti huu kuwa lugha hiyo ina dhima. Utafiti huu vilevile umebainisha kuwa lugha hiyo imetumika katika kutoa maelezo ya kina kumhusu mtoto yeyote aliyepatikana katika jamii ya Abagusii. Lugha hiyo pia, ni muhimu kwa vile inajenga na kuamua maisha ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Pia, lugha hiyo imechangia katika kutoa mielekeo, maoni na matendo ya watu wazima kwa watoto katika jamii ya Abagusii. Utafiti huu kadhalika umebainisha kuwa lugha hiyo imechangia jinsi mtoto anavyokua hadi atakapokuwa mwenye umri wa makamo. Pia, lugha hiyo inamwezesha mtoto kuimarika katika maisha yake na kuishi maisha mema yakilinganishwa na maisha yake ya siku za nyuma katika jamii ya Abagusii.

Athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii zimebainishwa katika sura ya nne. Athari zilizobainishwa zimefafanuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano. Aidha, athari hizo zimefafanuliwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa kwa mtoto. Imebainika wazi kuwa athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni mtoto; kuhama, kutelekezwa, kubaguliwa, kukata tamaa, kuchanganyikiwa akili, kuwa na tabia

mbaya, kupendwa, kukubalika, kufurahi na kuwa tabia na nzuri. Kadhalika, mifano kadhaa ya athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii imetolewa.

Sura ya mwisho ni hitimisho la utafiti huu na imeangazia muhtasari wa masuala mbalimbali katika kila sura. Baada ya muhtasari kubainishwa, sura hiyo vilevile imeshughulikia matokeo ya utafiti huu, matatizo ya utafiti huu na changamoto zilozomkabili mtafiti zimebainishwa. Kadhalika, mchango wa utafiti huu umebainishwa katika sura hiyo ya tano. Isitoshe, mapendekezo kwa wasomi au watafiti wengine yamejadiliwa kwa kubainisha maeneo ya isimujamii yaliyohitaji kutafitiwa ili kuyaziba mapengo yaliyopo katika matumizi ya lugha kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Abagusii.

## **5.2 Matokeo**

Utafiti huu umeazimia kubainisha lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Aidha, utafiti huu umebainisha dhima na athari za lugha hiyo katika jamii ya Abagusii. Baada ya kufanya utafiti huu, matokeo yaliakisi kwamba lugha hasi na chanya hutumika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Lugha hasi ni ile iliyoashiria kuwa mtoto alikuwa katika hali ya kusikitisha au alitenda jambo baya lililosababisha kero kwa wanajamii. Lugha hasi iliyobainishwa katika utafiti huu ni ya mtoto aliyekuwa; mgonjwa, mlemavu, yatima, aliyeishi katika mazingira ya umaskini, aliyetumia pombe na dawa za kulevya, mwizi, aliyefanya uasherati, aliyewatusi watoto wengine, aliyepigana na watoto wengine, zeruzeru, mzembe, aliyeoa au kuolewa, aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu na aliyetelekezwa na wazazi wake. Lugha chanya ni ile iliyosababisha wanajamii kumkubali na hata kumtukuza mtoto kwa vile alitenda jambo zuri. Lugha chanya

iliyobainishwa katika utafiti huu ni ya mtoto aliyekuwa na; kipaji maalumu, furaha, nidhamu, afya, bidii, ujasiri, aliyeishi katika mazingira ya utajiri na aliyependa kucheza.

Pia, imedhihirika wazi kuwa lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii si sawa kwa watoto wote. Lugha hiyo ilitumika katika mawasiliano baina ya mtoto na; watoto wengine katika jamii, wazazi wake, walezi wa mtoto, vijana, na watu wazima katika jamii ya Abagusii. Matumizi ya lugha hiyo katika mawasiliano ya kila siku, yalitofautiana kutoka mtoto mmoja hadi mwingine. Lugha hiyo hasa ililenga kutoa maelezo kuhusu taswira ya mtoto aliyezungumziwa. Lugha hasi na chanya zilitumika katika kutoa maelezo ya kina kuhusu taswira hasi na chanya za mtoto ambazo zilipatikana katika jamii ya Abagusii. Ilibainika vilevile kuwa taswira hizo hasi ni zile ambazo hazikubaliki kamwe katika jamii ya Abagusii. Baadhi ya watoto waliokuwa na taswira hizo waliweza kutengwa kwa vile iliaminika kuwa walileta chukizo na laana kubwa katika familia zao na hata katika jamii nzima. Imedhihirika wazi pia kuwa mtoto aliyekuwa na mojawapo ya taswira hizo huenda alipotoshwa na marafiki zake au aliandamwa na laana zilizotokana na mambo mabaya yaliyotendwa na wazazi au mababu zao siku za nyuma katika jamii ya Abagusii. Hivyo basi familia husika ilifanya juhudi kuwasiliana na mtoto huyo wakiwa na lengo la kumweleza kuhusu tabia yake. Aidha, lugha hiyo ilitumika katika kuwatahadharisha watoto wengine wajiepushe pale ilipowezekana kuwa na taswira hizo maishani mwao.

Dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii vilevile imebainishwa katika utafiti huu. Imebainika wazi kuwa mtoto aliweza kupokea mambo kadhaa ya manufaa yaliyomsaidia katika maisha yake. Dhima iliyodhihirika wazi katika utafiti huu iliyomsaidia mtoto maishani mwake ni; kumwelimishwa kuhusu mambo muhimu katika jamii, kupitisha

ujumbe kuhusu atakavyoweza kukuza maadili katika jamii, kumwonya mtoto kuhusu mambo mbalimbali aliyostahili kuwa makini nayo maishani kama vile kujiepusha na ngono. Pia, lugha hiyo ilitumika katika kurekebisha tabia ya mtoto aliyetenda mambo mabaya katika jamii ya Abagusii.

Aidha, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ilitumika katika kuwasiliana na mtoto kuhusu mada mbalimbali kama vile dini, mila au desturi, kumbembeleza mtoto hasa wakati alikataa kufanya jambo aliagizwa kufanya kama vile kwenda shuleni kusoma, kumsifu mtoto alipofanya kitendo kizuri kama vile kufanya majukumu aliyopewa na wakubwa wake ilivyostahili, kumfariji mtoto hasa wakati alikumbwa na mabaya kama vile kifo cha mpendwa wa karibu kama vile baba, mama, kaka au dada aliowategemea katika kupokea mahitaji yake muhimu ya kila siku kama vile; vyakula, mavazi na makazi.

Lugha hiyo pia, ilitumika katika kumlinganisha mtoto aliyezungumziwa na watoto wengine katika jamii. Sababu ya kumlinganisha mtoto huyo na watoto wengine ni kuwa ilisaidia pakubwa hasa kuboresha tabia yake. Lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto vilevile ilitumika kumhimiza mtoto aliyefanya majukumu aliyopewa vyema katika jamii ya Abagusii kama vile; masomo shuleni, kufanya vizuri kazi yoyote aliyopewa nyumbani kama vile; kuosha vyombo, kufua nguo au kuwalisha mifugo. Kadhalika, lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto ilitumika katika kumkemea mtoto hasa alipofanya jambo lolote ambalo ni kero kwa familia na hata jamii yote kama vile; mtoto aliyekuwa na tabia ya kuwaibia wanajamii vitu vyao, mtukutu au aliyejiunga na magenge ya majambazi yaliyowasumbua wanajamii.

Athari za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii zimebainishwa katika utafiti huu. Mawasiliano kwa kutumia lugha hiyo yalisababisha athari mbalimbali kwa mtoto. Utafiti huu ulibainisha kuwa athari hizo ni mtoto aliweza; kuhama kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi kwingine, kutelekezwa na wazazi wake, kubaguliwa katika familia, kukata tamaa, kuchanganyikiwa akili, kuwa na tabia mbaya, kupendwa, kukubalika, kufurahi na kuwa na tabia nzuri katika jamii ya Abagusii.

### **5.3 Changamoto**

Suala la utafiti huu limehusu dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Baada ya kufanya utafiti huu, imebainika kuwa baadhi ya wahojiwa hawakuwa tayari kutoa habari muhimu kuhusu lugha hiyo. Wahojiwa wengine walidhani kuwa mtafiti anajaribu kufanya upelelezi na hatimaye kufichua siri kuhusu watoto wao kwa watu wengine.

Wengine, hasa akina mama, walidai kuwa utamaduni wa Abagusii hauwaruhusu kuzungumzia watoto wao kwa watu ambao ni wageni kwao kwa vile walidhani kuwa huenda watoto wao wangekumbwa na shida siku za usoni. Aidha, wahojiwa wengine walichukulia kuwa watoto wao hasa wale waliofanya vyema kama vile katika masomo wangerogwa na hatimaye kufanya vibaya katika mitihani yao. Kutokana na tatizo hilo, mtafiti alilazimika kuwatafuta wasaidizi kutoa maelezo ya kina kuhusu azma ya utafiti huu. Wasaidizi hawa, hata hivyo, nao walikumbana na wakati mgumu kujaribu kuwashawishi wahojiwa ili watoe habari zilizohitajika. Wasaidizi hawa nao walidai malipo ya juu na mtafiti hakusita kutoa malipo hayo ili kufanikisha utafiti huu.

Changamoto nyingine ni kuwa baadhi ya wahojiwa walitoa maelezo yote kuhusu suala la utafiti wakitumia lugha ya Ekegusii, kisha mtafiti aliweza kutafsiri lugha hiyo kwa lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine ilikuwa vigumu kwa mtafiti kutafsiri lugha ya Ekegusii hadi lugha ya Kiswahili. Hali hii ilimlazimu mtafiti kuwatafuta wanajamii wenye tajriba pana katika lugha ya Ekegusii wamsaidie mtafiti kutafsiri lugha hiyo japo waliitisha malipo ya juu. Hata hivyo, wasaidizi hao walitoa msaada mkubwa katika kufanikisha utafiti huu.

#### **5.4 Mchango**

Mchango mkuu wa utafiti huu ni kwamba lugha imetumika na Abagusii kuwasiliana kuhusu mambo muhimu katika jamii. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyoshughulikiwa na lugha ni kuwasilisha taswira mbalimbali za watoto zinazopatikana katika jamii ya Abagusii. Aidha, imebainika wazi kuwa lugha teule iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni; hasi na chanya. Mtafiti ameweza kutumia mihimili ya nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano katika kuchanganua lugha hasi na chanya iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii.

Lugha hasi iliyochanganuliwa katika utafiti huu ni ya mtoto aliyekuwa na taswira zifuatazo; mgonjwa, mlemavu, yatima, aliyeishi katika mazingira ya umaskini, aliyetumia pombe au dawa za kulevya, aliyewaibia wanajamii vitu vyao, aliyefanya uasherati, aliyewatusi watu, aliyezoea kupigana, aliyezaliwa zeruzeru, aliyekuwa mzembe, aliyeoa au kuolewa, aliyeajiriwa kufanya kazi ngumu na aliyetelekezwa na wazazi wake. Aidha, utafiti huu

umechanganua lugha chanya ya mtoto aliyekuwa na taswira zifuatazo; kipaji maalumu, furaha, nidhamu, afya, bidii, mcheshi, ujasiri na aliyeishi katika mazingira ya umaskini.

Vilevile utafiti huu umebainisha kwamba dhima ya lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni: kuelimisha, kukuza maadili, kuonya, kurekebisha tabia, kuwasiliana, kubembeleza, kusifu, kufariji, kulinganisha, kuhimiza na kukemea mtoto. Utafiti huu pia umebainisha kuwa athari hasi za lugha iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ni; kuhama, kutelekezwa, kubaguliwa, kukata tamaa, kuchanganyikiwa kiakili na kuwa na tabia mbaya. Athari chanya zilizobainishwa katika utafiti huu ni; kupendwa, kukubalika, kuhisi salama, kufurahi, kutulia na kuwa na tabia nzuri.

### **5.5 Mapendekezo**

Utafiti huu umechanganua dhima ya lugha teule iliyowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Mtafiti hawezi kudai kuwa ameshughulikia yote yaliyomo kwenye sajili hii. Kuna mengine mengi ambayo hayajashughulikiwa kwenye utafiti huu na hata kwenye tafiti zilizotangulia. Mtafiti ameshughulikia taswira mbalimbali za watoto na lugha iliyowasilisha taswira hizo katika jamii ya Abagusii. Aidha, mtafiti ameshughulikia dhima na athari za lugha hiyo katika jamii ya Abagusii. Kuna sajili za lugha nyinginezo ambazo zinaweza kutafitiwa.

Aidha, mtafiti hakushughulikia suala la usanifu wa lugha iliyotumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii, jambo ambalo laweza kutafitiwa na watafiti wa baadaye. Vilevile utafiti huu ulijikita katika jamii ya Abagusii pekee, kuna pengo kwani kwa



uelewa wa mtafiti bado hakuna tafiti ambazo zimelinganisha lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii na ile inayopatikana katika jamii nyinginezo.

Utafiti huu ulitumia mihimili ya Ethnografia ya Mawasiliano. Kwa vile kuna mapengo baada ya kufanya utafititi huu, nadharia nyinginezo zinaweza kutumiwa katika kubainisha mada. Tafiti za baadaye zinaweza kujikita katika eneo lililochunguzwa au eneo lingine, kwa kufanya hivyo, huenda mambo mengine yakaibuka yenye uhusiano na mada hii ya utafiti. Utafiti huu umependekeza kuwa tafiti zijazo ziweze kubainisha tofauti au uwiano uliopo kati ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto wa kiume na kike katika jamii.

## MAREJELEO

- Alken, L. 1979. *Psychological Testing and Assessment (third edition)*. Boston: Allyn and Bacon.
- Aries, P. 1962. *Centuries of Childhood*. Harmondsworth: Penguin Books.
- Bauman, R. 1989. *Exploration in the Ethnography of Speaking: Studies in the social and cultural foundation of language*. New York: Cambridge University Press.
- Beeman, W. 1997. Communication. In: Barfield, T. (Ed.). *The Dictionary of Anthropology*. Oxford: Blackwell.
- Bellamy, C. 2002. *The State of the World's Children. UNICEF African Countries*. Nairobi: Heinrich Boell Foundation.
- Benedict, R. 1976. Continuities and Discontinuities in Cultural Conditioning. In: Arlene Skolnick (Ed.) *Rethinking Childhood: Perspectives on Development and Society*. (25) Boston: Little and Brown Company.
- Berelson, B. and G. Steiner. 1969. *Human Behaviour*. New York: Harcourt Brace.
- Bledsoe, C. 1989. The cultural meaning of AIDS and condoms for stable heterosexual relations in Africa: Recent evidence from the local printmedia. Paper presented at IUSSP seminar on Population Policy in Sub-Saharan Africa: Drawing on International Experience. Kinshasa, 27 Feb – 2 March.
- Brown, A. 2006. *Appropriate Language in Child and Youth*. In: Cyc – Online Magazine Page 34 – 38.
- Bryans, A. and J. Wolfendale. 1981. *Parental Involvement in Language Development*. Nairobi: Heineman Educational Publishers Ltd.

- Bundy, A. and G. Skard. 2008. The test of playfulness. L. D. Pharham and L. S. Facio (Eds), *Play in occupational therapy for children*. (2<sup>nd</sup> ed. pp 71 – 94). St. Louis, MO: Mosby.
- Cantwell, H. B. and D. A. Rosenberg. 1990. *Child Neglect*. Reno, NV: National Council of Juvenile and Family Court Judges.
- Cimpric, A. 2010. *Children Accused of Witchcraft and Theft. An anthropological Study of contemporary practices in Africa*. Dakar, Senegal: UNICEF.
- De Mause, L. 1976. *The History of Childhood*. London: Cambridge University Press.
- Ezra, B. 2007. *Child Rearing Among Abagusii Community*. In:  
<http://ezrabu.blogspot.com/2007/weaningtakeplaceinsecondandthird.html>  
 07/06/2017.
- Edmond, K., Z. Hill and B. Kirkwood. 2007. *Family and community practices that promote child survival, growth and development*. Geneva: WHO.
- Fasold, R. 1990. *The Sociolinguistics of Language*. Cambridge: Basil Blackwell.
- Finnegan, R. 2002. *Communicating*. London: Routledge.
- Fisher, E. P. 1992. The Impact of play on development: A meta – analysis in Play and Culture. *Play in occupational therapy for children* (2<sup>nd</sup> ed) pp 5, 159 – 181.
- Flynn, J. R. 2012. *Are We Getting Smarter? Rising IQ in the Twenty – First Century*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Freeman, J. 2010. *Gifted Lives: What Happens when Gifted Children Grow Up*. London: Routledge.
- Gleick, J. 2011. *Genius: The Life and Science of Richard Feynman*. (ebook ed.). London: Open Road Media.

- Goodale, A., I. Saunders and M. Sayer. 1999. The relationship between playfulness and coping in preschool children: A pilot Study. *American Journal of Occupational Therapy*, 53, 221 – 226.
- Gudgeon, C. 1991. “Politics and the language of child care.” In: *Journal of Child and Youth Care*: 20<sup>th</sup> January, 2006.
- Gregory, R. J. 1995. “Classification of Intelligence ” In Sternberg, R. J. *Encyclopedia of Human Intelligence*.
- Gumperz, J. J. and D. Hymes. 1972. *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. Oxford: Basic Blackwell Ltd.
- Herrington, S. and K. Studmann. 1998. Landscape interventions: New direction for the design of children’s outdoor play environments. *Landscape and Urban Planning*. 48(2 – 4), 191 – 205.
- Hunt, E. 2011. *Human Intelligence*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hunter, S. S. 1990. Orphans as a window on the AIDS epidemic in Sub-Saharan Africa: initial results and implications of a study in Uganda. *Social Science and Medicine*. 31, 6:681–690.
- Huston, A. C. 1991. *Children in Poverty: Child Development and Public Policy*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Hymes, D. 1962. *Ethnography of Speaking: Anthropology and Human Behaviour*. Washington D.C.: T. Gladwin and W. Sturtevant.
- Hymes, D. 1964. *Language in Culture and Society*. New York: Harper and Row Inc.
- Hymes, D. 1972. *Models of the Interaction of Language and Social Life: In Direction in Sociolinguistics*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

- Hymes, D. 1974. *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Hymes, D. 1996. *Ethnography, Linguistics, Narrative Inequality: Towards an Understanding of Voice*. Bristol P.A: Taylor and Francis.
- ILO. 2011. “*International and National Legislation – Child Labour*”. Geneva: ILO.
- ILO. 2012. *What is Child Labour?* Geneva. ILO.
- Ingstad, B. 1990. *The disabled person in the community: social and cultural aspects*. International Journal of Rehabilitation Research 13, 187 – 194.
- Jay, T. 1996. *What to Do When Your Students Talk Dirty*. San Jose: Resource Publications, Inc.
- Jelana, V. and N. Korac. 2003. A Roughly Mapped Terra Incognita: Images of the Child in Adult Oriented Media Contents. In Cecilia von Feilitzen & Ulla Carlson (Eds.). *Children and Media: Image, Education, Participation*. The UNESCO International Clearinghouse on Children and Violence on the Screen. 57 – 63.
- Jerop, S. and N. Oyori. 2002. *Portral of Disability through Personal Names and Proverbs in Kenya; Evidence from Ekegusii and Nandi*. In: [www.oyorijerop.portrayalofdisabilitythroughpersonalnamesandproverbs.html](http://www.oyorijerop.portrayalofdisabilitythroughpersonalnamesandproverbs.html). 13/02/2016 14:15.
- Kampaus, R. W. 2005. *Clinical Assessment of Child and Adolescent Intelligence (Second Edition)*. New York: Springer.
- Konner, M. 1991. *Childhood*. London: Little Brown Company Ltd.

- Korac, N. 1983. "Kids These Days..." A Seminar Researched and Presented by Young Journalists from Children's Express. 1999. In Cecilia von Feilitzen & Ulla Carlson (Eds.). *Children and Media. Image, Education, Participation*. The UNESCO. 23 – 33.
- Kunkel, D. and S. L. Smith. 1999. The News Media's Picture of Children in the United States. In Cecilia von Feilitzen & Ulla Carlson (Eds.). *Children and Media: Image, Education, Participation*. The UNESCO. International Clearinghouse on Children and Violence on the Screen. 39 – 51.
- Leathers, D. G. 1997. *Successful Nonverbal Communication, Principles and Application*. Boston: Allyn and Bacon.
- Lee, E. G. 2001. *Too White to Be Black and Too Black to Be White. Living with Albinism*. Bloomington IN: Author House.
- Levine, R. 1977. *Nyansongo: A Gusii Community in Kenya*. New York: Robert Krieger Publishing Co.
- Liles, B. L. 1975. *An Introduction to Linguistics*. Englewood Cliffs: Prentice Hall Inc.
- Lyons, J. 1977. *Semantics, Vol. 1*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Marcia, B. 2011. *The Image of the Child*. In:  
<http://www.marciaherbert.com/2011/09/theimageofthechild.html>  
 02/02/2017 13:25.
- Mayer, P. 1949. *The Lineage Principle in Gusii Society*. London: Oxford University Press.
- Mitchel, E. T. 2004. *Albinism in the Family*. Bloomington IN: Author House.
- MOH. 2005. *Basic Paediatric Protocols*. Republic of Kenya - Nairobi: MOH.

- Momanyi, J. N. 1996. *Politics and Nationalism in Colonial Kenya. The Case of Abagusii 1939 – 1963*. M. A. Thesis, Kenyatta University.
- Morreale, S. P. 2004. *Introduction to Human Communication*. Belmont: Wordsworth.
- Nalwanga, S. and J. Sengendo. 1987. Orphaned and disabled children in Luwero and Kabale Districts and in Ugandan child care institutions: A comparative profile to the general child population. Kampala: Makelele University.
- Nerlove, S. B. 1969. *Traits Dispositions and Situational Determinants of Behaviour Among Gusii Children of Southern Kenya*. Phd Thesis, Stanford University.
- O'Brien, J. 2000. The impact of occupational therapy on a child's playfulness. *Occupational Therapy in Health Care*, 12(2 – 3), 39 – 51.
- Ochieng, W. R. 1974. *A Pre-Colonial History of the Gusii of Western Kenya. C.A.D. 1500-1914*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Ozment, S. 2001. *The Loving Family in Old Europe*. Cambridge: Harvard University Press.
- Page, R. 1985. *Acts of Identity*. New York: Cambridge University Press.
- Pawson, E. and P, Tranter. 2001. *Children's access to local environments: A case study of Christ Church, New Zealand. Local Environment*, 6, 27 – 48.
- Phelan, J. 2001. "Notes on Using Plain Language in Child and Youth Care Work." CYC-ONLINE Issue 34. Nov. 2001, 25<sup>th</sup> Jan 2006.
- Pollock, L. H. 1983. *Forgotten Children: Parent – Child Relations from 1500 – 1900*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Sapir, E. 1949. *Language: An Introduction to the Study of Speech*. New York: Harcourt Brace and Company, Inc.

- Saville – Troike, M. 1982. *The Ethnography of Communication: An Introduction*. London: Basil Backwell publishers.
- Solley, B. A. 2005. *When Poverty's Children Write: Celebrating Strengths, Transforming Lives*. Portsmouth, NH: Heinemann, Inc.
- Spolsky, B. 1998. *Sociolinguistics*. Oxford: Oxford University Press.
- Stephenson, A. 2003. *Physical risk taking: Dangerous or endangered. EarlyYears: An International Journal of Research and Development*, 23, 35 – 43.
- TUKI. 2011. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: Oxford University Press.
- UNICEF. 1990. *Children and Aids: An Impending Calamity*. Paris: UNICEF.
- Wardhaugh, R. 1986. *An Introduction to Sociolinguistics*. Oxford: Basic Blackwell Ltd.
- WHO. 1993. *International Classification of Impairments, Disabilities and Handicaps*. Geneva – Switzerland: WHO.



## VIAMBATISHO

### KIAMBATISHO CHA 1

#### MAHOJIANO NYANJANI KWA WATU WAZIMA

**Maswali ya mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watu wazima kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii.**

Jina langu ni Robert Omuga Ombaye mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Maoni na mchango wako utatoa kuhusu suala hili utakuwa wa manufaa kwangu na wale watasoma kazi hii. Habari utakazonipa nitazihifadhi kwa siri na kuzitumia kwa ajili ya kufanikisha utafiti huu. Karibu.

1. *Banto ki banchete komokwanera omwana ase egesaku Kiomogusii ?* (Ni watu gani wanaopenda kumzungumzia mtoto katika jamii ya Abagusii?)
2. *Mbicha ki chiabana chigotoka ase egesaku Kiomogusii?* (Ni aina gani ya taswira za watoto zinazopatikana katika jamii ya Abagusii?)
3. *Nkwana ki chigokwanwa chikoorokia buya chibicha chia abana abwo gwantebia ase egesaku Kiomogusi?*(Ni aina gani ya lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii?)
4. *Emeremo emenene yechinkwana chikoera buya buna omwana akororekena ase egesaku kiomogusii nereri?* (Lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii ina dhima gani?)

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

## KIAMBATISHO CHA 2

### MAHOJIANO NYANJANI KWA MANAIBU WA MACHIFU, MACHIFU NA WATAALAMU WA HAKI ZA WATOTO

**Maswali ya mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na naibu wa machifu, machifu na wataalamu wa haki za watoto kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii.**

Jina langu ni Robert Omuga Ombaye mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Maoni na mchango wako utatoa kuhusu suala hili utakuwa wa manufaa kwangu na wale watasoma kazi hii. Habari utakazonipa nitazihifadhi kwa siri na kuzitumia kwa ajili ya kufanikisha utafiti huu. Karibu.

Jina lako \_\_\_\_\_

Umri wako \_\_\_\_\_

1. Wadhifa wako ni upi?
2. Ni kwa muda gani umehudumu katika wadhifa huo?
3. Baada ya kuhudumu kwa muda huo wote, ni taswira gani za watoto hupatikana katika jamii ya Abagusii?
4. Je, ni watu gani hutumia lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii?
5. Je, ni aina gani ya lugha hutumiwa katika kuwasilisha taswira mbalimbali za watoto ambazo umetaja katika jamii ya Abagusii?
6. Je, lugha inayowasilisha taswira mbalimbali za watoto katika jamii ya Abagusii inapotumika ina dhima gani?
7. Je, ni jinsi gani mtoto huathiriwa na matumizi ya lugha inayowasilisha taswira yake katika jamii ya Abagusii?

### KIAMBATISHO CHA 3

#### MASWALI YA MAHOJIANO NYANJANJANI KWA WATOTO NA VIJANA

**Maswali ya mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watoto au vijana kutoka eneo bunge la Nyaribari Chache, Kaunti ya Kisii.**

Jina langu ni Robert Omuga Ombaye mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Maoni na mchango wako utatoa kuhusu suala hili utakuwa wa manufaa kwangu na wale watasoma kazi hii. Habari utakazonipa nitazihifadhi kwa siri na kuzitumia kwa ajili ya kufanikisha utafiti huu. Karibu.

1. *Emiaka yao nerenga?* (Umri wako ni upi?)
2. *Aye nomworokiwa ore?* (Wewe ni mwanafunzi?)
3. *Kerasi irenga ogosoma?* (Unasoma darasa gani?)
4. *Inee, bicha ki chikoorokia abana ase egesaku kia Abagusii?* (Je, ni aina gani za taswira huwasilisha mtoto katika jamii ya Abagusii?)
5. *Inee, nkwana ki chikoorokia ebicha ya omwana ase egesaku kia Abagusii?* (Je, ni aina gani ya lugha inawasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii?)
6. *Emeremo emenene ye chinkwana chikoorokia ebicha y'omwana ase agesaku kiomogusii nereri?* (Je, lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii inapotumika ina dhima gani?)
7. *Inee, ekero omwana akwaneirwe buna akororekana ase egesaku kia Abagusii nki agokora?* Je, dhima ya lugha inayowasilisha taswir ya mtoto katika jamii ya Abagusii ni gani?

#### KIAMBATISHO CHA 4

### HOJAJI KWA WATOTO, VIJANA, WATU WAZIMA, MANAIBU WA MACHIFU, MACHIFU NA WATAALAMU WA HAKI ZA WATOTO KUTOKA ENEO BUNGE LA NYARIBARI CHACHE, KAUNTI YA KISII

Jina langu ni Robert Omuga Ombaye mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu dhima ya lugha teule katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii. Maoni na mchango wako utatoa kuhusu suala hili utakuwa wa manufaa kwangu na wale watasoma kazi hii. Habari utakazonipa nitazihifadhi kwa siri na kuzitumia kwa ajili ya kufanikisha utafiti huu. Karibu.

**Maagizo:** Weka alama ya ✓ kwenye kijisanduku kilicho mbele ya jibu sahihi.

1. Jina: \_\_\_\_\_
2. Jinsia: Mke  Mume
3. Umri wako: Miaka 13 - 19  Miaka 20- 30  Miaka 31- 40  Miaka 41 - 50   
Zaidi ya miaka 50
4. Kiwango cha elimu: Shule ya msingi  Shule ya upili  Chuo anuwai   
Chuo kikuu  Kingine (Eleza) \_\_\_\_\_
5. Kazi unayofanya: Mkulima  Mwalimu  Biashara  Daktari   
Nyingine (Eleza) \_\_\_\_\_
6. Je, ni taswira zipi za mtoto zinazopatikana katika jamii ya Abagusii?
  - a) Mtoto mzenbe
  - b) Mtoto zeruzeru
  - c) Mtoto mgonjwa
  - d) Mtoto yatima
  - e) Mtoto mcheshi
  - f) Mtoto mchangamfu

Nyingine (eleza) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

7. Je, ni aina gani ya lugha hututumika katika kuwasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii?

(a) Hasi

(b) Chanya

8. Je, ni aina gani ya lugha inayowasilisha taswira za watoto wafuatao?

(a) Mgonjwa (eleza) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

(b) Mzembe (eleza) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

(c) Mwenye afya (eleza) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

Nyingine (eleza) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

9. Je, lugha inayowasilisha taswira ya mtoto katika jamii ya Abagusii inapotumika ina dhima gani?

- (a) Kuelimisha
- (b) Kukuza maadili
- (c) Kuonya
- (d) Kurekebisha tabia

Nyingine (eleza) \_\_\_\_\_

---

---

---

---

---

10. Je, ni jinsi gani mtoto huathiriwa na matumizi ya lugha inayowasilisha taswira yake katika jamii ya Abagusii?

- a) Mtoto kuhama kutoka nyumbani
- b) Mtoto kutelekezwa
- c) Mtoto kubaguliwa
- d) Mtoto kukata tamaa

Nyingine (eleza) \_\_\_\_\_

---

---


---

---

---


# KIAMBATISHO CHA 5

Ramani ya Kenya inayoonyesha Kaunti ya Kisii



## KIAMBATISHO CHA 6

### Ramani ya Kaunti ya Kisii








KIAMBATISHO CHA 8

Ramani ya eneo bunge la Nyaribari Chache



KIAMBATISHO CHA 9

Ramani ya Wodi katika eneo bunge la Nyaribari Chache



# KIAMBATISHO CHA 10

Ramani ya mitaa midogo katika eneo bunge la Nyaribari Chache

